

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 4 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja, leo ni Kikao cha Arobaini na Tatu. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

MHE. MASHAURI M. NDAKI (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI):

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kwa niaba ya Mwenyekiti. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu.

Na. 360

Sharti la Kujiunga katika Vikundi ili Kupata Mikopo

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwahimiza wananchi wajiunge kwenye vikundi ili waweze kupata mikopo ya kuwasaidia kuendesha shughuli zao:-

Je, Serikali haoni kuwa sharti hilo linawakosesha fursa baadhi ya wananchi ambao pengine wanahitaji huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma za kifedha zinawafikia wananchi wake Serikali imetunga Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017 ambayo itawezesha kuchochea maendeleo stahiki na ubunifu wa huduma ndogo za kifedha ili kukidhi mahitaji halisi ya wananchi wa kipato cha chini na hivyo kuongeza ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Pia Serikali inalenga kutatua changamoto inayowapata wananchi juu ya mtazamo wa

mifumo ya ukopeshaji kwa vikundi au mtu mmoja mmoja. Sera hii itapelekea kutungwa kwa sheria itakayoweka utaratibu mzuri wa huduma ndogo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, utoaji mikopo kwa kutumia vikundi ni mfumo ambao hutumika kutoa mikopo midogo midogo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Mfumo huu hutumika kutoa mikopo kwa watu ambao uwezo wao wa kiuchumi ni mdogo, hasa kwa wakopaji ambao hawana dhamana. Pia mfumo huu husaidia kuweka dhamana mbadala ya usalama wa mikopo inayotolewa kwa kuwafanya wanakikundi kuwa na uwajibikaji wa pamoja juu ya mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umekuwa ukitumiwa na taasisi nyingi za kifedha ambazo zimekuwa zikitoa mikopo kwa watu wenye kipato cha chini ikiwepo mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inayomilikiwa na Serikali kutokana na faida yake katika kuhakikisha kuwa usalama wa mikopo hasa kwa wakopaji wasio na dhamana. Mfumo huu pia husaidia kurahisisha ufuatiliaji wa kuwajengea uwezo wanakikundi kupitia mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mfumo huu kutumika lakini ni pia mwananchi mmoja mmoja wamepatiwa fursa za uwezeshaji kupitia benki na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji kama vile Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi na Mfuko wa Wajasiriamali wadogo wadogo.

SPIKA: Mheshimiwa Kikwembe, swali la nyongeza.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kweli leo nimefurahi kidogo. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri amenijibu vizuri. Naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sera hii inalenga kutatua changamoto inayowapata wananchi kuhusu

mitazamo mbalimbali lakini umesema pia sera hii inalenga kuwakopesha wanavikundi na mtu mmoja mmoja, swali langu ni kwamba; ni kwa nini sasa Halmashauri nyingi zimekuwa zikiwalazimisha wananchi wakope wakiwa kwenye vikundi vya watu watano na kuendelea, jambo ambalo kimsingi linamnyima mkopaji mmoja mmoja mwenye uwezo wa kukopa ambaye anaweza akajidhamini ili aweze kujitendeleza katika maisha yake?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, naishukuru Serikali yangu kwa sababu imeweza kuondoa riba katika hii mikopo ambayo imekuwa ikitolewa na Halmashauri asilimia kumi, lakini, ni kwa nini sasa, bado tunasema kwamba, kwa mfano kwenye Mifuko ya Akinamama na Vijana, wazee na wanaume hawapati mikopo hii, jambo ambalo tunaweza tukawakopesha na wakaweza kuendeleza mifuko hiyo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kipengele cha kwanza alichouliza Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali lake anapendekeza ingefaa tukaanza kum-*address* mtu mmoja mmoja badala ya vikundi ambalo kimsingi na yeye mwenyewe atakubaliana na mimi na hata ukienda kule kwake, vikundi kwa maana ya ushirika ndiyo hasa njia ya kuweza kututoa sisi wanyonge. Naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kuwa vyovyote, yule ambaye ana uwezo wa kuweza ku-*access* mabenki, *window* hiyo ipo, lakini katika hii pesa ambayo inatolewa na Serikali ni vizuri kwanza tukajikita katika vikundi maana tukisaidia vikundi tunasaidia watu walio wengi zaidi.

SPIKA: Kwa lile la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Serikali inachokifanya ni kuona namna ya kuweza kuyagusa makundi yote kwa wakati mmoja. Ndiyo maana pamoja na kwamba tunayo Mifuko ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi lakini pia tunayo mifuko maalum kwa ajili ya akinamama na vijana, lakini kundi la wazee na watu wengine ambao hawadondokei katika sifa hizo, wenyewe pia kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wanayo fursa ya kwenda kukopeshwa mtu mmoja mmoja au kupitia vikundi pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba bado hata kama kuna mzee na mtu mwingine yeyote ambaye anahitaji kupata mikopo hii, hata kama hadondokei katika kundi la vijana na akinamama lakini fursa hiyo ipo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ipo 19 na imekuwa ikifanya kazi hiyo kuwawezesha wananchi kiuchumi.

SPIKA: Mheshimiwa Kemilembe nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kumekuwa kuna hamasa ya uhamasishaji mkubwa sana kwa wananchi wetu kujiunga na vikundi hivi ili waweze kupata mikopo hii asilimia 10 kutoka kwenye Halmashauri zetu, lakini kiuhalisia Halmashauri nyingi mikopo hii haitoki. Nataka kujua, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha Halmashauri zetu ili mikopo hii iweze kutoka na akinamama, wazee na watoto waweze kupata mikopo hii kama inavyoonekana?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa

Spika, swali hili limekuwa likijirudia mara kwa mara na majibu ambayo tumekuwa tukitoa, tumekuwa tukielekeza kwamba wakati tunakuja kuhitimisha bajeti kuna kipengele ambacho kitaingizwa katika *Finance Bill* ambacho kitamlazimisha kila Mkurugenzi kuhakikisha kwamba pesa hizi zinatengwa na zisipotengwa sheria zitachukuliwa ili kutoa adhabu kwa wale wote ambao hawatatimiza takwa hili la kisheria. Kwa sasa hivi, imekuwa ni kama *option* lakini tutakuja na kipengele ambacho kitamlazimisha kila Mkurugenzi *a-make sure* kwamba pesa hizi zinatengwa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu. Mheshimiwa Kadutu tafadhali.

Na. 361

**Shule za Mkindo na Ulyankulu Kupewa Hadhi ya
Kuwa na Kidato cha Tano na Sita**

MHE. JOHN P. KADUTU aliuliza:-

Kabla ya kuanzishwa Shule za Kata, kulikuwa na mpango wa kujenga shule katika tarafa. Kwenye Jimbo la Ulyankulu kulijengwa shule tatu ambazo ni Kashishi, Ulyankulu na Mkindo; Shule ya Kashishi hivi sasa ina kidato cha tano na sita:-

Je, ni lini Shule za Mkindo na Ulyankulu zitapewa hadhi ya kuwa na kidato cha tano na sita ili kuwapunguzia wanafunzi gharama za kufuata mbali masomo ya kidato cha tano na sita?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kwa ruhusa yako niondoe sentensi moja tu inayoanza na neno Tarafa mpaka pale mwisho na sita.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa, kila Tarafa angalau ina shule moja yenye kidato cha tano na sita. Mkakati ullopo kwenye maeneo ambayo tayari kuna shule zinazotoa elimu ya kidato cha tano na sita ni kuziimarisha kwa kuziwekea miundombinu, kuzipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuzipatia Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ili shule iweze kupandishwa hadhi na hatimaye kusajiliwa kama Shule ya Kidato cha Tano na Sita ni lazima itimize vigezo vifuatavyo:-

- (i) Iwe na miundombinu inayojitosheleza kama mabweni, madarasa, bwalo, jiko na maktaba;
- (ii) Iwe na huduma muhimu na za uhakika za maji na umeme; na
- (iii) Iwe na Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Shule za Sekondari Ulyankulu na Mkindo bado zina changamoto ya miundombinu isiyojitosheleza kama mabweni, madarasa, bwalo, jiko na maktaba. Hivyo, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ifanye jitihada za makusudi kuwezesha shule hizo mbili kufikia vigezo vinavyohitajika ili ziweze kusajiliwa. Aidha, kwa kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu pamoja na ile Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2018/2019 zimeshapitishwa na Bunge, itakuwa vigumu shule hizo kusajiliwa na kuanza kuchukua wanafunzi wa mwaka huo.

SPIKA: Mheshimiwa Kadutu, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa vile Naibu Waziri

ameona aondoe sentensi moja, mimi nasema *paragraph* yote majibu hayafanani na swali nililouliza. Mimi sitaki kuuliza maswali mengi, nimwombe tu Mheshimiwa Naibu Waziri au Mawaziri wote watatu wa TAMISEMI wafike Ulyankulu kujionea haya yaliyoandikwa, je ni kweli? Kwa sababu haya yote yaliyoandikwa si kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimwombe Naibu Waziri au wenzake waweze kufika Ulyankulu na kujionea kile wanachopewa na wataalam na je, ndicho kilichoko *site*?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Kakunda, leo umepiga Kisikongesikonge. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, naomba sana nimwombe Mheshimiwa John Kadutu, awepo Jimboni tarehe 10 Julai, ili tuweze kutembelea shule hizo kwa pamoja.

SPIKA: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, shule za sekondari za kidato cha kwanza mpaka cha nne Serikali imezipandisha hadhi baadhi yake kuwa shule za kidato cha tano na cha sita, kwa mfano, Kibakwe, Berege, Mazae na Kongwa Mjini. Hata hivyo, watoto katika shule hizi wanasoma katika mazingira magumu sana kwanza madarasa, hosteli pamoja na mabweni lakini hata chakula wanachopewa hela ni kidogo sana. Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu suala la kuboresha shule za *form five* na *six* katika kata hizi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza, yeye ni Mbunge mzoefu wa siku nyingi na kutokana na Ubunge wake ndiyo maana ameweza kupata maendeleo makubwa katika Jimbo lake hadi shule hizo alizozitaja zimesajiliwa kuwa katika hadhi ya kidato cha tano na sita. Kuwa na shule tatu au nne kwenye Jimbo moja za kidato cha tano na sita siyo kazi ndogo, ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jibu hili, napenda kujibu kwa ujumla kwamba shule zote za kidato cha tano na sita na hata za kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, zote zinapewa fedha sawasawa kwa nchi nzima. Kwa hiyo, haiwezekani kwa mfano tukasema kwamba, kwa sababu shule hizi sasa Mheshimiwa Mbunge amesema zina matatizo makubwa, basi tuziongezee shule zile za Jimbo lake tu, ni kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo, nakaribisha maoni kama haya ili tuweze kuyajadili kwa pamoja kwa ajili ya shule zote nchini badala ya shule moja moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Alhaj Bulembo nilikuona, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa swali la msingi la Ulyankulu liko katika Majimbo mengi ya nchi hii, kutokuwa na shule za *form five* na *form six*. Serikali inatoa *commitment* gani na lini itaanza kufanya *operation* katika kila jimbo kupata shule za *form five* na *form six*? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, maombi yaliyopo katika Wizara yetu ambayo sisi

tukiyapokea tunayapeleka Wizara ya Elimu kwa ajili ya usajili kwa sababu anayesajili ni Wizara ya Elimu ni mengi, lakini mengi yamekuja hivi karibuni, mwezi wa Nne mwishoni, mwezi wa Tano wakati tayari masuala ya bajeti yalikuwa yameshakamilika. Kwa hiyo, naomba sana nimwahidi Mheshimiwa Bulembo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na Bunge zima kwamba mwakani tutaweka utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba inavyofika Desemba, 2018, basi shule zote ambazo zina maombi maalum katika ofisi zetu za Serikali tutazisimamia ili ziweze kupata usajili.

SPIKA: Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu, mmepeleka maombi mwishoni sana. *(Kicheko)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimesimama kulihakikishia Bunge lako Tukufu Wizara yangu ambayo ndiyo ina jukumu la kusajili shule haina tatizo lolote la kusajili wakati wowote shule ambayo imekidhi vigezo. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Wakurugenzi na Maafisa Elimu kwa ujumla kama kuna shule ambayo inahitaji usajili, tunasajili wakati wowote ilmradi shule imekidhi vigezo. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tuendeleo na swali la Wizara hiyo hiyo ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, linaulizwa na Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula na kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Kafumu nimekuona.

Na. 362

Matengenezo ya Barabara ya Buhekela-Miswaki-Loya-Iyumbu

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU (K.n.y. MHE. MUSSA R. NTIMIZI) aliuliza:-

Barabara ya Buhekela-Miswaki-Loya-Iyumbu inaunganisha Majimbo ya Igunga, Manonga, Igagula na

Singida Magharibi, pia inaunganisha Mikoa miwili ya Tabora na Singida, ina Mbuga kubwa ya Wembele ambapo wananchi wanalima mpunga na kulisha Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida lakini ni mbovu sana:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuitengeneza barabara hiyo kwa umuhimu wake huo wa kiuchumi na kimawasiliano?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Buhekela-Miswaki-Loya-Iyumbu inahudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini (*TARURA*), katika Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga yenye kipande chenye urefu wa kilometa 102.79 ambayo ni barabara ya Igunga-Itumba-Simba na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwa maana ya Uyui yenye kipande chenye urefu wa kilometa 66.05 ambayo ni barabara ya Miswaki - Loya kilometa 28.68 na Loya-Nkongwa kilometa 37.37.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imepanga kufanya matengenezo ya muda maalum kilometa sita na matengenezo ya kawaida kilometa moja kwa gharama ya Sh.225,000,000. Mpaka sasa barabara zenye urefu wa kilometa sita zimeshachongwa na maandalizi ya kuziweka changarawe yanaendelea. Vilevile *TARURA* Halmashauri ya Igunga imepewa shilingi milioni 297 kwa ajili ya kujenga boksi kalvati tatu na kufanya matengenezo ya muda maalum kilometa 1.6.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ujenzi wa boksi kalvati tatu umefikia asilimia 30. Katika mwaka wa fedha 2018/2019

TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imetengewa Sh.165,000,000 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kilometa 23 na ujenzi wa boksi kalvati moja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (Uyui) imeidhinishiwa Sh.400,000,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya kilometa 20 kwa kiwango cha changarawe pamoja na kujenga kalvati moja. Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kafumu, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nakushuru. Swali la kwanza, kwa kuwa barabara hii ya Buhekela-Miswaki-Loya mpaka Iyumbu na ile barabara ya Igunga-Itumba-Simbo ni barabara ambazo zinapita kwenye Mbuga ya Wembele mahali ambapo ni lazima ujenge tuta kubwa ili barabara iwezekane siyo kuchonga, kwa hiyo, kuna madaraja mengi yanahitajika kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Sh.225,000,000 za barabara ya Iyumbu na zile Sh.297,000,000 za barabara ya Itumba hazitoshi kabisa kuzijenga barabara hizi. Waziri anatoa *commitment* gani kuhusu kuongeza bajeti ili kujenga hii barabara kwa kiwango ambacho zitaweza kupitika wakati wowote?

Swali la pili, kwa kuwa ile barabara ya Igunga-Itumba-Loya kipande cha Itumba - Loya hakina fedha, kwa sababu inaenda Simbo kwanza. Ni lini basi Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kile kipande cha Itumba-Loya?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, sijui hivyo vichocho vya Itumba-Loya huko unavifahamu Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, ni kweli swali hili amekuwa akiuliza sana kuhusu kipande hicho cha Mbuga ya Wembele ambayo inahitaji *special consideration* na ni ukweli usiopingika kwamba inahitaji bajeti kubwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali tunalitambua hili, lakini kinachogomba ni suala la bajeti, pale hali itakavyokuwa imeimarika hatutasahau kwa sababu eneo lile linahitaji pesa nyingi. Naamini katika bajeti zijazo, kabla hatujafika 2020 tutakuwa tumeshaikamilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Vigwaza - Kwala - Kimaramasale inayounganisha Majimbo matatu ya Mkoa wa Pwani, Jimbo la Bagamoyo, Kibaha Vijiji na Kisarawe, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ikizingatiwa kule kuna bandari kavu?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali, Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nimshukuru Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa swali lake.

Mheshimiwa Spika, niseme tu barabara hii inahudumiwa na *TANROADS* na katika ule mpango mkakati wetu tunao utaratibu wa kuitengeneza. Kwa sasa tunajitahidi kuhakikisha barabara hii inapitika wakati wote na kwa umuhimu wa kipekee kwa sababu ya kuwa na hii

bandari kavu tutaipeleka kwenye kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge avumilie kidogo utaratibu upo wa kuifanya hii barabara iwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa David Silinde nilikuona, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nami nina swali dogo la nyongeza. Tatizo lililopo katika Jimbo la Igalula lipo vilevile katika Jimbo la Momba hususan katika barabara ya kutoka Kakozi-Kapele - Ilonga ambako ni Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kandege, Jimbo la Kalambo.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri ahadi ya *TANROADS* ya kutengeneza barabara hiyo na yeye sasa hivi ndiye Waziri, haoni sasa ni wakati muafaka kutengeneza barabara hiyo ambayo inaunganisha mikoa miwili ya Songwe pamoja na Mkoa wa Rukwa, lakini vilevile Jimbo la Momba na Jimbo lake la Kalambo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nataka nimwombe Mheshimiwa Silinde tu avumilie kwa sababu sijatembelea Mkoa wa Songwe, lakini utaratibu wa Serikali kisera ni kwamba umuhimu wa kwanza ni kuhakikisha tunaunganisha mikoa. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi na katika bajeti yetu tuna *provision* na nikienda kule tutazungumza kwa upana zaidi ili aone namna ambavyo tumejipanga kuijenga barabara hii Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya fedha na Mipango, swali linaulizwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad Mbunge wa Wingwi.

Na. 363

Kero ya Ulipaji Kodi ya Mizigo Kutoka Zanzibar Kwenda Tanzania Bara

MHE. JUMA KOMBO HAMAD aliuliza:-

Mfumo wa ulipaji kodi za kusafirisha bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umekuwa ukilalamikiwa kwa muda mrefu kwamba unakwaza na kuvunja harakati za biashara Zanzibar na hivyo kusababisha uchumi wa Zanzibar kushuka:-

Je, Serikali ipo tayari kuunda Kamati kwa ajili ya kushughulikia mfumo wa ulipaji kodi za mizigo kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chimbuko la malalamiko ya kodi wakati mizigo inaposafirishwa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara linatokana na kuwepo kwa mifumo tofauti ya kuthamini bidhaa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hali hiyo inasababishwa na viwango tofauti vya ushuru wa forodha vinavyopaswa kulipwa kwa bidhaa ya aina moja kutoka nje ya nchi na kusafirishwa kwenda sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uthaminishaji bidhaa zote zinazolingia Tanzania Bara unafanyika kwa kutumia mifumo ya *TANCIS* na *Import Export Commodity Database* ikiratibiwa na kituo cha Huduma za Forodha kilichopo Dar

es Salaam. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitumii mifumo hiyo na hivyo kusababisha kuwepo na tofauti ya kodi kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utofauti wa mifumo inayotumika, bidhaa zote za nje zinazolingia Tanzania Bara, kupitia Zanzibar hufanyiwa uhakiki licha ya kuwa zimethaminiwa Zanzibar. Iwapo uthamini wa Tanzania Bara utakuwa sawa na ule uliofanywa Zanzibar, hakuna kodi itakayotozwa Tanzania Bara. Ikiwa kodi iliyolipwa Zanzibar ni kidogo, Mamlaka ya Mapato hukusanya tofauti ya kodi iliyoziidi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukusanya tofauti ya kodi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kutumia mifumo ya *IECD* na *TANCIS* haina lengo la kuuwa biashara Zanzibar, hatua hiyo inalenga kuleta usawa wa gharama za kufanya biashara na ushindani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea kujadiliana ili kuona kuwa suala hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Aidha, kwa kuwa Serikali zetu mbili hazijashindwa kutatua changamoto hii, ni dhahiri kabisa kuwa hakuna sababu ya kuunda Kamati ya kushughulikia mfumo wa ulipaji kodi kwa mizigo inayotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Hata hivyo, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2), Bunge lako Tukufu ni Mhimili unaojitegemea na hivyo Serikali haina mamlaka ya kuunda Kamati ndogo ya Bunge kwa ajili ya jambo hili au jambo lolote lile.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Wingwi, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Zanzibar ni Kisiwa kidogo chenye wakazi wachache sana, wakazi wa Zanzibar ni kati ya 1,000,000 mpaka 1,500,000 na kutokana na hali hiyo Zanzibar inategemea soko la bidhaa kutoka nje. Maana yake Zanzibar inategemea soko la bidhaa

zinazotoka nje kusafirishwa nchi jirani au baadhi ya nchi nyingine ili kutafuta soko na ndiyo maana Zanzibar imejiandalia mfumo wake mahsusi ili kufanikisha wafanyabiashara kutoka nchi nyingine ikiwemo Tanzania Bara wafike Zanzibar wachukue bidhaa zinazotoka nje kwa ajili ya kwenda kufanya biashara sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali haioni kwamba kullazimisha Zanzibar kufata mfumo wa *TANCS* ndiyo maana ya kua soko la bidhaa kutoka nje kwa pale Visiwa vya Zanzibar? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Waziri kasema haiwezekani kuunda Tume, Bunge haliwezi kuunda Tume. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, Je, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ipo tayari kuunda Kamati Ndogo wakiwemo Wabunge, Maafisa wa *TRA* na yeye mwenyewe kwenda Zanzibar kukutana na wadau, wafanyabiashara wa Zanzibar hususan Taasisi ya Wafanyabishara Zanzibar ili kuangalia ukubwa wa tatizo hili na kulitafutia ufumbuzi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba hiki kinachotokea ni kuhakikisha kunakuwa na ushindani katika soko la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana bidhaa zinazouzwa kutoka Zanzibar zilizotoka nje kuja Tanzania Bara lazima zifanyiwe uthamini ili kuhakikisha wafanyabiashara wanaotumia Bandari za Serikali ya Jamhuri ya Tanzania Bara wanapata ushindani ulio sawia.

Mheshimiwa Spika, amesema kwamba wafanyabiashara kutoka nchi nyingine. Kumekuwa na tatizo la wafanyabiashara kutoka nchi nyingine kwenda kununua bidhaa Zanzibar na kuja kuzi-*dump* katika soko la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana kwa sababu bidhaa zile hazijazalishwa Zanzibar lazima zinapoingia Tanzania Bara ziweze kulipa kodi husika ili ushindani huo uweze kuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, napenda kumwambia Mheshimiwa Kombo kwamba nimesema kwenye jibu langu la msingi Serikali zetu mbili, Serikali ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinalifanyia kazi tatizo hili na tuna uhakika kwamba changamoto hii itafika mwisho, kwa sababu majadiliano yamefika sehemu nzuri na tuna imani kubwa kwamba changamoto hii itafika mwisho sasa.

SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir nilikuona, swali fupi la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Ni lini Serikali italeta marekebisho ya Sheria Bungeni ili umeme unaonunuliwa Tanzania Bara kwenda Zanzibar uweze kupatiwa msamaha wa kodi kama ilivyo bidhaa nyingine zinazozalishwa Tanzania Bara kwenda Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati, Waziri wa Nishati alisema vizuri kabisa kuhusu jambo hili, kwamba nalo ni katika mambo ambayo yapo katika mijadala kuhakikisha kwamba kodi inayotozwa kwa umeme unaouzwa Zanzibar inafanyiwa kazi. Nimwombe Mheshimiwa Khadija Nassir pamoja na Wazanzibari wote na Watanzania wote jambo hili litafanyiwa kazi kwa muda muafaka kabisa.

SPIKA: Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, uliza swali lako sasa.

Na. 364

**Watumishi wa Afya ambao Hawakuwepo
kwenye Mifuko ya Kijamii**

MHE. LUCIA M. MLOWE aliuliza:-

Wapo Watumishi katika sekta ya afya, hususan Madaktari na Wauguzi ambao walijiriwa katika miaka ya 1980 kupitia Serikali Kuu, lakini wakati ule hapakuwa na makato ya mfuko wa kijamii na kuanzia mwaka 1999, Serikali ilianza kuwakata mishahara yao kwenye Mfuko wa *PSPF*:-

Je, Serikali inawafikiriaje Watumishi hao ambao fedha zao hazikukatwa na mifuko ya kijamii wakati huo hususan Mfuko wa *PSPF*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya Julai 1999, mfumo wa malipo ya mafao ya kustaafu kwa watumishi wa Serikali Kuu haukuwa wa kuchangia. Kwa mantiki hiyo, watumishi wote wa umma waliokuwa kwenye ajira ya masharti ya kudumu wanastahili malipo ya uzeeni, wakiwemo watumishi wa sekta ya afya hata kama hawakuchangia. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya tano (5) ya Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa *PSPF*, watumishi wote wa Serikali Kuu ambao walijiriwa na kuthibitishwa katika ajira ya masharti ya kudumu na pensheni, wanakuwa wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa *PSPF* kuanzia tarehe ya kuanzishwa kwa mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi Na.2 ya Mwaka 1999 kwa Watumishi wa Umma, ambayo ilianzisha Mfuko wa Pensheni wa *PSPF*, wastaafu wote ambao ni wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa *PSPF* na wanaoguswa na Sheria hii wanalipwa

mafao yao ya kustaafu na Mfuko wa Pensheni wa *PSPF* kwa kipindi chote cha utumishi wao. Hii inamaanisha kwamba, mafao yao yanakokotolewa kuanzia tarehe ya kuajiriwa hadi wanapostaafu utumishi wao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

SPIKA: Mheshimiwa Mlowe nimekuona swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwenye jibu lake la msingi kwamba watumishi wanapaswa kulipwa mafao yao hata kama hawakuwa wanakatwa, lakini hilo halifanyiki. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba hawa watumishi wanapata mafao yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa watumishi wastaafu wanapata pensheni yao ndogo sana, kuna watumishi wanapata Sh.50,000 kwa mwezi, kwa kweli kiasi hicho ni kidogo sana. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inaongeza kiasi hicho cha pensheni? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba hili jambo analosema halifanyiki, siyo sahihi. Kwa sababu watumishi wote ambao walijajiriwa na walikuwa hawachangii kabla ya Mfuko wa Pensheni wa *PSPF* kuanzishwa walikuwa wakilipwa na Serikali Kuu kupitia Hazina. Kwa sasa kile kilichokuwa kinalipwa kupitia Hazina ndicho kimeunganishwa na malipo yao ya *PSPF* na wanalipwa pensheni yao yote kama ambavyo wanastahili kulipwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, sina uhakika sana labda nikae na Mheshimiwa Mbunge ni wastaafu gani

wanaolipwa pensheni ya Sh.50,000, kwa sababu Serikali iliongeza pensheni ambayo ni kiwango cha chini kutoka Sh.50,000 kwenda Sh.100,000 na Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii inalipa Sh.100,000 kwa watumishi wote kama kiwango cha chini. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mlowe hujasema kweli leo bwana, hakuna wa elfu 50.

MBUNGE FULANI: Wapo!

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi swali la nyongeza tafadhali. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ukiacha waaguzi lakini pia wafanyakazi wengi wa Idara zingine Serikalini wanacheleweshewa sana mafao. Mfano ni Askari Magereza wanastaafu lakini wanakaa zaidi ya miaka miwili hawajaenda kwao. Wanaganda kwenye zile kota za Magereza *lane*, mafao hamna, mtu kastaafu miaka miwili anadhaliika kwao Tanga, kwao Kilimanjaro, kwao wapi, hawezi kwenda kwa sababu hajapewa mafao yao wala pensheni.

Mheshimiwa Spika, sasa hii Serikali inawaangalia kwa jicho lipi hawa Askari Magereza kwa sababu, wao wamezoea kuwa-*support* Polisi ambao wanatukamata, lakini wahalifu wako maeneo mbalimbali, wanakusanywa yale maeneo mbalimbali, wanapelekwa eneo moja ambalo ni Magereza. Wale jamaa wana kazi ngumu sana kuwatunza mle, lakini wanafanya utumishi wao, wanakuja wanastaafu, mtu anakaa *Police Lane* miaka miwili hajapewa *pension* wala mafao yake, kwa nini wanawafanyia hivi Askari Magereza? (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Niliacha swali hilo refu liendeleo maana linatoka kwa mtu mwenye uzoefu, anazungumza vitu halisi, siyo maswali ya kutungatunga tu. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa uzoefu huo wa Magereza, majibu tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ameuliza, kuhusu mkakati wa Serikali yetu, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbilinyi, mkakati wa kwanza wa Serikali yetu ilikuwa ni kulipa madeni yote ya michango ya mwajiri ambayo Serikali ilikuwa ikidaiwa na mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpaka leo ninapooonea madeni yote yaliyokuwa yanadaiwa ya michango Serikali yetu ya Awamu ya Tano tayari imeshalipa zaidi ya shilingi bilioni 282 ili kuhakikisha wastaafu wetu wanalipwa mafao yao kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa pili, ilikuwa ni kuona jinsi gani ya kuunganisha Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii, ili pesa zilizopo ziweze kutumika inavyotakiwa na kuwanufaisha wastaafu wetu pale wanapostaafu. Namwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Julai Mosi, mifuko yote imeshaunganishwa na sasa tuna mifuko miwili, tatizo hili litaondoka bila wasiwasi wowote.

SPIKA: Ahsante sana tuendeleo. Waheshimiwa wenye hoja kwenye mambo haya, leo ni Wizara ya Fedha na Mipango kwa hiyo, mtaweza kuchangia baadaye kidogo. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu. Mheshimiwa Qambalo, tafadhali.

Na. 365

Wanyamapori Kuharibu Mali na Kujeruhi Watu – Karatu

MHE. QAMBALO W. QULWI aliuliza:-

Matukio ya Wanyamapori kutoka nje ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda katika vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo Wilayani Karatu na kuharibu mazao ya wananchi na kujeruhi watu yamekuwa yakijirudia mara kwa mara:-

(a) Je, ni nini mkakati wa Serikali kuwadhibiti wanyama hao ili wabaki katika maeneo waliyotengewa;

(b) Fidia/Kifuta jasho kinachotolewa pindi wanyama wanapofanya uharibifu ni kidogo sana na imepitwa na wakati. Je, ni lini Serikali italeta marekebisho ya kifuta jasho, ili kuendana na mazingira ya sasa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mali na maisha ya binadamu kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu unajitokeza katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Ngorongoro. Katika Eneo la Ngorongoro uharibifu unajitokeza zaidi katika maeneo ya mashamba na makazi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu inakabiliana na changamoto ya uharibifu wa mali na maisha ya binadamu kwa kufanya doria za pamoja. Aidha, Mamlaka ya Ngorongoro ina vituo vitano katika maeneo ya Kilimatembo, Elewana, Nitini, Bonde la Faru na Masamburai kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, vilevile magari mawili yamenunuliwa kwa ajili ya madhumuni hayohayo.

Mheshimiwa Spika, juhudi nyingine zinazofanyika ni kuendelea kutoa elimu ya namna ya kujihami na kudhibiti wanyamapori, hususan tembo. Elimu hiyo, inahusisha matumizi ya pilipili, mafuta machafu na mizinga ya nyuki kuzunguka mashamba kama njia ya kufukuza tembo.

Mheshimiwa Spika, fedha za kifuta jasho na kifuta machozi hazitolewi kama fidia bali hutolewa kwa ajili ya

kuwafariji wananchi walioathirika na wanyamapori wakali na waharibifu. Hivyo, fedha hizo kuwa ni kidogo na hazilingani na hali halisi ya uharibifu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na wingi wa matukio pamoja na ufinyu wa bajeti Serikali imeamua kupitia Kanuni za Kifuta Machozi na Kifuta jasho ili kuondoa changamoto zilizopo kiutendaji.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, Mbunge wa Karatu, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na kuwa na doria za pamoja kati ya halmashauri na hifadhi hizo na pamoja na kuwa na hivyo vituo vilivyotajwa bado kasi ya wanyama waharibifu na wakali kutoka ndani ya hifadhi na kwenda nje kwenye makazi ya wananchi, imeendelea kuwa kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo tunayo kwenye Halmashauri zetu ni Halmashauri hazina usafiri kwa ajili ya kuwafukuza wanyama hao, Halmashauri hazina silaha stahiki kwa ajili ya wanyama hao, lakini pia, bajeti ndogo ambazo Halmashauri tunazo, pia, uchache wa watumishi wa sekta hiyo ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, hapa imesemwa kuna magari mawili yamenunuliwa kwa ajili hiyo. Magari hayo mawili naamini yako Ngorongoro hayako Karatu huku ambako tatizo lilipo. Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza akaongea na watu wake wa Ngorongoro ili angalau gari moja liwekwe Halmashauri, wale Maofisa wa Halmashauri pindi tatizo linapotokea waweze kwenda kushughulika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, fedha hizi za kifuta jasho au kifuta machozi, pamoja na kwamba, ni ndogo sana lakini pia, zinachelewa sana kuwafikia...

SPIKA: Mheshimiwa Willy, swali sasa.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Spika, swali; kwa nini fedha hizi zisilipwe kwenye hifadhi husika badala ya mlolongo ambao sasa hivi zinalipwa kutoka Wizarani?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Japhet Hasunga, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto hizi za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mengi. Changamoto ziko katika upande wa usafiri, watumishi, pamoja na vifaa vile vinavyotakiwa kutumika katika kupambana na hao wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe kusema tu kwamba, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, magari mawili yameshanunuliwa na tayari kweli yako pale. Jitihada ambazo tutafanya ni kulingana na jinsi ambavyo amependekeza Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha angalau gari moja linakuwepo katika maeneo yale kusudi pale linapotokea tukio basi gari hilo liweze kusaidia katika juhudi hizo za kupambana na wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kuhusiana na fedha za kifuta jasho na kifuta machozi kwamba, ziwe zinatolewa na hifadhi inayohusika, ni suala ambalo labda tutaliangalia wakati tunapitia upya hizi sheria ambazo tutaona kama kweli, inafaa. Kwa hivi sasa ilivyo tuna mfuko maalum ambao unatumika kwa ajili ya kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, huu mfuko bado unakabiliwa na changamoto ya kuwa na fedha za kutosha. Kwa hiyo, katika pendekezo analolileta nafikiri tutaliangalia, tutaona kama inafaa, tunaweza tukalichukua. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso ni jirani wa huko huko kwenye swali. Uliza swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Changamoto ambazo zinakabili vijiji hapa nchini vinavyopakana na hifadhi za wanyama zimekuwa ni changamoto za muda mrefu kwamba, wanyama wanaingia na kuharibu mazao na kuuwa watu, lakini ukiangalia nchi mbalimbali zilizoendelea duniani wanaweka *electrical fence*, ili kudhibiti moja kwa moja tatizo hili. Je, Serikali kwa nini isianze kwa awamu kutekeleza na kuweka hizo *electrical fence*, ili angalau kukomesha kabisa tatizo hili? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, dada yangu ambaye amekuwa akifuatilia kwa karibu sana matukio mbalimbali na amekuwa alifanya kazi nzuri sana, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu *electrical fence* kuwekwa katika hifadhi zetu zote ni suala zuri, lakini uwezo wa kifedha ndiyo changamoto. Ukiangalia ukubwa wa hifadhi tulizonazo kwamba, zote tutaweka *electrical fence* kwa kweli, inaweza ikachukua muda mrefu sana. Sitaki kutoa *commitment* ya Serikali, lakini tutaendelea kulifanyia kazi ili tuone kwamba, kama litawezekana, kama pale ambapo bajeti itaruhusu basi tunaweza kulitekeleza.

SPIKA: Kwa sababu ya muda tunaendelea na swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 366

Kuzuia Wanyama Waharibifu – Jimbo la Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Kila mwaka wanyama waharibifu wamekuwa wanakula mazao ya wakulima katika Jimbo la Bunda na

Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kulipa fidia ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa wakulima hao:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuzuia wanyama hao wakiwemo Tembo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua madhara yanayosababishwa na wanyamapori waharibifu na wakali, hususan tembo, kwa wananchi waishio kandokando ya maeneo ya hifadhi, ikiwemo Wilaya ya Bunda. Katika Wilaya ya Bunda Vijiji vinavyopata usumbufu wa mara kwa mara kutokana na wanyamapori waharibifu na wakali ni Kunzugu, Bukore, Nyatwali, Balili, Tamau, Serengeti, Nyamatoke, Kihumbu, Hunyari, Mariwanda, Mugeta, Guta, Kinyambwiga na Kinyangerere.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwanusuru wananchi kutokana na madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yote yanayopakana na maeneo ya hifadhi. Utekelezaji wa mikakati hiyo unaendelea ambapo katika Wilaya ya Bunda yafuatayo yamefanyika:-

(i) Umeanzishwa ushirikiano wa kudhibiti wanyamapori waharibifu kati ya watumishi kutoka Kikosi Dhidi ya Ujangili Bunda, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Pori la Akiba Ikorongo - Gurumeti, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na Mwekezaji *Gurumeti Reserve*;

(ii) Kutafuta vitendea kazi kwa ajili ya doria za wanyamapori waharibifu;

(iii) Vikundi 83 vimeanzishwa kwenye vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi kwa ajili ya kuchukua

hatua za awali za kudhibiti wanyamapori hao pindi kunapokuwa na matukio ya wanyamapori waharibifu, wakati wakisubiri msaada wa Askari Wanyamapori;

(iv) Wizara imetoa tochi 100 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Mwangi mkali husaidia kufukuza tembo usiku kwa vijiji vinavyounda vikundi hivyo vya kufukuza wanyamapori;

(v) Mafunzo kwa wananchi juu ya mbinu za kukabiliana na wanyamapori waharibifu yametolewa kwa vijiji, sambamba na kuwashauri kuepuka kulima kwenye shoroba za wanyamapori;

(vi) Kuweka madungu (minara) ambayo Askari Wanyamapori wanaitumia kufuatilia mwenendo wa tembo;

(vii) Kutumia teknolojia ya mizinga ya nyuki ambayo imewekwa pembezoni mwa mashamba; na

(viii) Mpango wa kutumia ndege zisizo na rubani kwa ajili ya kufukuza tembo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lengo la mikakati hii ni kuhakikisha kwamba, matukio ya uvamizi wa tembo yanashughulikiwa kwa haraka iwezekanavyo. Sambamba na mikakati hiyo Wizara imekuwa ikitoa fedha za kifuta jasho au kifuta machozi pale ambapo mazao yameharibiwa au wananchi wamejeruhiwa au kuuawa na wanyamapori wakali, akiwemo tembo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Machi hadi mwezi Oktoba, 2017, Wizara imelipa kifuta jasho na kifuta machozi cha jumla ya Sh.249,741,250 kwa wahanga 1,284 na vijiji 14 katika Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayosababisha matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kuendelea kuwepo ni kuzibwa kwa shoroba na mapito ya wanyamapori. Kutokana na hali hiyo Serikali ina mpango wa

kufufua shoroba za wanyamapori katika maeneo mbalimbali nchini kwa mujibu wa Kanuni za Shoroba, GN. 123 ya tarehe 16 Machi, 2018. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, niwapongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kunipa gari la kusaidia kufukuza wanyama waharibifu kwenye maeneo yangu, lakini pia, najua wana mpango wa kupeleka fedha za kifuta jasho katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa, sasa ni miaka 15 Vijiji vya Hunyali, Kihumbu, Maliwanda, Salakwa, Kyandegge, Tingilima, wamekuwa ni wahanga wakuu wa wanyama waharibifu wa mazao, sasa Serikali ina mpango gani sasa mbadala ikiwepo kupima vijiji hivyo ili kupata Hati Miliki za Kimila na kuendesha maisha ya wananchi wa makazi hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa kuona ni kuamini na kuamini ni kuona, ni lini sasa Wizara au Waziri atatembelea maeneo haya, ili kujihakikishia hali halisi ya uharibifu huo?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Getere, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kwanza ni kweli kabisa kwamba, sasa hivi Wizara ina mpango mkubwa mahususi wa kuhakikisha kwamba vijiji vyote ambavyo vinazungukwa na Hifadhi za Taifa vinakuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi. Hili tunalifanya kuanzia mwaka wa fedha unaoanza Julai mwaka huu. Katika kutekeleza hilo

tunashirikiana na Wizara ya Ardhi, ambapo ndiyo wamepewa hizi fedha kwa ajili kusaidia kupima vijiji vyote hivi ili wawe na mpango mzuri na kuhakikisha matumizi yanaeleweka vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu kwenda kutembelea na kujionea hali halisi, naomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari wakati wowote mara baada ya Mkutano huu wa Bunge kumalizika tutapanga ni lini tunaweza kufika kule ili tujionee hali halisi ilivyo huko.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mtaona muda wetu ni mdogo. Swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Mpakani Tunduma.

Na. 367

Ujenzi wa Barabara ya Mpemba hadi Ileje

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Mpemba hadi Ileje kwa kiwango cha lami ili kuunganisha na kuboresha mpaka wa Malawi na Tanzania katika eneo la Isongole?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpemba – Isongole ambayo ni barabara kuu yenye urefu wa kilometa 50.3 inaunganisha nchi yetu na nchi jirani ya Malawi inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*), Mkoa wa

Songwe. Barabara hiyo inaanzia katika Barabara Kuu ya TANZAM, eneo la Mpemba, katika Mamlaka ya Mji wa Tunduma, Wilaya ya Momba. Barabara hii ni kiungo cha kufika katika Mji wa Itumba ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ileje na maeneo ya jirani ya nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii na kwa kuwa, ndiyo barabara inayounganisha wananchi wa sehemu mbalimbali wa Wilaya ya Ileje na nchi jirani ya Malawi na Zambia, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inaendelea kujenga Barabara ya Mpemba – Isongole kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa utekelezaji wa mradi upo kwenye hatua za awali, zikiwemo ujenzi wa Kambi ya Mhandisi mshauri ambayo imefikia 80%, kusafisha eneo la ujenzi wa barabara kilometa 10, ujenzi wa makalvati manne na uwekaji wa tabaka la chini la barabara.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni 4.455 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami na katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii, ili mradi huu uweze kukamilika kama ulivyopangwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yanayotoa faraja kwa wananchi wa Tunduma pamoja na Ileje, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wananchi wa Kata ya Bupigu, Kata ya Malangali, Kata ya Isoko na Kata ya Ikinga katika Wilaya ya Ileje wamekuwa na adha kubwa sana ya kuamka Saa nane ya usiku na kusubiri usafiri kuja makao makuu ya Mkoa wa Songwe. Ni lini Serikali itajenga barabara hii ya kutoka Isongole mpaka Ikinga, ili kuondoa adha hii ya Wananchi wa Ileje?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna kipande cha barabara kilometa 1.6 kimejengwa katika Mji wa Tunduma

na kimejengwa kwa sababu, wananchi wa Mji wa Tunduma wakati Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa Ujenzi, wakati anapita anakwenda Rukwa, walimsimamisha pale na wakamwomba barabara ile ijengwe haraka iwezekanavyo na sasa Serikali imejenga kipande kile cha kilometa 1.6, lakini kipande kile kimejengwa chini ya kiwango. Je, ni lini Serikali itakuja kuhakiki kipande kile cha barabara ili wananchi wa Tunduma waweze kufurahia mpango wa ujenzi wa barabara kwenye Mji wa Tunduma?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mbunge wa Tunduma, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama anavyouliza, anapenda kujua katika swali lake la kwanza, katika hizi Kata za Lupingu, Malangali na Ikinga, kuna sehemu ambayo ina uharibifu mkubwa, kwamba, kwa kweli, maeneo mengi tumekuwa na uharibifu kutokana na mvua zimekuwa nyingi, lakini kama tulivyopitishiwa bajeti na Bunge lako, tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo, ili kuhakikisha kwamba, maeneo haya yanapitika.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujapata kipande cha lami katika eneo hili nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Tunduma kwa ujumla kwamba wakati hizi mvua zinapungua tumejipanga kwa ajili ya kufanya marekebisho makubwa ili maeneo haya yapitike. Kwa hiyo, nimtoe tu wasiwasi kwamba tutafanya marekebisho ili wananchi waendeleo kupata huduma ili waondokane na hii adha ambayo wanaipata.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu kile kipande cha kilomita 1.6 ambacho Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba hakikujengwa katika *standard* inayotakiwa; niseme tu kwa sababu nitakuwa na ziara ya maeneo yale kwamba tutayaona kwa pamoja ili tuone kwamba hii kilomita 1.6 ina shida gani ili tuone kama kweli

ni kiwango hakikuwa kimefikiwa au labda saa nyingine ndiyo ilikuwa kuna shida tofauti ya hapo kwa sababu kuna wakati mwingine barabara zinajengwa lakini mazingira ambayo hayakutegemewa yanaweza yakatokea barabara ikaharibika.

Mheshimiwa Spika, tutaiona kwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge halafu tuone tutachukua hatua kama kutakuwa na shida yoyote kuhusu kipande hiki ambacho umekitaja.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Catherine Magige kwa niaba yake nimeokuona Mheshimiwa Amina Mollel.

Na. 368

Fidia kwa Wananchi wa Mkoa wa Arusha

MHE. AMINA S. MOLLEL (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi 55 wa Kata za Oldonyosambu na Mateves Wilayani Arumeru Mkoani Arusha waliopisha ongezeko la barabara ya Arusha-Namanga toka mwaka 2013.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mali za wananchi 55 wa Kata ya Oldonyosambu walioathiriwa na ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga ilifanyika mwaka 2013 na kiasi cha shilingi milioni 281.501 kilihitajajika kwa ajili ya kuwalipa fidia. Uhakiki wa tathmini hiyo ulifanyika na

umekamilika, tayari Serikali imeshatoa Shilingi milioni 66.821 katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kulipa sehemu ya fidia hiyo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya fidia yatafanyika kwa pamoja kwa wananchi wote mara baada ya Wizara yangu kupokea fedha zote zinazohitajika kwa ajili ya kulipa fidia hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa wananchi wote wanne (4) kwa Kata ya Mateves wameshalipwa fidia yenye jumla ya shilingi bilioni 2.225, hivyo hakuna mwananchi wa Kata ya Mateves anayeidai Serikali fidia.

SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, kama una swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ninalo. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu hayo ya Serikali lakini mpaka Mheshimiwa Mbunge anaandika swali hili ni kwamba katika Kata hiyo ya Mateves bado kuna wananchi ambao wanadai fidia ya malipo hayo kwamba bado hawajatimiziwa. Je, Waziri yuko tayari kufuatilia na kuhakikisha kwamba wananchi hawa wote wanapata malipo yao kama ilivyokubalika awali? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ningependa tu kupata *commitment* ya Serikali amesema kwamba atakapokea fedha hizo. Je, katika msimu huu wa mwaka 2017/2018 au ni mpaka katika bajeti nyingine na pengine tu kwamba Waziri wenyewe yupo tayari kwenda sasa na Mheshimiwa Mbunge ili kwenda kusikiliza hizo kero na malalamiko ya wananchi na kuweza kuwakamilishia fidia yao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mafupi, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, nimp ongeze sana Mheshimiwa Mollel na Mheshimiwa Mbunge Catherine Magige kwa ushirikiano wao namna ambavyo wanafuatilia ili kuhakikisha kwamba wananchi wao katika maeneo haya ya Arusha wanapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya juhudi kubwa sana kulipa fidia hizi. Ukiangalia kwa ujumla wake kwamba kulikuwa na jumla ya madai ya shilingi bilioni 2.5, lakini mpaka sasa tunavyozungumza bilioni 2.291 zimekwishalipwa ina maana kwamba asilimia 92 ya madai yote imeshalipwa. Hii inaonesha kwa jinsi gani Serikali iko *committed* kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanaodai wanapata haki zao na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba hiki kiasi cha shilingi milioni kama 214 kilichobaki ni kiasi ambacho ni kidogo, lakini ni muhimu kilipwe mapema. Kwa hiyo, tunafuatia na niseme tu kwamba ni wakati wowote na niko tayari kuhakikisha kwamba fedha zikipatikana kutoka Hazina hawa wananchi wanalipwa mara moja. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi, kama tulivyowalipa hawa wengine na wao watalipwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *commitment* ya Serikali , nisema wakati niko *committed* kama nilivyoahidi hata wiki iliyopita wakati nikijibu swali lako Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafika maeneo haya ili sasa tuweze kuona pia kwamba ni nini kinachotakiwa kufanyika ili mambo yaende sawia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya mwisho kwa siku ya leo ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Muheza, tafadhali.

Na. 369

Tatizo la Maji Muheza

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi zake ikiwemo ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za kutoa maji Mto Zigi kwenda Muheza na Vijiji vyake?

(b) Je, Serikali ina mpango gani zaidi ya huo wa kuwaletea maji wananchi wa Muheza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kutekeleza ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambapo imekamilisha usanifu wa kutoa maji kutoka Mto Zigi kwenda Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekelezwa katika mradi huo ni ujenzi wa kitekeo cha maji (*Intake*) katika Mto Zigi, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilometa 23, uunganishaji wa vijiji vitakavyopitiwa na bomba kuu umbali wa kilometa 12 kila upande, pamoja na upanuzi na ukarabati wa mtandao wa usambazaji maji katika Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeendelea na utekelezaji wa oboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Muheza, kwa mpango wa muda mfupi. Kazi zinazotekelezwa ni ulazaji wa mabomba

urefu wa kilomita 16.9 kutoka Pongwe Jijini Tanga hadi Kitisa Wilaya ya Muheza. Gharama za utekelezaji wa mradi huo nishilingi milioni 413.5

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha fedha shilingi bilioni 3.17 kwa ajili ya kuendelea na uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Muheza na vijiji mbalimbali katika Wilaya hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Balozi Adadi, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. BALOZI ADADI. M.RAJABU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza: Kwanza napenda kuwapongeza sana Mawaziri wote yeye Naibu Waziri ameshafika Muheza pamoja na Waziri mwenyewe wiki iliyopita Ijumaa alikuwa Muheza na ameonesha ishara kwamba kweli Muheza inakaribia kupata maji. Isitoshe pia Mwewe katika kipindi cha *Clouds TV* imesema kwamba Muheza itapata maji hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Zigi kutoa maji kutoka Mto Zigi mpaka Mjini Muheza ni kati ya miradi 17 ambayo tunategemea kupata mkopo wa Serikali ya India ya dola milioni 500. Nataka kujua mradi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, la pili, pale Muheza Halmashauri ya Wilaya imenunua mtambo wa kuchimba visima, lakini mtambo huu tunashindwa kuutumia kikamilifu kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Kwenye bajeti hii ya wakati huu tumepangiwa zaidi ya bilioni moja na tuna mpango wa kuchimba zaidi ya visima 50, Halmashauri imekwishapitisha.

Mheshimiwa Spika, nataka Waziri awahakikishie wananchi wa Muheza kwamba Urasimu utaondolewa, tunataka kuchukua kiasi cha fedha kutoka kwenye hiyo bilioni ambayo tumepangiwa ili tuweze kutumia mtambo huu ili

tuweze kuchimba visima. Nataka Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi kwamba urasimu huo utaondolewa na utasaidia ku-*facilitate* mipango hii iweze kuendelea.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri, lakini niwahakikishie wananchi wa Muheza wana Mbunge mfuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kudhamiria kwa kutatua tatizo la maji kabisa katika Mji wa Muheza tumeona haja ya kuwekeza mradi mkubwa wa maji kati ya miradi ile 17 na utekelezaji wa maji inategemea na upatikanaji wa fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mpaka sasa Serikali imeshasaini mkataba na ile Serikali ya India mradi wa mkopo wa milioni 500 katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie yeye pamoja na wananchi wa Muheza wakati wowote mradi ule utaanza mara moja. Sisi kama Wizara ya Maji tutasimamia na kufuatilia fedha zile mradi uanze mara moja na kwa wakati katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo lakini tuwapongeze kwa kununua mtambo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge leo saa saba tukutane na Katibu Mkuu wa Maji ili katika kuhakikisha namna gani tunaweza tukawasaidia wananchi wa Muheza waondokane na tatizo hilo la maji katika kuhakikisha tunawaunga mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu naomba tuendelee na matangazo. Leo tuna wageni wengi kweli *is a record*. Nitaanza na wageni ambao wako kwenye jukwaa la Spika.

Wageni watatu ambao ni Watumishi kutoka Ofisi ya Spika wa Bunge la Ghana, *our visitors from Ghana Head of Deputy Speaker's Secretariat – Mr. Mathew Tawiah, Head of the First Deputy Speaker's - Secretariat - Ms. Janet Frimpong, Head of the Second Deputy Speaker's Secretariat – Ms. Anita Papafio, your most welcome.* Inaonekana Bunge la Ghana lina Manaibu Spika wawili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni 55 wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Philip Mpango ambao ni hawa wafuatao:-

Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Suzana Mkapa; Naibu Katibu Dkt. Hatibu Kazungu; Naibu Katibu Mkuu Ndugu Amina Shaaban; Kamshina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) - Ndugu Charles Kichere; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Profesa Juma Assad; Kamshina wa Bajeti, Ndugu Mary Maganga; Kamshina wa Sera (*CPAD*), Ndugu Benedicto Mgonya; Mhasibu Mkuu wa Serikali, ndugu Francis Mwakapalila; Msajili wa Hazina, Ndugu Mafutah Bunini; Mkaguzi wa Ndani wa Serikali, Ndugu Mohamed Mtonga; Kamshina Msaidizi wa Kitengo cha Utakasishaji wa Fedha Haramu, Ndugu Gilbert Nyombi; Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha (*JFC*), Ndugu Ernest Mchanga;

Wengine ni Kaimu Kamishna wa Idara ya usimamizi wa Sera ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Ndugu John Mboya; Kamshina wa Idara ya Sera na Ununuzi wa Umma, Dkt. Fredrick Mwakibinga; Mtendaji Mkuu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dkt. Albina Chuwa; Kamshina Msaidizi wa Bajeti, Ndugu Pius Mponzi; Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa (*PPF*), Ndugu William Erio; Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni (*GEPP*), Ndugu David Msangi; Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (*PSPF*), Ndugu Adam Mayingu, wameambatana na Wakuu wa Taasisi, Mashirika, Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Raphael Chegeni wanaotoka Singapore, *our*

visitors from Singapore please! Madam Elaina Chong and Madam Farizan Demoran, your welcome. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne (4) wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWTG) ambao ni wanamitindo kutoka Jiji Dar es Salaam Ndugu Khadija Mwanamboka, Ndugu Fideline Iranga, Ndugu Frank Gongona na Ndugu Richard Mlekoni. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Raphael Chegeni nimeshawataja.

Wageni 11 wa Mheshimiwa Juma Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni Walimu tarajali kutoka Mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambao ni wapiga kura wake kutoka Karatu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Khadija Nassir Ali ambaye ni mtoto wake kutoka Dodoma, Ndugu Abdulrahman Festo Mselia. *(Makofi)*

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Bonnah Kaluwa ambao ni wanafunzi kutoka shule ya Sekondari Tusiime iliyopo Jijini Dar es Salaam, wanafunzi wa Tusiime wako wapi? Ooh! karibuni sana Tusiime. Hii ni moja ya shule bora kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao ni Viongozi wa CCM, Mji wa Mbalizi Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Fred Mwampashi, karibuni sana wageni wetu toka Mbeya. *(Makofi)*

Wageni Watatu (3) wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni wapiga kura wake kutoka Nachingwea, Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Wageni 51 wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni wanafunzi wa Vyuho Vikuu vilivyopo Dodoma wanaotokea

Halmashauri zote za Mkoa wa Singida wakiongozwa na Ndugu Yohana Msita, Wanyampaa wako wapi? Inaelekea hawapo leo au wapo *basement* maana wageni ni wengi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Chief John Kadutu ambao ni wachezaji wa Timu ya Ulyankulu Veterans kutoka Ulyankulu wakiongozwa na Mheshimiwa Juma Hamduni, Diwani. Karibuni sana Walyankulu. (Makofi)

Wapo pia wageni saba (7) wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambao ni wapiganaji wake kutoka Chunya Mkoani Mbeya. Mheshimiwa Mwambalaswa ananiambia hawa ndiyo kiboko ya CHADEMA, Mbeya. (Kicheko)

Pia, wageni 94 wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni Walimu na wanafunzi wa Shule ya Mount Everest kutoka Dar es Salaam, Ooh! wanapendeza, karibuni sana Shule ya Mount Everest, karibuni watoto wetu. (Makofi)

Wapo pia wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambao ni jamaa zake kutoka Mkoani Morogoro. (Makofi)

Wageni Wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni marafiki zake toka Jijini Dar es Salaam. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo ni Wanachuo 40 kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) cha Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. Wanafunzi 30 na walimu watano (5) kutoka shule ya Sekondari ya Denis ya Morogoro, karibuni sana watoto wetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa William Ngeleja anatutaarifu kwamba timu yetu ya Mpira wa miguu jana iliwafunga St. John's bao moja na mchezaji aliyefunga bao hilo ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, mchezaji bora wa jana alikuwa ni Mheshimiwa Hamidu Bobali. (Makofi)

Kwa upande wa Bunge Queen's ilipata magoli 75 *against* St. John's *University* ilipata magoli matatu tu. Nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Esther N. Matiko ambaye peke yake Mheshimiwa Esther Matiko alifunga magoli 47 kati ya hayo 75. Hongera sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Jumapili timu yetu ya mpira wa miguu iliwaifunga Kadutu *Boys* ambayo wapo hapo juu magoli matatu dhidi ya sifuri..

MHE. JOHN P. KADUTU: Aaah! *(Kicheko)*

SPIKA: Magoli matatu kwa mawili, wafungaji wetu walikuwa Mheshimiwa Alex R. Gashaza na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na mchezaji bora katika mechi hiyo alikuwa Ahmed Juma Ngwali. Tunawasisitiza Waheshimiwa Wabunge kuhudhuria michezo kila *weekend* kuwatia moyo wachezaji wetu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naona niwatangazie kwamba Ofisi ya Bunge tumepokea barua kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikitoa rai kwa Wabunge ambao mlipoka matrekta kutoka SUMAJKT kulipa madeni yenu ya matrekta hayo na zana zake ambayo mliyakopa haraka sana.

Itakumbukwa kwamba tarehe 17 Mei, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alitoa maelekezo kwa wadaiwa wote wa matrekta na zana zake wa SUMAJKT warejeshe madeni yao ndani ya kipindi cha siku thelathini. Kufuatia maelekezo hayo Wabunge wote mnaodaiwa ni SUMAJKT mnatakiwa kuresha madeni hayo kabla ya tarehe 23 Juni, 2018. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Walipe!

SPIKA: Majina yenu ninayo hapa sijui niyasome?

MBUNGE FULANI: Soma!

Waheshimiwa kuna wanaoafiki nisome na wasioafiki. Wasioafiki wameshinda. Kwa hiyo Waheshimiwa kwa kweli tulipe madeni haya. Nimeaangalia kwenye orodha ile ya wanaodaiwa haya nikasema labda tuangalie kwenye malipo yetu ya Bunge tuwakate kule, nikakuta kule nako hawana hata kitu, kwa hiyo sina pa kukata. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, kutakuwa na mafunzo pamoja na mazoezi ya maonesho ya mavazi (*fashion show*) kwa Waheshimiwa Wabunge mtakaoshiriki onesho la mavazi, siku ile ya hafla ya uchangishaji fedha za kuboresha mazingira ya mtoto wa kike shuleni kwa majimbo yote. Kwa hiyo, tunawaomba sana wale ambao mtashiriki kwenye *fashion show* hiyo tuwataarifu kwamba Mwanamindo Maarufu Khadija Mwanamboka yuko kwenye jukwaa letu hapo, ameshawasili kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo ya mazoezi. Mazoezi hayo yatafanyika katika Ukumbi wa Msekwa, C na D, saa saba mchana mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Damas Ndumbaro, anawatangazia Wabunge wa Nyanda za Juu Kusini, Wabunge Vijana na Wabunge wote kufika kwenye *presentation* ya Tamasha la Maji Maji Selebuka, leo tarehe 4 Juni, katika ukumbi wa zahanati ya zamani saa 7.30 mchana.

Naona tumemaliza sasa inabidi tuendelee na mambo mengine.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Katibu nisomee majina:

NDG. LINAH KITOSI-KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Ryoba,

Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Chegeni.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mheshimiwa Chegeni, kifupi jamani.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, naomba tu kutumia kanuni ya 68(7), lakini naomba tu nieleze kwamba, kuna baadhi ya mkoa ambayo ni mipya, lakini kwa bahati mbaya sana haina vitendea kazi vya zimamoto. Mkoa wa Simiyu ni mkoa mpya lakini, una gari la zimamoto ambalo limeshakuwa chakavu halifanyi kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Chegeni hilo jambo limetokea lini katika mambo yetu?

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa halijatokea leo hii, lakini naomba tu nilieleze.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Chegeni, kinyume na kanuni uliyoisoma. Mheshimiwa Ryoba.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) na ile ya 47, kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, pale Serengeti katika Kijiji cha Nyichoka, wameuawa simba tisa. Hali ya wanyama kutoka nje ya hifadhi, ni mbaya sana. Tunakoelekea inaonekana Serikali haiko *serious* na wanyama wanaotoka nje ya hifadhi. Sasa wanatoka nje ya hifadhi wanauawa, Serikali haina mkakati wowote mpaka sasa hivi wa kuzuia hawa wanyama. Kwa hiyo, nataka mwongozo wako, Serikali ina utaratibu gani wa kuhahikikisha kwamba inazuia hawa wanyama wasitoke nje ya hifadhi?

Mheshimiwa Spika, hawa wanyama wanauawa mwisho wataisha, maana wamekwenda wamekula ng'ombe, bahati mbaya sana wafugaji wameweka sumu

kwenye mzoga, wameenda wamekula wamekufa; na sio Serengeti peke yake walikwenda pia na huku maeneo ya Karatu Karatu huku, ikawa hivyo hivyo na Serikali bado iko kimya.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ryoba, tumekupata. Maliasili m-*note down* hilo lililotokea, ni taarifa nzuri Mheshimiwa, Serikali wameipokea moja kwa moja. Ni jambo la hatari, maana Serengeti ina simba wachache sana, kama unaweza kuwaua tisa kwa mpigo ni hatari.

Mheshimiwa Mlowe.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa kanuni ya 68(7), naomba mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema. Wakati Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali langu nililouliza la 364, alisema kwamba si kweli kusema kwamba watumishi wastaafu wanapokea shilingi hamsini elfu. Nina ushahidi kabisa, kuna hata wazazi wa baadhi ya Wabunge huku ndani wanapokea pesa hizo, hamsini elfu kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kuhusu suala hili kwa sababu nimeambiwa ni mwongo lakini hali kuwa najua ni ukweli, kuna watu wanapokea fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mlowe, Naibu Waziri alipojibu alisema yeye hana taarifa, lakini angependa kama una taarifa hizo basi uwapatie ili waweze kuzifanyia kazi. Kwa hiyo ujumbe umefika, wewe wawasilishie ili muweze kuliweka vizuri kwa pamoja.

Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushuru. Mwongozo wangu utatokana na swali namba 369, ambapo kila wakati tulikuwa tukiulizia maswali...

SPIKA: Kanuni gani Mheshimiwa?

MHE. AMINA S. MOLLEL: Kanuni ya 68(7), kuhusu swali namba 369, limetokea leo. Kutokana na swali hili tumekuwa tukizungumzia masuala ya maji na shida kubwa ya maji iliyopo katika maeneo mengi. Hata hivyo, baadhi ya wananchi katika Vijiji vya Oldonyosambu na Oldonyowasi maji wanayopata yana kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride*.

Mheshimiwa Spika, hili ni janga kwa sababu watoto wanapata ulemavu wa kupinda miguu, pia akinamama wanapinda mgongo. Inaumiza sana, kwa sababu kizazi kinachozaliwa pale kinapata ulemavu. Upo ulemavu unaokubalika lakini ulemavu huu unatokana na janga la maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride* haukubaliki. Tunazalisha kizazi ambacho watoto wale wanapata ulemavu ambao kwa kweli kama Serikali tukipeleka maji tutaondoa ulemavu huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli ya Serikali ni jitihada gani za haraka, zinafanyika katika kuokoa kizazi kile ili kuondokana na hili janga la ulemavu ambao unaweza kuepukika. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel, kwa hoja yako muhimu sana. Wizara ya Maji ichukueni hiyo, namna gani ya ku-*deal* na *fluoride* ambazo zinasababisha matatizo makubwa kwa watoto.

Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa kanuni ya 68(7), lakini nikisoma pamoja na kanuni ya 47. Kama utaona inafaa na kwa udharura na unyeti wa jambo hili, ningeomba lijadiliwe na Wabunge ili litolewe mwongozo. Juzi wakati Waziri wa Madini anahitimisha hoja yake hapa, alipiga marufuku kusafirisha *carbon* kutoka kwenye mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.

Mheshimiwa Spika, wale wazalishaji wa dhahabu wanapokuwa wamezalisha dhahabu, wanapokuwa wameichakata inakuwa *in carbon form* wanaipeleka kwenye *plant* inayoitwa *illusion*, ile *plant* ndiyo inayotumika kukamata dhahabu na kuuza, sasa inakuwa dhahabu kamili ili iuzwe.

Mheshimiwa Spika, kwenye mikoa yetu ambayo mingi tunazalisha dhahabu, kwa mfano Mkoa wa Mara, hatuna hiyo *plant ya illusion*; Mkoa wa Mara hakuna kabisa hiyo *plant* na Mkoa wa Mara kuna wachimbaji wadogo wengi sana, hasa kwenye Jimbo langu la Tarime, wengi wanafika hata mia nane mia tisa na wanategemea kuzalisha dhahabu kwa ajili ya maisha yao, wamekopa kwenye Mabenki, wamekopa kwenye SACCOS na wengine wamekopa kwa watu binafsi. Kwa hiyo kitendo cha kupiga marufuku kuanzia Juni mosi ghafla tu, kwamba watu wasisafirisha *carbon*, inaenda kuharibu uchumi wa watu wengi sana na watu wengi majumba yao yatauzwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye hilo, uzalishaji wa *carbon* hii, uki-*extract* na ukakamata dhahabu, sehemu pekee ambayo kanda ya ziwa watu wanauza dhahabu ni Mwanza. Sasa, hata kama kungekuwa na *illusion plant*, ukisema watu wa-*extract* wasafirisha dhahabu ni hatari kweli kweli. Pia watumishi wa TMAA wa kukaa pale na kuangalia *loyalty* ya Serikali kwenye kila *plant* itakapozalishwa mimi naona ni kazi ambayo Serikali inajipa ambayo ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, ningepomba hili jambo, lizungumzwe kama jambo la dharura, kwa sababu kuna wananchi wengi sana, na nafikiri ni mikoa mingi sana, ambao wana *carbon* ndani na wanaenda kuzuiliwa kusafirisha kuanzia jana na maisha yao wanadaiwa na Mabenki na italeta usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili kama utakubali lijadiliwe na Wabunge hapa watoe mwongozo kwa Serikali ili watu hawa wasije wakaharibu uchumi wao.

SPIKA: Hilo jambo tuachie tu, tulifanyie kazi, ili tuweze kujua nini ni nini, kwa sababu si wengi hapa ambao tunafahamu hii *illusion* ni kitu gani na kikoje. Wizara isingeweza kukurupuka tu kusema hivyo lazima kuna sababu za msingi sana. Kwa hiyo, tupeane muda tutapata kwa wakati muafaka maelezo kuhusu jambo hilo, sasa kama yatakuwa hayatoshi ndio tutakuwa na majadiliano kama itabidi.

Mheshimiwa Musukuma, ndiye wa mwisho.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami nasimama kwa kanuni ya 68(7) ikisomwa na 47, nadhani nina imani busara yako mimi sina sababu ya kuomba suala hili lijadiliwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, imefanya vizuri sana kuhamasisha wananchi na wafanyabiashara waweze kulipa kodi kwa kutumia mashine za *EFD*. Hata hivyo, tunavyozungumza ni zaidi ya siku 10 mashine za *EFD* nchi nzima, kupita kwenye *shell*, madukani na sehemu zingine hazifanyi kazi na wafanyabiashara wengi hawana mbadala hata ya risiti ya mkono ambayo *TRA* hawaitambui, kwa hiyo watu wanafanya biashara bila ya kutoa risiti, leo karibu siku 10, Serikali imepoteza mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kauli ya Serikali, hasa kwa *supplier alie-supply EFD machines* ambayo sasa anazi-*temper*, tunakuwa tunakula hasara, hatukusanyi kodi na hatuna mbadala nyingine ya Serikali ni nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, nakushuru.

SPIKA: Kwa sababu leo ni Wizara ya Fedha na Mipango, hilo Waziri analichukua moja kwa moja, yatakuwa ni moja ya maeneo ambayo atayatolea ufafanuzi wa kutosha kabisa, kati ya leo na kesho pia. Kwa hiyo tuwe makini tu kufuatilia.

Kwa hiyo mipango yote ikafanyika na tumewajibika kama Bunge katika kila hatua. Sitaki kwenda na kila jambo ambalo lilitokea katika kila hatua, ikibidi huko mbele nitakuja kueleza, kwa sababu tulikuwa tunafahamu kila kinachoendelea na tunajua kila kilichoendelea. Ilibidi sisi kama Bunge kama tulivyokuwa tumepanga ratiba yetu iishie tarehe 30 ile ile na tulifanya hivyo, tulifika pale.

Tukumbuke msiba unakuwa ni wa familia, ndio wenye kauli ya mbele zaidi kuliko sisi au watu wengine. Hata kama tulikuwa tumekubaliana mwanzoni, iwe hivi iwe tarehe 30 familia wana uwezo wa kubadili wakati wowote maamuzi yao na wakafanya wanavyoona inafaa, lakini sisi kama taasisi tunapoishia pale tulipopanga tunaishia pale.

Iko misiba mingine, kwa mfano nchi ya Nigeria na kwingine kule, ninyi mnafahamu, wanachukua hata miezi mitatu kabla ya kumzika marehemu, wengine wanachukua mwezi. Sasa hatuwezi Bunge tukaenda mahali tukaweka matanga pale tukaa miezi mitatu tunasubiri mpaka siku ambayo familia itasema sasa ndipo izike, haiwezekani. Lazima tuwe na muda muafaka na muda ule unafahamika na kila mtu anakuwa anajua tunashiriki vipi na mwisho wetu ni wapi.

Tulipata ushauri muhimu sana, kutoka kwa Mwenyekiti wa Wabunge wa Kigoma, Mheshimiwa Nsanzugwanko, tangu mapema na hata mahali pale, kwamba kwa kabila la Waha na kwa kweli Watanzania kwa ujumla huwa hatugombe msiba, watu hawanyang'anyani marehemu. Kwa hiyo kwa busara iliyotokea pale baada ya kukaa na wenzetu tukakubaliana kwamba tuwakabidhi familia ili familia iweze kuendelea na hatua iliyobaki kwa sisi pale tulipofika ikawa ndio mwisho wa zoezi letu na tukafanya hivyo kwa amani na salama kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, isingetarajiwa hata kidogo Spika aende kwenye uwanja ulioandaliwa na vyama vya

kisiasa, nika pale nianze kuingia kwenye siasa za kuanza kujadili hatma ya marehemu, kwamba Mbunge gani atafuata, wa chama gani na kadhalika na mimi niko pale, hata kumzika bado, hiyo biashara nisingeweza kufanya hivyo na sijawahi kufanya na hata Maspika walionitangulia hawajawahi kufanya. (Makofi)

Siku zote tunapowapeleka marehemu wetu huwa tunawapeleka kwa familia, huwa tunaaga pale kwenye familia, tunakwenda makaburini kama jambo hilo liko tayari, tunamalizia pale kwa wote. Kwa hiyo, utamaduni mwingine wa kwenda kwenye viwanja na kadhalika hata kama awe ni Mbunge wa chama gani, Spika hawezi kwenda kwenye viwanja vya aina hiyo, haiwezekani.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, napenda tu niliweke sawasawa jambo hili na niwaombe rafiki zangu akina Selasini na wengine ambao tunashiriki vikao na tunaamua kwa pamoja, halafu mkitoka huko mnamahamia *facebook* na mnaanza kusema maneno ya ajabu na ninyi ni watu wazima tunaheshimiana, kidogo haipendezi, kama mtataka tuwe tunajibishana hatua kwa hatua, kila hatua tunajibishana na kuwaumbua na nini linakuwa ni jambo ambalo halitawaletea heshima kwenye majimbo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni vizuri tunapokuwa kwenye kikao na wewe mwenyewe umehudhuria na umeshiriki, unafahamu jambo lenyewe mwanzo mwisho, halafu tena wewe ndiye unakuwa namba moja kuzungumza mambo ambayo hayana mantiki na ku-*confuse* watu ni jambo ambalo halina maana hata kidogo.

Tunawashuruku wale wote waliotupa ushirikiano mahali popote katika jambo hili. (Makofi)

Katibu tuendeleo.

NDG. LINAH KITOSI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Fedha na Mipango

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango tafadhali, karibu sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/2019. Aidha, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na busara ya kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vema majadiliano ya mapendekezo ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2018/2019. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, kwa kuchaguliwa tena, pamoja na Mwenyekiti mpya, Mheshimiwa Jitu Soni. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru

Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyotoa ambayo yamesaidia sana katika kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbo, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Mheshimiwa Justin Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini; Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido; na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha, lakini pia Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa kuchaguliwa kuwakilisha wananchi wa majimbo yao katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mheshimiwa Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji – Mbunge wa Kondo na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano anaonipatia katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango unafanikiwa. Aidha, nawashukuru Bw. Doto James, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Shaaban, Dkt. Khatibu Kazungu na Bi. Susan Mkapu kwa kusimamia vizuri shughuli za kila siku za kiutendaji za Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza kwa dhati Profesa Florence Luoga, Gavana mpya wa Benki Kuu ya Tanzania na kumshukuru yeye pamoja na Bw. Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kusimamia kwa weledi taasisi nyeti walizokabidhiwa. Nawashukuru pia, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zote zilizoko chini ya Wizara,

Wakuu wa Vitengo na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kutimiza wajibu wao vema wa kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imejikita katika maeneo makuu mawili. Kwanza, ni Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/2018 na pili ni Malengo na Maombi ya fedha kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka huu wa fedha unaoenda ukingoni.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia mafungu tisa ya kibajeti pamoja na taasisi na mashirika 36 yaliyo chini yake na tumeonesha kwenye jedwali la kwanza ukurasa 136 wa kitabu cha hotuba. Mafungu hayo ni: Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 – Deni la Taifa; Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 – Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu; Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 66 – Tume ya Mipango; na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na muhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa nne hadi ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2017/2018. Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018 ambayo yameainishwa katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 10 mpaka ukurasa wa 81.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla. Katika kutekeleza jukumu hili Wizara ilijikita katika kuhakikisha kuwa malengo ya ukuaji uchumi, mfumuko wa bei na mapato na matumizi ya Serikali yanafikiwa. Katika

mwaka 2017 kasi ya ukuaji wa uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha na kufikia wastani wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, ukuaji huo ulichangiwa na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta ya madini na uchimbaji wa mawe ambayo ilikua kwa asilimia 17.5; sekta ya maji asilimia 16.7; sekta ya uchukuzi na uhifadhi mizigo asilimia 16.6; na sekta ya habari na mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 14.7.

Mheshimiwa Spika, wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.3 na umeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.8 mwezi Aprili, 2018. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za kigeni, kuimarika kwa uzalishaji wa umeme, utekelezaji thabiti wa sera za fedha, urari wa malipo, kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni pamoja na usimamizi wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapato ya kodi kwa mwaka 2017/2018 yanatarajiwa kufikia asilimia 13.0 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 13.3 mwaka 2016/2017. Aidha, nakisi ya bajeti inatarajia kufikia asilimia 2.1 mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa; katika mwaka 2017/2018, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019. Mpango huu ni wa tatu katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Utekelezaji wa Mpango utasaidia kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hivyo Serikali inaendelea kuandaa mazingira wezeshi ili kuhuisha ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imekamilisha na kuchapisha Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa

Maendeleo wa Miaka Mitano. Mkakati huo unatoa mwongozo wa utekelezaji wa Mpango huo ambao utaiwezesha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025. Mkakati unalenga maeneo yafuatayo:-

Viwanda vya nguo, ngozi, madawa, maeneo maalum ya kiuchumi, ukuaji wa miji na usimamizi wa maendeleo ya miji.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa ya Maendeleo iliyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ilifanya ufuatiliaji wa miradi 29 katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Pwani, Iringa na Mbeya. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha miradi ya sekta ya umma na binafsi na sekta za viwanda, kilimo, uvuvi, maji, afya, elimu, mifugo, ujenzi na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya ufuatiliaji yalikuwa kubainisha hatua halisi za utekelezaji wa miradi husika, changamoto na hatua stahiki za kuzitatua ili yazingatiwe katika maandalizi ya mpango wa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini. Wizara imekamilisha taarifa ya mwanzo ya Hali ya Umaskini na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2016/2017. Taarifa hii inabainisha mwelekeo wa hali ya umaskini, changamoto na jinsi ya kukabiliana nazo. Aidha, imeonesha viashiria vitakavyotumika na kubainisha wapi tulipoanzia (*baselines*) ili kupima mafanikio katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inaonesha mafanikio yafuatayo:-

Wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 63.3 mwaka 2015 na kufikia miaka 64.4 mwaka 2017;

vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka wastani wa vifo 38 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 34.5 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2017. Pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka Sh.1,918,931 mwaka 2015 na kufikia Sh.2,275,601 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 18.6. Kuongezeka kwa umiliki wa samani katika kaya nao umeongezeka na upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya ya jamii, maji safi na salama, umeme na miundombinu ya barabara umekuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya umasikini nchini iliyofanyika mwaka 2015/2016 kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki ya Dunia ilionesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi (*basic need poverty*) umeendelea kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 26.4 mwaka 2015/2016. Malengo ya Serikali ni kupunguza umaskini hadi kufikia asilimia 12.7 mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kubainisha hali ya umaskini hususani wa kipato, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Benki ya Dunia hivi sasa inaendesha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (*Household Budget Survey*) kwa mwaka 2017/2018. Hatua iliyofikiwa ni ukusanyaji wa takwimu za mapato na matumizi ya kaya kwa miezi sita ya kwanza ya 2018 katika mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo tunatarajia kuwa matokeo rasmi ya hali halisi ya umaskini na hususan wa kipato katika ngazi ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya yatatolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Machi, 2019. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote kwamba katika kitabu changu cha Hotuba ukurasa wa 13 sehemu hii ya Mikakati ya Kupunguza Umaskini isomeke kama nilivyosoma sasa.

Mheshimiwa Spika, nne, Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali, nikianza na Mapato ya Ndani. Katika mwaka 2017/2018 sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi trilioni 19.9 ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi

Aprili, 2018 jumla ya makusanyo ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi trilioni 14.8, sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 12.6, sawa na asilimia 74 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 17.1. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 1.78 sawa na asilimia 82 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 2.18; na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 437.6, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya shilingi bilioni 687.3 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, vile vile, hadi kufikia Aprili 2018, Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 4.9 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 80 ya shilingi trilioni 6.1 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 4.12 zilikopwa kwa ajili ya kulipia dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva (*rollover*) na shilingi bilioni 832.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, mikopo kutoka kwenye chanzo hiki, ilielekezwa kulipia sehemu ya madeni ya wakandarasi wa barabara, maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, Misaada na Mikopo nafuu toka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2018 Serikali imepokea kiasi cha shilingi trilioni 1.86 sawa na asilimia 47 ya lengo la shilingi trilioni 3.9 na kati ya kiasi kilichopokelewa, shilingi bilioni 70.2 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, sawa na asilimia saba ya ahadi ya shilingi bilioni 941.26; shilingi bilioni 180.52 ni mifuko ya pamoja ya kisékta sawa na asilimia 33 ya ahadi ya shilingi bilioni 556.08 na shilingi bilioni 1,612.6 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 65 ya ahadi ambayo ilikuwa ni shilingi trilioni 2.47.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na sekta, washirika wa maendeleo na wadau wengine ilifanikiwa kuandaa na kukamilisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework*) ambao uliidhinishwa na Serikali mwezi Agosti 2017. Mwongozo huu

umeanza kutekelezwa mwaka 2017/2018 na utadumu hadi 2024/2025. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayonufaika na fedha za nje ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tano, ni Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Katika uandaaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018, Wizara ilifanya uboreshaji wa mfumo wa uandaaji na usimamizi ya Bajeti ya Serikali (*Central Budget Management System*) ambao umeanza kutumika rasmi katika uandaaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Pamoja na mambo mengine, mfumo huo utarahisisha utoaji na uchambuzi wa taarifa za mapato na matumizi na pia na utaondoa kabisa tatizo la uingizwaji wa takwimu za bajeti mara mbili kama ilivyokuwa kwenye mifumo iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

Kuendesha mafunzo ya mfumo wa *CBMS* kwa maofisa 246 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa; Kuandaa, kuweka kwenye tovuti ya Wizara, kuchapisha na kusambaza nakala 3,000 za Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2018/2019; Ukamilishaji wa Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 Juzuu Na. I, II, III na IV ambapo nakala 2,150 zilichapishwa na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na pia kusambazwa kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa na Wadau wengine; na Uandaaji wa Kijitabu cha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018 Toleo za Wananchi (*Citizens Budget*) kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, sita, ni Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi; katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya uhakiki wa madeni ya Serikali kama ifuatavyo:-

Uhakiki wa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF, PPF, PSPF, GEPF, LAPF na NHIF*); Uhakiki wa madeni ya Mamlaka ya Uchimbaji Visima (*DDCA*) uliofanyika katika Halmashauri mbalimbali za Mikoa ya Katavi, Morogoro, Arusha, Pwani na Lindi ambapo kiasi cha shilingi Trilioni 1.1 kiliokolewa kutokana na uhakiki huo; na Uhakiki wa madeni ya Wizara, Idara Zinzajitegemea, Wakala za Serikali 61 na Sekretarieti za Mikoa 26 umekamilika. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi maalum katika maeneo yafuatayo:-

Hospitali Teule ya Mvumi Dodoma; Mradi wa *SELF Microfinance Fund*, kuchunguza ukwepaji wa kodi katika Biashara ya vinywaji vikali; kukagua mfumo wa kukusanya maduhuli na Wakala wa Usafiri wa Mwendu wa Haraka (*DART*) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na kiasi kikubwa ambacho kimeokolewa baada ya kufanya uhakiki, naomba kusisitiza kuwa Wizara yangu itaendelea kuhakiki madeni yote kabla ya kuyalipa. Kama tungelipa madeni haya bila kujiridhisha tungekuwa tumepoteza fedha nyingi sana za wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yaliyotekelezwa chini ya Usimamizi na Udhhibiti wa Fedha za Umma ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 19 hadi 24.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Malipo; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa malipo kwa kuunganisha mfumo wa malipo wa *TISS* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Tabora na Kigoma. Aidha, mfumo wa *TISS* umeunganishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 25 na 37), Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57), Jeshi la Polisi (Fungu 28), Jeshi la Wananchi (Fungu 38), Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 39) na kuwapatia mafunzo Watumishi ili kuwawezesha kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara imesimika mfumo wa malipo (*EPICOR*) kwenye Ubalazi wa Tanzania kule Nairobi-Kenya kwa lengo la kudhibiti matumizi nje ya bajeti. Kadhalika, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya viwango vya kimataifa (*IPSAS*) kwenye uandaaji wa Hesabu kwa Wahasibu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma 650 na kuwezesha kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa kutumia Viwango vya Kimataifa (*IPSAS Accrual Basis*).

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali; Serikali imeendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134. Mwezi Novemba 2017, Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kwa kipindi kilichoishia Juni, 2017. Tathmini hiyo inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Spika, Uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 34.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56; thamani ya sasa ya deni la nje pekee kwa pato la Taifa ni asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250.

Mheshimiwa Spika, kazi ya viashiria hivyo vinne ni kupima uwezo wa nchi kukopa. Viashiria vilivyobaki vinapima uwezo wa nchi kulipa deni. Kutokana na tathmini, ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani umefikia asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Kwa kuzingatia vigezo hivyo Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kukopa ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo iliyoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhimilivu huo wa deni Serikali imeendelea kuchukua tahadhari kwa kukopa kwenye vyanzo vyenye masharti ya gharama nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo itakayochochea ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na ujenzi wa mitambo ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kila robo mwaka inapitia viwango vya Deni la Serikali ili kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu. Vile vile, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha ukaguzi wa deni hilo na Serikali inapitia taarifa hiyo kwa lengo la kuzingatia ushauri uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya malipo ya deni la Serikali iko katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 26 hadi 28.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha; katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea na kazi ya kuboresha Mfumo wa kutolea taarifa za kulipia mishahara kwa watumishi wa umma kwa njia ya kielektroniki, ambapo mfumo wa kutolea taarifa za malipo ya mishahara ya watumishi wa umma na hati za mishahara (*Government Salary Slip Portal*) umekamilika na kuanza kutumika mwezi Julai, 2017. Watumishi wa umma wanaweza kupata hati za mishahara kwa njia za kielektroniki mahali popote palipo na mtandao. Aidha, maboresho haya yamepunguza gharama kubwa za usambazaji wa taarifa za mishahara.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imesimika mfumo wa makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi, (*Government electronic Payment Gateway - GePG*) ambapo hadi sasa taasisi 86 zimeunganishwa na kati ya hizo taasisi 51 zimeanza kukusanya maduhuli kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mali za Serikali; ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora wa mali za Serikali,

Wizara imeendelea kufanya uthamini wa mali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Hadi Aprili 2018, uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali katika mafungu 48 ulifanyika ili kuwa na taarifa sahihi za mali za Serikali za mafungu hayo. Aidha, Wizara imefanya uhakiki maalum wa mali za watu binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali katika vituo 145 vya Polisi Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa fidia zinazotokana na upungufu wa uangalizi na usimamizi wa mali hizo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika katika usimamizi wa mali za Serikali ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 31 mpaka 32.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Umma; katika mwaka 2017/2018, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Ununuzi na Ugavi 75 juu ya matumizi ya mfumo wa uagizaji wa mahitaji ya hati ya ununuzi (*Local Purchase Order-LPO's*) kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (*Epicor*); na kukamilisha zoezi la tathmini ya Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa matokeo ya zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa chini ya ununuzi wa umma, rufani za zabuni za umma, huduma ya ununuzi Serikalini na kupitia Bodi ya Watalaam wa Ununuzi na Ugavi ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 32 mpaka 35.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Ofisi ilifanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali Zinazojitegemea 55, Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Wakala za Serikali 37, Mifuko Maalum 15, Taasisi nyingine za Serikali 60 na Balozi za Tanzania nje ya nchi 40. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 na Mashirika ya Umma 105.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine za ukaguzi wa hesabu za Serikali zilizofanyika ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 35 mpaka 37.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma; katika mwaka 2017/2018, Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini na uchambuzi wa mikataba ya utendaji Kazi 31 iliyoingiwa baina ya Msajili wa Hazina na Wenyevitani wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma katika mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, lengo la zoezi hilo ni kupima utekelezaji wa mikataba hiyo kwa mujibu wa viashiria vya mafanikio, ambapo mambo ya msingi yanayozingatiwa katika tathmini ni pamoja na utawala bora, usimamizi wa fedha, usimamizi wa rasilimali watu na huduma kwa mteja. Katika zoezi la mikataba ya utendaji, kigezo ni taasisi husika kuwa na bodi hai na kuwa na bajeti iliyoidhinishwa. Matokeo ya tathmini yanaonesha wastani wa taasisi kufanya vizuri kwa asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kufanya uchambuzi wa taasisi na mashirika ya umma ambayo majukumu yao kwa namna moja au nyingine yanafanana kwa lengo la kuunganisha taasisi hizo ili kuongeza tija na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kusimamia mashirika na taasisi za umma ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 37 mpaka 39.

Mheshimiwa Spika, Mafao ya Wastaafu na Mirathi; katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi trilioni 1.0 kwa ajili ya kulipia michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Hadi kufikia Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 716.19 sawa na asilimia 71 kilitumika kulipa michango ya mwajiri kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuiagiza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iandikishe wanachama wake, kuwapa vitambulisho vya uanachama na kutunza vizuri na kwa usahihi taarifa za uchangiaji kwa kipindi chote cha utumishi wa wanachama ili kuwaondolea usumbufu siku za kustaafu kwao kama ilivyoelekezwa na Miongozo ya Mamlaka ya Udhubiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nawakumbusha watumishi wa umma wawe na tabia ya kukagua taarifa za madaraja ya mishahara, makato ya lazima na yale yasiyo ya lazima kutoka kwenye mishahara yao na kutoa taarifa kwa wakati kwa mamlaka husika ili kama kuna makato hayako sawasawa mamlaka husika zichukue hatua za kurekebisha mapema na kuisaidia Serikali kuepuka tozo zinazoweza kutozwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kusimamia mafao ya wastaafu na mirathi ni kama ilivyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 39 mpaka 41.

Mheshimiwa Spika, Udhubiti wa Utakatishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi; katika mwaka 2017/2018, Kitengo cha Udhubiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi kimeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhubiti wa Fedha Haramu na kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupokea na kuchambua taarifa 254 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kuwasilisha taarifa za kiintelijensia 32 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, katika kujenga uwezo wa watumishi, maafisa wa kitengo walipata mafunzo ya namna bora ya uchambuzi na upembuzi wa taarifa za miamala shuku katika Kituo cha Kudhibiti Fedha Haramu (*Financial Intelligence Centre*) cha Afrika ya Kusini na Maafisa wanne (4) walihudhuria mafunzo ya *Financial Action Task Force*

Standards yaliyofanyika nchini Korea Kusini ambayo ni muhimu katika nyanja ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kusimamia utekelezaji wa Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi ni kama ilivyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya kuanzia ukurasa wa 41 mpaka 43.

Mheshimiwa Spika, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuratibu na kuchambua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, kulingana na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, uchambuzi wa miradi ya ubia hupitia hatua tatu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mamlaka za utekelezaji kuwasilisha andiko la awali la mradi kwa ajili ya uchambuzi; pili, mamlaka kuandaa taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu; na tatu mamlaka ya utekelezaji wa miradi ikishirikiana na Mshauri Mwelekezi huandaa na kuwasilisha taarifa ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hufanya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kuangalia, pamoja na mambo mengine maeneo makuu matatu. Kwanza, ni uhamishaji wa mianya hasi ya mradi kwenda kwa sekta binafsi; pili ni uwezo wa Serikali kugharimia mradi; na tatu ni manufaa ya mradi kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Endapo mradi unakidhi vigezo utaidhinishwa na Kamati ya Wataalam wa *PPP* kwa ajili ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefikia hatua mbalimbali za uchambuzi wa miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*. Upembuzi yakinifu wa mradi wa uzalishaji wa madawa muhimu na vifaa tiba wa Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*) umekamilishwa na kuwasilishwa kwenye kitengo cha ubia kwa ajili ya hatua za uidhinishaji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga na kuendesha vyuo 10 vya VETA kwa utaratibu wa PPP katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Manyara, Tabora na Shinyanga. Wizara imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na kuwasilisha kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mapendekezo yanayotakiwa kuzingatiwa ili mradi uwe na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Barabara ya Tozo kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze. Taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi imefanyiwa uchambuzi ambapo Wizara imetoa idhini yenye masharti (*Conditional Approval*) ya kutekeleza kabla ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza. Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu, mkusanyaji wa mapato na mwendesha Mfuko zilitangazwa na wazabuni wamepatikana; na Wizara imekamilisha uchambuzi wa andiko la awali la mradi wa Mradi wa Mwambani Port lililowasilishwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania; hatua inayoendelea ni maandalizi ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa katika kusimamia utekelezaji wa PPP zimeoneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 44 mpaka 46.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Mashirika ya Umma Chini ya Wizara. Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu inaratibu na kusimamia mashirika na taasisi za umma 36. Utekelezaji wa majukumu ya taasisi na mashirika haya kwa mwaka 2017/2018 ni kama ilivyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 47 mpaka 78.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 yameoneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 79 mpaka 81.

Mheshimiwa Spika, Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na ukwepaji wa kodi, kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya masharti nafuu pamoja na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uelewa mdogo wa wananchi juu ya dhana ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi ambayo ni pana na inabadilika kwa kasi. Pia baadhi ya wawekezaji kutelekeza mali walizouziwa na Serikali wakati wa zoezi la Ubinafsishaji, na uelewa mdogo wa dhana ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Hatua zilizochukuliwa ni zifuatazo:-

Kwanza, ni kutekeleza mkakati wa ulipaji kodi kwa hiari na kuendelea kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kujenga mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato; Kuendelea kuelimisha wadau mbalimbali kupitia makongamano, mikutano na warsha kuhusu dhana ya utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kuendeleza mazungumzo na Washirika wa Maendeleo kuhusu njia mpya za kutoa na kupokea misaada na mikopo; Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeongeza nguvu katika kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wawekezaji wote ili kuhakikisha wanaendesha viwanda na mali walizouziwa kwa kuzingatia masharti ya mikataba ya mauzo; na Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze malengo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2018/2019. Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2015 – 2020), Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na masuala mtambuka kama vile jinsia, watu wenye ulemavu, mazingira, UKIMWI, makundi mengine yaliyo katika

mazingira hatarishi na masuala ya lishe kwa jamii pamoja na maelekezo na ahadi zilizotolewa kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Kwanza kwa upande wa kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla. Katika kipindi cha mwaka wa 2018/19 shabaha zitakuwa ni zifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.1 mwaka 2017;

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2017/2018 na asilimia 15.6 mwaka 2016/2017;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 kutoka matarajio ya asilimia 13 mwaka 2017/2018 na asilimia 13.3 mwaka 2016/2017; na

(v) Nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 kutoka asilimia 2.1 mwaka 2017/2018 na asilimia 1.5 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa; kutokana na kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, imebidi kuupitia muundo wa Wizara ili uweze kuyaingiza mabadiliko haya ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu pamoja na maslahi ya watumishi kwa ujumla. Muundo wa Wizara uko katika hatua za mwisho za kuidhinishwa na mamlaka husika, ambapo imependekewa iundwe Divisheni ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa itakayoongozwa na Kamishna na kuwa na kifungu chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo katika mwaka 2018/2019, shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa katika uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ni pamoja na:

Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020; Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019; Kufanya tathmini ya muda wa kati katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Kukamilisha uundwaji wa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa miradi ya kitaifa ya maendeleo; na Kufuatilia matumizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (*Public Investment Management Operational Manual*).

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini; katika mwaka ujao wa fedha Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa juhudi za kupunguza umaskini ikiwemo:-

Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Jitihada za Kuondoa Umaskini nchini (*Poverty Monitoring System*); Kufuatilia utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika mipango ya kitaifa na kisekta na Malengo ya Maendeleo Endelevu (*SDGs*) ya mwaka 2030 na programu zinazolenga kuondoa umaskini katika maeneo ya vijijini na mijini; Kufanya uchambuzi wa kina juu ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2017/2018; Kutoa mafunzo kwa Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu jitihada za kupambana na umaskini na kutunza mazingira ili kuweza kujumuisha katika mipango na bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, mipango mingine katika uratibu wa Mikakati wa Kupunguza Umaskini iko kwenye hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 87 hadi 89.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Kusimamia sera za fedha na za kibajeti zinazolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; Kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kuimarisha mkakati shirikishi wa

mawasiliano na walipa kodi na kuboresha utaratibu wa utozaji kodi; Kujenga uwezo wa watumishi ili kukabiliana na tatizo la uhamishaji faida (*Transfer Pricing*) unaofanywa na kampuni zenye mitandao ya kimataifa kwa lengo la kukwepa au kupunguza kodi; Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ulipaji kodi kupitia mfumo wa vitalu vya walipakodi; Kusimamia zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ili kuboresha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali; na kuongeza kasi ya uthaminishaji wa majengo ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine iko katika hotuba yango ukurasa wa 89 hadi 90.

Mheshimiwa Spika, Mikopo na Misaada; katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea na uratibu wa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo mbalimbali nchini. Washirika wa maendeleo wameahidi kuchangia Bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 2,676.64. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 545.76 ni kwa ajili ya misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (*General Budget Support*), shilingi bilioni 125.86 kwa ajili ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na shilingi bilioni 2,005.02 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha mpango kazi wa kutekeleza Mwongozo Mpya wa Ushirikiano (*Development Cooperation Framework*); na Kukagua miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Katika mwaka ujao wa fedha Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kuendelea kuboresha mfumo mpya wa uandaaji na

usimamizi wa bajeti ya Serikali ili kurahisisha utoaji wa mgao wa fedha za matumizi kila mwezi na kuendesha mafunzo ya mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho, kuchapisha na kusambaza nakala 2,200 vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2018/2019 kama yalivyopitishwa na Bunge, kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020, Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali za kila Robo Mwaka, vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2019/2020 na kuviwasilisha Bungeni na kuvisambaza kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa kwa wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ziko katika hotuba yangu ukurasa wa 92 hadi ukurasa wa 93.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi ya Serikali; katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa miongozo mbalimbali ya ukaguzi wa ndani iliyotolewa na Wizara na kutoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Ndani katika maeneo ya ukaguzi wa miradi, ukaguzi wa kiufundi, usimamizi wa vihatarishi, mfumo wa usimamizi wa kazi za ukaguzi na mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mipango mingine ambayo Wizara inatarajia kutekeleza katika usimamizi wa udhibiti wa fedha za umma iko katika hotuba yangu ukurasa wa 94 mpaka 95.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Malipo; katika mwaka ujao wa fedha, wizara imepanga kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu (*Treasury Single Account*) kwa lengo la kuboresha mfumo wa matumizi ya umma ili

kuiongezea Serikali uwezo wa kugharamia shughuli zake kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea na usimikaji na usimamizi wa mifumo ya malipo ya kieletroniki ili kuondoa ucheleweshaji wa malipo kwa wadau mbalimbali wakiwemo wastaafu, watoa huduma kwa Serikali pamoja na watumishi wa umma. Vile vile Wizara itaendelea na uunganishaji wa mfumo wa malipo kwenye Balozi saba ili kudhibiti matumizi nje ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali; katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itahakikisha kuwa deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu na kutokuwa mzigo kwa uchumi wetu na kuendelea kuwa fursa na kichocheo cha maendeleo kwa nchi yetu. Aidha, Serikali itaendelea kukopa kwa uangalifu kwa kuzingatia masharti nafuu. Mikopo hiyo itatumika kwenye miradi ya maendeleo ya kuchochea ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mchango wa Mwajiri Kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; Wizara itaendelea kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria ya mwajiri ya kila mwezi kwa ajili ya watumishi wa umma kwenye mfuko mpya wa hifadhi ya jamii utakaochukua nafasi ya mifuko ya hifadhi ya jamii iliyounganishwa ya *PSPF, GEPF, LAPF* na *PPF* pamoja na mifuko ambayo haitaunganishwa ya *NSSF, ZSSF, WCF* na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwasisitiza Maafisa Utumishi wote wanaohusika na kuingiza taarifa za watumishi wa umma kwenye mfumo wa kompyuta wa kutunza taarifa za watumishi wa umma, waingize taarifa za watumishi kwa ukamilifu na kwa usahihi ili uwasilishaji wa michango ya mwanachama na mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwe kamili na sahihi kwa kipindi chote cha utumishi na hatimaye kurahisisha malipo ya mafao, pensheni na mirathi wakati wa hitimisho la utumishi wa umma ili kuwaondolea usumbufu watumishi wa umma walioitumikia nchi yao kwa weledi na uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha; katika mwaka 2018/2019, Wizara imepanga

kusimamia na kuboresha uendeshaji na utumiaji wa mfumo wa taarifa za mishahara ya watumishi wa umma (*Government Salaries Payment Platform*) kwa kuunganisha mfumo huo na taasisi za kibenki na mfumo wa pensheni kwa ajili ya urahisishaji wa huduma za mikopo na pensheni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara itaendelea kuunganisha taasisi 260 katika mfumo wa kukusanya mapato yasiyo ya *kodi* (*Government Electronic Payment Gateway System*) ili kuweza kufanikisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Vile vile Wizara itaunganisha mifumo 10 ya kielektroniki ya taarifa za fedha kwa lengo la kuiwezesha mifumo iweze kubadilishana taarifa.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mali za Serikali; katika mwaka 2018/2019, Wizara imepanga kufanya kaguzi za mali za Serikali katika Balozi kumi, kufanya kaguzi maalum na kutoa elimu ya utumiaji na utunzaji bora wa mali katika taasisi mbalimbali za Serikali ili kuepusha hasara zinazoweza kuzuilika.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Umma; katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara imepanga kufanya yafuatayo:-

Kukamilisha uandaaji na kuzindua Sera ya Ununuzi wa Umma pamoja kuanza utekelezaji wa sera hiyo; Kukusanya maoni ya wadau kuhusu changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma kwa lengo la kuzifanyia marekebisho pale itakapohitajika; Kuwajengea uwezo Maafisa Ununuzi na Ugavi Serikalini juu ya matumizi ya mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi na ugavi; Kuendesha mafunzo kwa Maafisa Ununuzi na Ugavi kuhusu matumizi ya mfumo wa malipo wa *EPICOR* katika ununuzi; Kuandaa mpango kazi wa usimamizi wa ununuzi wa umma katika Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na Kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika katika eneo hili ziko kwenye hotuba yangu ukurasa wa 98 mpaka 101.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali; katika mwaka ujao wa fedha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma. Ili kufikia malengo hayo, ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele vinane kama ifuatavyo:-

Kufanya ukaguzi wa mafungu ya bajeti za Wizara, Idara zinazojitegemea, wakala na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani.

Kufanya ukaguzi wa sekta ya gesi, mafuta na madini, kufanya maboresho ya mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA na kukagua ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Aidha, ofisi imelenga kufanya ukaguzi wa kiufanisi na kaguzi maalum katika maeneo yatakayoainishwa.

Pia kuwajengea wakaguzi uwezo wa kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi kwenye sekta ya gesi asilia na mafuta, sekta ya madini, sekta mtandao na katika uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao (*Financial crimes auditing*). Vile vile, ofisi itaendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Ukaguzi katika Mikoa ya Rukwa na Mara.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambazo zitafanyika kwa upande wa usimamizi wa mashirika na taasisi za umma lakini pia upande wa mafao ya wastaafu na mirathi, upande wa udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, Tume ya Pamoja ya Fedha lakini pia upande wa PPP zote zimeelezwa kwenye kitabu cha hotuba yangu; na naomba yote yaliyopo kwenye kitabu cha hotuba yapokelewe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Maombi ya Fedha kwa mwaka 2018/2019; mwaka ujao wa fedha wizara inakadiria kukusanya maduhuli shilingi bilioni 597.8 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango na mauzo ya leseni za udalali.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha; Wizara ya Fedha na Mipango imepanga kutumia kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 12,058.71 kwa Mafungu yote Nane. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,763.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,295.21 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi bilioni 65.76 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 693.26 kwa ajili ya matumizi mengineyo; na shilingi bilioni 10,004.48 ni malipo ya deni la Serikali na michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, katika fedha za matumizi ya maendeleo, shilingi bilioni 1,266.03 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 29.18 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha; Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango. Kwenye Fungu hili Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida – Sh.57,022,927,000 ambapo mishahara ni shilingi bilioni 7.58 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 49.44. Miradi ya maendeleo Sh.28,790,817,000. Kati ya hizo shilingi bilioni 19.64 ni fedha za ndani na fedha za nje shilingi bilioni 9.15.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina. Wizara inaomba kuidhinishiwa fedha kwa ajili ya Fungu hili kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida Sh. 531,890,056,000. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 21.47 ni mishahara, matumizi mengineyo shilingi bilioni 510.42.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, upande wa miradi ya maendeleo Shilingi bilioni 1,247.61, ambapo fedha za ndani ni bilioni 1,236.19 na fedha za nje ni shilingi bilioni 11.42.

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa. Kwenye Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida Sh.10,013,706,140,000 ambapo mishahara ni shilingi bilioni 9.23 na matumizi mengineyo Shilingi bilioni 10,004.48.

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali. Katika Fungu hili, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida Sh.46,725,409,000. Kati ya fedha hizo mishahara shilingi bilioni 7.91, matumizi mengineyo shilingi bilioni 38.82. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Sh.3,200,000,000 kati ya fedha hizo shilingi 2,000,000,000 ni fedha za ndani na fedha za nje ni shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, Fungu namba 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kwa ajili ya fungu hili, matumizi ya kawaida tunaomba Sh.54,592,065,000; kati ya fedha hizi mishahara ni bilioni 2.36 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 52.23. Miradi ya Maendeleo, Sh.1,650,000,000 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni moja na fedha za nje ni shilingi bilioni 0.65

Mheshimiwa Spika, Fungu namba 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; katika Fungu hili tunaomba Bunge lako Tukufu lituidhinishie matumizi ya kawaida Sh.2,155,075,000 ambapo kati ya hizo mishahara ni bilioni 0.57 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 1.58.

Mheshimiwa Spika, Fungu namba 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu. Katika fungu hili kwa mwaka ujao

wa fedha tunaomba matumizi ya kawaida Bunge lako lituidhinishie Sh.2,015,586,000 na miradi ya maendeleo – Sh.248,363,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kwa fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha tunaomba kuidhinishiwa matumizi ya kawaida Sh.55,394,216,000 ambapo mishahara ni bilioni 16.65 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 38.75. Upande wa miradi ya maendeleo tunaomba Sh.13,712,092,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.20 ni fedha za ndani na bilioni 6.51 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara www.mof.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa hotuba yako hiyo nzuri.

HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2018/19 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 TANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/18 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha 2018/19.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulingoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na busara katika kulingoza Taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vema majadiliano ya mapendekezo ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2018/19. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb.) kwa kuchaguliwa tena pamoja na Makamu Mwenyekiti mpya Mhe. Jitu Vrajlal Soni (Mb.). Aidha, nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyotoa ambayo yamesaidia sana katika kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2018/19.

4. **Mheshimiwa Spika**, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. Damas Ndumbo - Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mhe. Justin Monko – Mbunge wa Singida Kaskazini, Mhe. Dkt. Stephen Kiruswa - Mbunge wa Jimbo la Longido, Mhe. Dkt. Godwin Mollel - Mbunge wa Jimbo la Siha na Mhe. Maulid Mtulia - Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa kuchaguliwa kuwakilisha Wananchi wa majimbo yao katika Bunge lako Tukufu. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mhe. Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini na Mhe. Kasuku Samson Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji - Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano anaonipatia katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango unafanikiwa. Aidha, nawashukuru Bw. Doto James - Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bibi Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu na Bi. Susan Mkapa kwa kusimamia vizuri shughuli za kila siku za kiutendaji za Wizara yangu. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Prof. Florens Luoga - Gavana mpya wa Benki Kuu ya Tanzania na kumshukuru yeye pamoja na Bw. Charles Kichere - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Dkt. Albina Chuwa – Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kwa kusimamia kwa weledi taasisi nyeti walizokabidhiwa. Nawashukuru pia, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zote zilizoko chini ya Wizara, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kutimiza wajibu wao vema wa kuwatumikia Watanzania.

6. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu imejikita katika maeneo makuu mawili yafuatayo: Kwanza, ni Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18 na pili, Malengo na Maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/19.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia mafungu tisa ya kibajeti pamoja na Taasisi na Mashirika 36 yaliyo chini yake (**Jedwali Na. 1 ukurasa 136**). Mafungu hayo ni Fungu 50-Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 21-Hazina, Fungu 22-Deni la Taifa, Fungu 23-Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10-Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13-Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 7- Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 66-Tume ya Mipango na Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

8. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na muhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 4 hadi ukurasa wa 9**.

2.1 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2017/18

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/18 ambayo yameainishwa katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 10 hadi ukurasa wa 81**.

2.1.1 Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

10. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imejikita katika kuhakikisha kuwa malengo ya ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, na mapato na matumizi ya Serikali yanafanikiwa. Katika mwaka 2017, kasi ya ukuaji wa uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha na kufikia wastani wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2016. Ukuaji huo ulichangiwa na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta ya madini na uchimbaji mawe (asilimia 17.5), sekta ya maji

(asilimia 16.7), sekta ya uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 16.6) na sekta ya habari na mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 14.7.

11. *Mheshimiwa Spika*, wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.3 na umeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.8 mwezi Aprili, 2018. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za kigeni, kuimarika kwa uzalishaji wa umeme, utekelezaji thabiti wa sera za fedha, urari wa malipo, kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni pamoja na usimamizi wa bajeti ya Serikali. Mapato ya kodi kwa mwaka 2017/18 yanatarajia kufikia asilimia 13.0 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 13.3 mwaka 2016/17. Aidha, nakisi ya bajeti inatarajia kufikia asilimia 2.1 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2016/17.

2.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

12. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19. Mpango huu ni wa tatu katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21). Utekelezaji wa Mpango utasaidia Taifa kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hivyo, Serikali inaendelea kuandaa mazingira wezeshi ili kuhuisha ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Aidha, Wizara imekamilisha na kuchapisha Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17-2020/21. Mkakati huo unatoa mwongozo wa utekelezaji wa Mpango huo ambao utaiwezesha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025. Mkakati unalenga maeneo yafuatayo: viwanda vya nguo, ngozi, madawa, maeneo maalum ya kiuchumi, ukuaji wa miji na usimamizi wa maendeleo ya miji.

13. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa ya Maendeleo iliyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ilifanya ufuatiliaji wa miradi 29 katika mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Pwani, Iringa na Mbeya. Miradi iliyofuatiwa ilijumuisha miradi ya sekta ya Umma na Binafsi, na sekta za Viwanda, Kilimo, Uvuvi, Maji, Afya, Elimu, Mifugo, Ujenzi na Miundombinu. Malengo makuu ya ufuatiliaji yalikuwa kubainisha hatua halisi za utekelezaji wa miradi husika, changamoto na hatua stahiki za kuzitatua ili yazingatiwe katika maandalizi ya Mpango wa mwaka 2018/19.

2.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

14. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha Taarifa ya mwanzo ya Hali ya Umaskini na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2016/17. Taarifa hii inabainisha mwelekeo wa hali ya umaskini, changamoto na jinsi ya kukabiliana nazo. Aidha, imeonesha viashiria vitakavyotumika na kubainisha wapi tulipoanzia (baselines) ili kupima mafanikio katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030.

15. **Mheshimiwa Spika**, taarifa hiyo inaonesha mafanikio yafuatayo: wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 63.3 mwaka 2015 na kufikia miaka 64.4 mwaka 2017; vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka wastani wa vifo 38 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 34.5 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2017; Pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka shilingi 1,918,931 mwaka 2015 na kufikia shilingi 2,275,601 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 18.6; kuongezeka kwa umiliki wa samani katika kaya nao umeongezeka na upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya ya jamii, maji safi na salama, umeme na miundombinu ya barabara umekuwa bora zaidi.

16. **Mheshimiwa Spika**, tathmini ya hali ya umaskini nchini iliyofanyika mwaka 2015/16 kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki ya Dunia ilionesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi umeendelea kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2015/16. Malengo ya Serikali ni kupunguza umaskini hadi kufikia asilimia 12.7 mwaka 2025/26. Hata hivyo, ili kubainisha hali ya umaskini hususan wa kipato, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Benki ya Dunia hivi sasa inaendesha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey -HBS) kwa mwaka 2017/18. Hatua iliyofikiwa ni ukusanyaji wa takwimu za mapato na matumizi ya kaya kwa miezi sita ya kwanza ya 2018 katika mikoa yote. Kwa msingi huo tunatarajia kuwa matokeo rasmi ya hali halisi ya umaskini na hususan wa kipato katika ngazi ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya yatatolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Machi, 2019.

2.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

(a) Mapato ya Ndani

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, sera za mapato zililinga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 19,977.0 ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Aprili, 2018 jumla ya makusanyo ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 14,838.5, sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 12,611.0 sawa na asilimia 74 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 17,106.4; mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 1,789.9 sawa na asilimia 82 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 2,183.4; na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 437.6, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya shilingi bilioni 687.3 kwa mwaka.

Vile vile, hadi kufikia Aprili 2018, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 4,958.0 kutoka soko la ndani sawa na asilimia

80 ya shilingi bilioni 6,168.9 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,125.7 zilikopwa kwa ajili ya kulipia dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva (rollover), na shilingi bilioni 832.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, mikopo kutoka kwenye chanzo hiki, ilielekezwa kulipia sehemu ya madeni ya wakandarasi wa barabara na maji na umeme.

(b) Misaada na Mikopo nafuu toka kwa Washirika wa Maendeleo

18. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Aprili 2018 Serikali imepokea kiasi cha shilingi bilioni 1,865.76 sawa na asilimia 47 ya lengo la shilingi bilioni 3,971.10. Kati ya kiasi kilichopokelewa, shilingi bilioni 70.2 ni Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS) sawa na asilimia 7 ya ahadi ya shilingi bilioni 941.26, shilingi bilioni 180.52 ni za mifuko ya pamoja ya kisekta sawa na asilimia 33 ya ahadi ya shilingi bilioni 556.08 na shilingi bilioni 1,612.61 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 65 ya ahadi ya shilingi bilioni 2,473.77.

19. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Sekta, Washirika wa Maendeleo, na Wadau wengine ilifanikiwa kuandaa na kukamilisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework - DCF*) ambao uliidhinishwa na Serikali mwezi Agosti 2017. Mwongozo huu umeanza kutekelezwa mwaka 2017/18 na utadumu hadi 2024/25. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayonufaika na fedha za nje ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumiwa kwa mujibu wa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

2.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

20. *Mheshimiwa Spika*, katika uandaaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18, Wizara ilifanya Uboreshaji wa Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi ya

Bajeti ya Serikali (Central Budget Management System – CBMS) ambao umeanza kutumika rasmi katika uandaaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Pamoja na mambo mengine, mfumo huo utarahisisha utoaji na uchambuzi wa taarifa za mapato na matumizi na pia na utaondoa kabisa tatizo la uingizwaji wa takwimu za bajeti mara mbili kama ilivyokuwa kwenye mifumo iliyopita.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendesha mafunzo ya mfumo wa CBMS kwa maofisa 246 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa; kuandaa, kuweka kwenye tovuti ya wizara, kuchapisha na kusambaza nakala 3,000 za Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2018/19; ukamilishaji wa Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19 Juzuu Na. I, II, III na IV ambapo nakala 2,150 zilichapishwa na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na pia kusambazwa kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa na Wadau wengine; na uandaaji wa Kijitabu cha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18 Toleo za Wananchi (Citizens Budget) kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

2.1.6 Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya uhakiki wa madeni ya Serikali kama ifuatavyo: Uhakiki wa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (NSSF, PPF, PSPF, GEPIF, LAPF na NHIF), uhakiki wa madeni ya Mamlaka ya Uchimbaji Visima (DDCA) uliofanyika katika Halmashauri mbalimbali za mikoa ya Katavi, Morogoro, Arusha, Pwani na Lindi ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1,166.85 kiliokolewa kutokana na uhakiki huo; na uhakiki wa madeni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali 61 na Sekretariati za Mikoa 26 umekamilika. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi maalum katika maeneo yafuatayo; Hospitali Teule ya Mvumi Dodoma; Mradi wa *SELF Microfinance Fund*, kuchunguza ukwepaji wa kodi katika Biashara ya vinywaji vikali; Kukagua mfumo wa kukusanya

maduhuli (ITS/AFCS system) wa Wakala wa Usafiri wa Mwendu wa Haraka (DART) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

22. *Mheshimiwa Spika*, majukumu mengine yaliyotekelezwa chini ya Usimamizi na Udhibiti wa fedha za Umma ni kama inavyooneshwa kwenye kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 19 hadi ukurasa wa 24**.

2.1.7 Usimamizi wa Malipo

23. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa malipo kwa kuunganisha mfumo wa malipo wa TISS katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Tabora na Kigoma. Aidha, mfumo wa TISS umeunganishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 25 na 37), Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57), Jeshi la Polisi (Fungu 28), Jeshi la Wananchi (Fungu 38), Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 39) na kuwapatia mafunzo Watumishi ili kuwawezesha kutumia mfumo huo. Vile vile, Wizara imesimika mfumo wa malipo (EPICOR) kwenye ubalozi wa Tanzania kule Nairobi-Kenya kwa lengo la kudhibiti matumizi nje ya bajeti. Kadhalika, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya viwango vya kimataifa (IPSAS) kwenye uandaaji wa Hesabu kwa Wahasibu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma 650 na kuwawezesha kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa mwaka wa fedha 2016/17 kwa kutumia Viwango vya Kimataifa (IPSAS Accrual Basis).

2.1.8 Deni la Serikali

24. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134. Mwezi Novemba 2017, Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Serikali kwa kipindi kilichoishia Juni 2017. Tathmini hiyo inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu.

Uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 34.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56; thamani ya sasa ya Deni la nje pekee kwa pato la Taifa ni asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250.

25. Mheshimiwa Spika, kazi ya viashiria hivyo vinne ni kupima uwezo wa nchi kukopa. Viashiria vilivyobaki vinapima uwezo wa nchi kulipa deni. Kutokana na tathmini, ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani umefikia asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje.

26. Mheshimiwa Spika, Pamoja na uhimilivu huo Serikali imeendelea kuchukua tahadhari kwa kukopa kwenye vyanzo vyenye masharti na gharama nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo itakayo chochea ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na ujenzi wa mitambo ya kufua Umeme. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kila robo mwaka inapitia viwango vya Deni la Serikali ili kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu. Vile vile, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha ukaguzi wa deni hilo na Serikali inapitia taarifa hiyo kwa lengo la kuzingatia ushauri uliotolewa.

27. Mheshimiwa Spika, taarifa ya malipo ya Deni la Serikali iko katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 26 hadi ukurasa wa 28.**

2.1.9 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha

28. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea na kazi ya kuboresha Mfumo wa kutolea taarifa za kulipia mishahara kwa watumishi wa Umma kwa njia ya Kielektroniki (*Government Salaries Payment Platform and Government Online Salary Slip Portal*) ambapo mfumo wa kutolea taarifa za malipo ya Mishahara ya watumishi wa Umma na hati za mishahara (*Government Salary Slip Portal*) ulikamilika na kuanza kutumika mwezi Julai, 2017. Watumishi wa umma wanaweza kupata hati za mishahara kwa njia ya kielektroniki mahala popote palipo na mtandao. Aidha, maboresho haya yamepunguza gharama kubwa za usambazaji wa taarifa za mishahara. Pia Wizara imesimika mfumo wa makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi, (*Government electronic Payment Gateway - GePG*) ambapo hadi sasa taasisi 86 zimeunganishwa na kati ya hizo taasisi 51 zimeanza kukusanya maduhuli kwa njia ya kielektroniki.

2.1.10 Usimamizi wa Mali za Serikali

29. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora wa Mali za Serikali, Wizara imeendelea kufanya uthamini wa mali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Hadi Aprili 2018, uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali katika Mafungu 48 ulifanyika ili kuwa na taarifa sahihi za mali za Serikali za Mafungu hayo. Aidha, Wizara imefanya uhakiki maalum wa Mali za Watu binafsi zilizochini ya uangalizi wa Serikali kwa vituo 145 vya Polisi Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa fidia zinazotokana na upungufu wa uangalizi na usimamizi wa Mali hizo.

30. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizofanyika katika usimamizi wa Mali za Serikali ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu **ukurasa wa 31-32**.

2.1.11 Ununuzi wa Umma

31. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi 75

juu ya matumizi ya mfumo wa uagizaji wa mahitaji wa Hati ya Ununuzi (*Local Purchase Order-LPO*) kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (Epicor); na kukamilisha zoezi la tathmini ya Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa matokeo ya zoezi hilo.

32. *Mheshimiwa Spika*, shughuli nyingine zilizotekelezwa chini ya Ununuzi wa Umma, Rufaa za Zabuni za Umma, Huduma ya Ununuzi Serikalini, na kupitia Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 32 hadi ukurasa wa 35**.

2.1.12 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

33. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17. Ofisi ilifanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea 55, mikoa yote 26 ya Tanzania Bara; Wakala za Serikali 37, Mifuko maalum 15, Taasisi nyingine za Serikali 60, Balozi za Tanzania nje ya nchi 40. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 na Mashirika ya Umma 105.

34. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali zilizofanyika ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 35 hadi ukurasa wa 37**.

2.1.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

35. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini na uchambuzi wa Mikataba ya Utendaji Kazi 31 iliyoingiwa baina ya Msajili wa Hazina na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma katika mwaka 2016/17. Lengo la zoezi hilo ni kupima utekelezaji wa mikataba hiyo kwa mujibu wa viashiria vya mafanikio ambapo mambo ya msingi yanayozingatiwa

katika tathmini ni pamoja na: utawala bora; usimamizi wa fedha; usimamizi wa rasilimali watu; na huduma kwa mteja. Katika zoezi la Mikataba ya Utendaji, kigezo ni taasisi husika kuwa na bodi hai na kuwa na bajeti iliyoidhinishwa. Matokeo ya tathmini yanaonesha wastani wa taasisi kufanya vizuri kwa asilimia 70.

36. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kufanya uchambuzi wa taasisi na mashirika ya umma ambayo majukumu yao kwa namna moja au nyingine yanafanana kwa lengo la kuunganisha taasisi hizo ili kuongezea tija na kupunguza gharama za uendeshaji.

37. *Mheshimiwa Spika*, shughuli zingine zilizotekelezwa katika kusimamia Mashirika na Taasisi za Umma ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 37 hadi ukurasa wa 39**.

2.1.14 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

38. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,008.61 kwa ajili ya kulipia michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 716.19 sawa na asilimia 71 kilitumika kulipa michango ya mwajiri kwa watumishi wa umma. Aidha, nitumie fursa hii kuiagiza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iandikishe wanachama wake, kuwapa vitambulisho vya uanachama na kutunza vizuri na kwa usahihi taarifa za uchangiaji kwa kipindi chote cha utumishi wa wanachama ili kuwaondolea usumbufu siku za kustaafu kwao kama ilivyoelekezwa na Miongozo ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Vile vile, ninawakumbusha watumishi wa Umma wawe na tabia ya kukagua taarifa za madaraja ya mishahara, makato ya lazima na yale yasiyo ya lazima kutoka kwenye mishahara yao na kutoa taarifa kwa wakati kwa mamlaka husika ili kama kuna makato hayako sawasawa mamlaka husika zichukue hatua za kurekebisha mapema na

kuisaidia Serikali kuepuka tozo zinazoweza kutozwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi nyingine za fedha.

39. Mheshimiwa Spika, shughuli zingine zilizotekelezwa katika kusimamia Mafao ya Wastaafu na Mirathi ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 39 hadi ukurasa wa 41**.

2.1.15 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi kimeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kufanya yafuatayo: Kupokea na kuchambua taarifa 254 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kuwasilisha taarifa za kiintelijensia 32 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, katika kujenga uwezo wa watumishi, Maafisa wa Kitengo walipata mafunzo ya namna bora ya uchambuzi na upembuzi wa taarifa za miamala shuku katika Kituo cha Kudhibiti Fedha Haramu (Financial Intelligence Centre – FIC) cha Afrika ya Kusini na Maafisa wanne (4) walihudhuria mafunzo ya *Financial Action Task Force (FATF)* standards yaliyofanyika nchini Korea Kusini ambayo ni muhimu katika nyanja ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

41. Mheshimiwa Spika, shughuli zingine zilizotekelezwa katika kusimamia utekelezaji wa Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 41 hadi ukurasa wa 43**.

2.1.16 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuratibu na kuchambua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuishauri Serikali

juu ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, kulingana na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103; uchambuzi wa miradi ya Ubia hupitia hatua tatu zifuatazo; (i) Mamlaka za utekelezaji kuwasilisha andiko la awali la mradi kwa ajili ya uchambuzi (ii) Mamlaka kuandaa taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu (iii) Mamlaka ya utekelezaji wa miradi ikishirikiana na Mshauri Elekezi kuandaa na kuwasilisha Taarifa ya Upembuzi Yakinifu.

Wizara hufanya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kuangalia, pamoja na mambo mengine maeneo makuu matatu: (a) Uhamishaji wa mianya hasi ya mradi kwenda kwa sekta binafsi; (b) Uwezo wa Serikali kugharimia mradi; na (c) Manufaa ya mradi kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Endapo mradi unakidhi vigezo utaidhinishwa na Kamati ya Wataalam wa PPP kwa ajili ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia.

43. Mheshimiwa Spika, Wizara imefikia hatua mbalimbali za uchambuzi wa miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Uzalishaji wa Madawa muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Madawa (MSD) umekamilishwa na kuwasilishwa kwenye Kitengo cha Ubia kwa ajili ya hatua za uidhinishaji; Mradi wa Kujenga na Kuendesha Vyuo 10 vya VETA kwa Utaratibu wa PPP katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Manyara, Tabora na Shinyanga.

Wizara imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na kuwasilisha kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mapendekezo yanayotakiwa kuzingatiwa ili mradi uwe na tija kwa Taifa; Mradi wa Barabara ya Tozo kutoka Dar Es Salaam hadi Chalinze, taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi imefanyiwa uchambuzi ambapo Wizara imetoa idhini yenye masharti (*Conditional Approval*) ya kutekeleza kabla ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia; Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar es Salaam Awamu ya kwanza, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu, mkusanyaji mapato na mwendesha mfuko zilitangazwa na wazabuni wamepatikana; na Wizara

imekamilisha uchambuzi wa andiko la awali la mradi wa Mradi wa Mwambani Port lililowasilishwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, hatua inayoendelea ni maandalizi ya Upembuzi Yakunifu.

44. Mheshimiwa Spika, shughuli zingine zilizotekelezwa katika kusimamia utekelezaji wa PPP ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 44 hadi ukurasa wa 46.**

2.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

45. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu inaratibu na kusimamia mashirika na taasisi za umma 36 zilizo chini yake. Utekelezaji wa majukumu ya taasisi na mashirika haya kwa mwaka 2017/18 ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 47 hadi ukurasa wa 78.** Aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara kwa mwaka 2017/18 ni kama unavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 79 - 81.**

2.3 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

2.3.1 CHANGAMOTO

46. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

- i. Ukwepaji wa kodi;
- ii. Kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya masharti nafuu pamoja na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- iii. Uelewa mdogo wa wananchi juu ya dhana ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi ambayo ni pana na inabadilika kwa kasi;
- iv. Baadhi ya wawekezaji kutelekeza mali walizouziwa na Serikali wakati wa zoezi la Ubinafsisishaji; na
- v. Uelewa mdogo wa dhana ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

2.3.2 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

47. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo:

i. Kutekeleza mkakati wa ulipaji kodi kwa hiari na kuendelea kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kujenga mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato;

ii. Kuendelea kuelimisha wadau mbalimbali kupitia makongamano, mikutano na warsha kuhusu dhana ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

iii. Kuendeleza mazungumzo na Washirika wa Maendeleo kuhusu njia mpya za kutoa na kupokea misaada na mikopo (*New Financing Instruments*);

iv. Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeongeza nguvu katika kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wawekezaji wote ili kuhakikisha wanaendesha viwanda na mali walizouziwa kwa kuzingatia Masharti ya Mikataba ya Mauzo; na

v. Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi.

3.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19

48. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016 /17- 2020/21), Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (2015 – 2020), Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja

na masuala mtambuka kama vile Jinsia, watu wenye ulemavu, Mazingira, UKIMWI, makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi na masuala ya lishe kwa jamii pamoja na maelekezo na ahadi zilizotolewa Kitaifa.

3.1 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

3.1.1 Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Uchumi Jumla

49. Mheshimiwa Spika, shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

(vi) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.1 mwaka 2017;

(vii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja;

(viii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2017/18 na asilimia 15.6 mwaka 2016/17;

(ix) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 13.0 mwaka 2017/18 na asilimia 13.3 mwaka 2016/17; na

(x) Nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 2.1 mwaka 2017/18 na asilimia 1.5 mwaka 2016/17.

3.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

50. Mheshimiwa Spika, kutokana na kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, imebidi kuupitia muundo wa Wizara ili uweze kuyaingiza mabadiliko haya ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu pamoja na maslahi ya watumishi kwa ujumla.

Muundo wa Wizara uko katika hatua za mwisho za kuidhinishwa na Mamlaka husika, ambapo imependekezwa iundwe Divisheni ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa itakayoongozwa na Kamishna na kuwa na kifungu chake.

51. *Mheshimiwa Spika*, hivyo katika mwaka 2018/19, shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa katika uratibu wa mipango ya maendeleo ya Taifa ni pamoja na: Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20; Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19; Kufanya tathmini ya muda wa kati katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Kukamilisha uundwaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa usimamizi wa miradi ya kitaifa ya Maendeleo; na Kufuatilia matumizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management - Operational Manual - PIM – OM).

3.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

52. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa juhudi za kupunguza umaskini ikiwemo kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Jitihada za Kuondoa Umaskini nchini (Poverty Monitoring System - PMS); kufuatilia utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika Mipango ya kitaifa na kisekta na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 na programu zinazolenga kuondoa umaskini katika maeneo ya vijijini na mijini; kufanya uchambuzi wa kina juu ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS-2017/18); kutoa mafunzo kwa Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu jitihada za kupambana na umaskini na kutunza mazingira ili kuweza kujumuisha katika mipango na bajeti zao.

53. *Mheshimiwa Spika*, Mipango mingine katika uratibu wa Mikakati wa Kupunguza Umaskini iko katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 87 hadi ukurasa wa 89**.

3.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

(a) Mapato ya Ndani

54. *Mheshimiwa Spika*, katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka 2018/19, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kusimamia sera za fedha na za kibajeti zinazolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kuimarisha Mkakati Shirikishi wa Mawasiliano na Walipa kodi na kuboresha utaratibu wa utozaji kodi; kujenga uwezo wa watumishi ili kukabiliana na tatizo la uhamishaji faida (Transfer Pricing) unaofanywa na kampuni zenye mitandao ya kimataifa kwa lengo la kukwepa au kupunguza kodi; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ulipaji kodi kupitia Mfumo wa Vitalu vya Walipakodi; kusimamia zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, taasisi na mashirika ya umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) ili kuboresha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali; na kuongeza kasi ya uthaminishaji wa majengo ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo.

55. *Mheshimiwa Spika*, mikakati mingine iliyopangwa iko katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 89 hadi ukurasa wa 90**.

(b) Misaada na Mikopo

56. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea na uratibu wa upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo mbalimbali nchini. Washirika wa Maendeleo wameahidi kuchangia Bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 2,676.64. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 545.76 ni kwa ajili ya Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS), shilingi bilioni 125.86 kwa ajili ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na shilingi bilioni 2,005.02 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

57. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha Mpango Kazi wa kutekeleza Mwongozo mpya wa ushirikiano (*Development Cooperation Framework- DCF*); na kukagua miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.

3.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

58. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo: kuendelea kuboresha Mfumo mpya wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali (CBMS) ili kurahisisha utoaji wa mgao wa fedha za matumizi kila mwezi na kuendesha mafunzo ya mfumo huo; kufanya marekebisho, kuchapisha na kusambaza nakala 2,200 Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2018/19 kama yalivyopitishwa na Bunge, kuchapisha na kusambaza: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20, Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali za kila Robo Mwaka, Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2019/20 na kuviwasilisha Bungeni na kuvisambaza kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa kwa Wadau wengine.

59. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ziko katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 92 hadi ukurasa wa 93**.

3.1.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Serikali

60. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa miongozo mbalimbali ya ukaguzi wa ndani iliyotolewa na Wizara na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa ndani katika maeneo ya ukaguzi wa miradi, ukaguzi wa kiufundi, usimamizi wa vihatarishi, mfumo wa usimamizi wa kazi za ukaguzi na mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

61. **Mheshimiwa Spika**, mipango mingine ambayo Wizara inatarajia kutekeleza katika usimamizi wa udhibiti wa fedha za umma iko katika hotuba yangu **ukurasa wa 94 hadi ukurasa wa 95**.

3.1.7 Usimamizi wa Malipo

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu (*Treasury Single Account*) kwa lengo la kuboresha mfumo wa matumizi ya Umma ili kuiongezea Serikali uwezo wa kugharamia shughuli zake kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea na usimamizi wa mfumo wa malipo ya kieletroniki (EFT na TISS) ili kuondoa ucheleweshaji wa malipo kwa wadau mbalimbali wakiwemo wastaafu, watoa huduma kwa Serikali pamoja na watumishi wa Umma. Vile vile, Wizara itaendelea na uunganishaji wa mfumo wa Malipo (Epicor) kwenye Balozi saba (7) ili kudhibiti matumizi nje ya bajeti.

3.1.8 Deni la Serikali

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Serikali itahakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu na kutokuwa mzigo kwa uchumi wetu na kuendelea kuwa fursa na kichocheo cha maendeleo kwa nchi yetu. Aidha, Serikali itaendelea kukopa kwa uangalifu kwa kuzingatia masharti nafuu. Mikopo hiyo itatumika kwenye miradi ya maendeleo yenye kuchochea ukuaji wa uchumi.

3.1.9 Mchango wa Mwajiri (Serikali) kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria ya mwajiri ya kila mwezi kwa ajili ya watumishi wa umma kwenye Mfuko Mpya wa Hifadhi ya Jamii utakaochukua nafasi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyounganishwa ya PSPF, GEPF, LAPF na PPF pamoja na mifuko ambayo haitaunganishwa ya NSSF, ZSSF, WCF na Bima ya Afya (NHIF).

65. Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii kuwasisitiza maafisa utumishi wote wanaohusika na kuingiza taarifa za watumishi wa umma kwenye mfumo wa kompyuta wa kutunza taarifa za watumishi wa umma waingize taarifa za watumishi kwa ukamilifu na usahihi ili uwasilishaji wa michango ya mwanachama na mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwe kamili na sahihi kwa kipindi chote cha utumishi na hatimaye kurahisisha malipo ya mafao, pensheni na mirathi wakati wa hitimisho la utumishi wa umma ili kuwaondolea usumbufu watumishi wa umma walioitumikia nchi yao kwa weledi na uaminifu.

3.1.10 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kusimamia na kuboresha uendeshaji na utumiaji wa mfumo wa taarifa za mishahara ya watumishi wa umma (Government Salaries Payment Platform - GSPP) kwa kuunganisha mfumo huo na taasisi za kibenki na mfumo wa pensheni kwa ajili ya urahisishaji wa huduma za mikopo na pensheni. Aidha, Wizara itaendelea kuunganisha taasisi 260 katika mfumo wa kukusanya mapato yasiyo ya kodi (Government Electronic Payment Gateway System - GePG), ili kuweza kufanikisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Vile vile, Wizara itaunganisha mifumo 10 ya kielektroniki ya taarifa za kifedha kwa lengo la kuiwezesha mifumo iweze kubadilishana taarifa.

3.1.11 Usimamizi wa Mali za Serikali

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kufanya kaguzi za mali za Serikali katika balozi kumi (10), kufanya kaguzi maalum na kutoa elimu ya utumiaji na utunzaji bora wa mali katika taasisi mbalimbali za Serikali ili kuepusha hasara zinazoweza kuzuilika.

3.1.12 Ununuzi wa Umma

68. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kukamilisha uandaaji

na kuzindua Sera ya Ununuzi wa Umma pamoja kuanza utekelezaji wa sera hiyo; kukusanya maoni ya wadau kuhusu changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma kwa lengo ya kuzifanyia marekebisho pale itakapohitajika; kuwajengea uwezo maafisa ununuzi na ugavi serikalini juu ya matumizi ya mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi na ugavi; kuendesha mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi kuhusu matumizi ya mfumo wa malipo wa EPICOR katika ununuzi; kuandaa mpango kazi wa usimamizi wa ununuzi wa umma katika Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma.

69. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ziko katika hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 98 hadi ukurasa wa 101**.

3.1.13 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

70. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma. Ili kufikia malengo hayo, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele nane (8) kama ifuatavyo: kufanya ukaguzi wa mafungu ya bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani; kufanya ukaguzi wa sekta ya gesi, mafuta na madini; kufanya maboresho ya mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA; na kukagua ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Aidha, Ofisi imelenga kufanya ukaguzi wa kiufanisi na kaguzi maalum katika maeneo yatakayoainishwa; kuwajengea wakaguzi uwezo wa kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi kwenye sekta ya gesi asilia na mafuta, sekta ya madini, Serikali mtandao na katika uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao (Financial crimes auditing). Vile vile, ofisi itaendelea

na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Ukaguzi katika Mikoa ya Rukwa na Mara.

3.1.14 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Msajili wa Hazina imepanga kutekeleza yafuatayo: kufanya mapitio na kufuatilia kampuni ambazo Serikali ina Hisa chache na hazijawasilisha gawio serikalini; kufanya uchambuzi wa uwekezaji unaofanywa na Mashirika ya Umma katika Kampuni Tanzu na kampuni nyinginezo; kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kufanya urejeshaji wa viwanda vinavyosuasua na kuwapatia wawekezaji mahiri; kusimamia kwa karibu ukusanyaji wa madeni ya ubinafsishaji wa iliyokuwa Benki ya NBC; kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mifuko ya Jamii, Taasisi za Fedha pamoja na wadau mbalimbali katika suala zima la uwekezaji na ufufuaji wa viwanda, kampuni na mashamba yaliyobinafsishwa.

72. Mheshimiwa Spika, Mipango mingine katika kusimamia Mashirika ya Umma iko katika hotuba yangu **ukurasa wa 102 hadi ukurasa wa 103.**

3.1.15 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

73. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuboresha, kutunza na kusimamia huduma za Pensheni kwa wastaafu wanaolipiwa Hazina ikiwa ni pamoja na kuendelea kulipa kwa wakati mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali, mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba. Aidha, wizara itaendelea kuboresha masijala ya pensheni kwa kuendelea kuhifadhi kumbukumbu za wastaafu kielektroniki, ili kurahisisha malipo kufanyika kwa wakati.

74. Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kwa maafisa utumishi wote wanaohusika kuandaa mapema nyaraka za watumishi wanaotarajia kustaafu na kuziwasilisha

Hazina zikiwa zimekamilika ili malipo ya mafao, pensheni na mirathi ya wastaafu wa kawaida yafanyike kwa wakati na kuwaondolea adha ya usumbufu watumishi pindi wanapokuwa wamestaafu. Aidha, nahimiza ofisi zote za umma zitunze taarifa za watumishi wa umma kielektroniki kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao.

3.1.16 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

75. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Kitengo cha Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2012 na Sheria ya Udhibiti Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar ya Mwaka 2009 kwa kutekeleza yafuatayo: kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu (*The Anti-Money Laundering Act, 2006*) na kanuni zake za mwaka 2012 ili kuendana na mahitaji; kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na taarifa za usafirishaji wa fedha kutoka na kuingia nchini kupitia mipakani; na kuendelea kuwasilisha taarifa za intelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria.

3.1.17 Tume ya Pamoja ya Fedha

76. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Tume ya Pamoja na Fedha imepanga kufanya uchambuzi wa Mapato na Matumizi yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano.

3.1.18 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

77. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Ubia ili kuimarisha usimamizi wa mifumo ya usimamiaji wa miradi ya ubia na kupunguza mlolongo wa uidhinishaji

wa miradi hiyo; kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP); kuandaa miongozo ya kitaalam ya kuainisha na kufanya uchambuzi wa miradi ya PPP; na kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa miradi ya ubia kwenye Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na taasisi binafsi.

78. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika inategemea kukamilisha maandiko ya ujenzi wa reli ya Mchuchuma/ Liganga – Mtwara na reli ya Tanga – Arusha – Musoma kwa kiwango cha *standard gauge*; ujenzi wa miundombinu ya reli katika jiji la Dar Es Salaam kwa ajili ya treni ya abiria na mradi wa kusambaza gesi asilia nchini. Aidha, Wizara itaendelea na hatua ya kutangaza mradi wa ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa madawa muhimu na vifaa tiba chini ya MSD ili kuwapata wawekezaji.

3.1.19 Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma itaendelea kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma katika maeneo mbalimbali, hususan: marekebisho ya sheria za kodi ili sheria hizi ziendane na Sheria ya Uwekezaji; kuhuisha mikataba ya madini ambayo inapata misamaha ya kodi na mfumo wa kufanya maoteo ya viashiria vya uchumi jumla.

80. Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya maboresho ni pamoja na: kuandaa na kukamilisha Sera ya Kitaifa ya Ufuatiliaji na Tathmini; kuhuisha mikataba ya makubaliano na Washirika wa Maendeleo ili iendane na Sheria za Kodi za Tanzania; kufanya tathmini ya matokeo ya kiutendaji ya mfumo wa vihatarishi katika Wizara, Taasisi, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani; kuanzisha Ofisi mpya za Mhakiki Mali

wa Serikali katika mikoa ya Simiyu, Katavi na Songwe; kufanya marekebisho ya sheria ya Udalali ya mwaka 1928; na kuimarisha ununuzi wa Umma.

3.1.20 Mradi wa Kimkakati wa kuongeza mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (Strategic Revenue Generation in LGAs Project)

81. *Mheshimiwa Spika*, kupitia Mradi huu, Wizara itatoa fedha katika Serikali za Mitaa zitakazokidhi vigezo vya miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa kitaifa juu ya Usimamiaji na Uandaji wa Miradi ya Kimkakati ya kuongeza mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

3.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

82. *Mheshimiwa Spika*, mipango na malengo ya bajeti kwa mwaka 2018/19 kwa upande wa mashirika na taasisi za umma zilizochini ya wizara ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia **ukurasa wa 109 hadi ukurasa wa 127**.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

4.1 MAKADIRIO YA MAPATO

83. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 597.81 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

4.2 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

84. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Fedha na Mipango imepanga kutumia kiasi cha jumla ya **shilingi**

12,058,714,013,500 (Bilioni 12,058.71) kwa mafungu yote nane. Kati ya fedha hizo, shilingi **10,763,501,474,000 (Bilioni 10,763.50)** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,295,212,539,500 (Bilioni 1,295.21)** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **shilingi 65,764,075,000 (Bilioni 65.76)** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 693,257,399,000 (Bilioni 693.26)** kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC) na shilingi **10,004,480,000,000 (Bilioni 10,004.48)** ni malipo ya deni la Serikali na michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, katika fedha za matumizi ya maendeleo, **shilingi 1,266,033,128,500 (Bilioni 1,266.03)** ni fedha za ndani na **shilingi 29,179,411,000 (Bilioni 29.18)** ni fedha za nje.

MAOMBI YA FEDHA

4.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

85. *Mheshimiwa Spika*, katika fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 57,022,927,000 (bilioni 57.02)**. Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 7,577,332,000 (bilioni 7.58)**

(ii) Matumizi mengineyo – **Shilingi 49,445,595,000 (bilioni 49.44)**

(b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 28,790,817,000 (bilioni 28.79)**. Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 19,642,535,000 (bilioni 19.64)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 9,148,282,000 (bilioni 9.15)**.

4.2.2 FUNGU 21 - HAZINA

86. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya Kawaida – **Shilingi 531,890,056,000 (bilioni 531.89)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara ya fungu hili - **Shilingi 21,467,017,000 (bilioni 21.47)**.

(ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 510,423,039,000.00 (bilioni 510.42)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 1,247,611,267,500 (bilioni 1,247.61)**. Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 1,236,190,593,500 (bilioni 1,236.19)**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 11,420,674,000 (bilioni 11.42)**

4.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA

87. *Mheshimiwa Spika*, katika fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – **Shilingi 10,013,706,140,000 (bilioni 10,013.71)**. Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 9,226,140,000 (bilioni 9.23)**

(ii) Matumizi Mengineyo (Malipo ya Madeni na Michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii) – **Shilingi 10,004,480,000,000 (bilioni 10,004.48)**

4.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI

88. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 46,725,409,000 (bilioni 46.72)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara – **Shilingi 7,908,675,000 (bilioni 7.91)**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi Shilingi 38,816,734,000 (bilioni 38.82)**

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 3,200,000,000.00 (bilioni 3.20)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 2,000,000,000.00 (bilioni 2.00)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,200,000,000.00 (bilioni 1.20)**.

4.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

89. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 54,592,065,000.00 (bilioni 54.59)**. Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 2,362,279,000.00 (bilioni 2.36)**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi Shilingi 52,229,786,000.00 (bilioni 52.23)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 1,650,000,000.00 (bilioni 1.65)**. Kati ya fedha hizo:

- (i) Fedha za Ndani – **Shilingi 1,000,000,000.00 (bilioni 1).**
- (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 650,000,000.00 (bilioni 0.65).**

4.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA

90. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 2,155,075,000 (bilioni 2.15).** Kati ya fedha hizo:-
 - (i) Mishahara - **Shilingi 574,933,000 (bilioni 0.57)**
 - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 1,580,142,000 (bilioni 1.58).**

4.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU

91. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 2,015,586,000 (bilioni 2.01).**
- (b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 248,363,000 (bilioni 0.25)** ambazo ni fedha za nje.

4.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

92. *Mheshimiwa Spika*, katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida – **Shilingi 55,394,216,000 (bilioni 55.39)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 16,647,699,000 (bilioni 16.65)**.

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 38,746,517,000 (bilioni 8.75)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 13,712,092,000 (bilioni 13.71)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani – **Shilingi 7,200,000,000 (bilioni 7.20)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 6,512,092,000 (bilioni 6.51)**.

5.0 SHUKRANI

93. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru sana Wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu.

94. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz).

95. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita msemaji wa Kamati ya Bajeti aje asome ripoti yake kwa nusu saa na akimaliza tu kusoma Mwenyekiti wa Bajeti ambaye hotuba yake itasomwa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa

Jitu Soni, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ajiandae.

Mheshimiwa Jitu, karibu sana.

MHE. JITU V. SONI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; ambayo inajumuisha Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 – Deni la Taifa; Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali; na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) (c) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kupitia na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Fungu 45). Kamati ilitekeleza jukumu hili na kufanya mashauriano na Serikali na mwisho kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu haya, Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Fedha na Mipango kati ya mwezi Machi na Aprili, 2018, Dodoma na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na

Mafungu yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Ujumla Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mafungu yote manane yaliidhinishiwa kutumia jumla ya Sh.11,676,591,286,252.00. Kati ya fedha hizo shilingi 10.26 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Mafungu yote na shilingi trilioni 1.41 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, mchanganuo wa fedha za matumizi ya kawaida ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 72.53 ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 727.5 ilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni 9.4 ni kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na huduma nyingine. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, shilingi trilioni 1.37 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 42.3 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 7.21, sawa na asilimia 62.2 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 7.1 sawa na asilimia 72 ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 69.5 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia tano tu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Mafungu yake nane kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati imefanya uchambuzi katika mafungu manane yaliyo chini ya Wizara hii na kuona kuwa baadhi ya Mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna Mafungu ambayo hayakupatiwa fedha za kutosha hivyo kuathiri utendaji wake wa kazi. Hata hivyo, hali sio nzuri kwa upande wa utolewaji wa fedha za maendeleo kwenye Mafungu yote manane (rejea jedwali namba moja).

Mheshimiwa Spika, ukirejea jedwali namba moja, utaona kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2018; kati ya Mafungu nane yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, ni Mafungu mawili tu yalikuwa yamepokea fedha zaidi ya asilimia 60 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge (matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo).

Mheshimiwa Spika, Mafungu yaliyopokea zaidi ya asilimia 60 ni; Fungu 22 – Deni la Taifa na Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali; na Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali yamepokea fedha chini ya asilimia 60 kwa kipindi husika. Kwa upande wa Fungu 7 – Msajili wa Hazina amepokea asilimia 17.25 na Fungu 21 – Hazina imepokea asilimia 21.2.

Mheshimiwa Spika, hali ya utolewaji wa fedha kwa Mafungu haya siyo ya kuridhisha hata kidogo ukilinganisha na utekelezaji wa majukumu ya msingi wa Mafungu haya. Katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hakuna hata Fungu moja ambalo limepokea bajeti ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kuwa mwenendo wa ugawaji wa fedha kwa baadhi ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango si wa kuridhisha. Hii ni dhahiri kuwa utekelezaji wa shughuli nyingi za Wizara hii umeathirika kwa kiasi kikubwa ukizingatia kuwa mgawanyo na wajibu wa Serikali (*Government Instrument*) kwa Wizara ya Fedha na Mipango ni kutafuta na kusimamia ukusanyaji wa mapato pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa Mafungu mbalimbali. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kwa Mafungu yake hautoi tija kwa Mafungu husika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 12.1 kwa Mafungu yote nane. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 10.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.29 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida yanajumuisha kiasi cha shilingi bilioni 313.6 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 495.3 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi trilioni 10.04 ni kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa na huduma nyingine. Aidha, kwa upande wa fedha za matumizi ya maendeleo, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 1.29 ambayo inaoneshwa katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini Wizara kwa Mwaka 2018/2019. Makadirio ya mapato na matumizi haya yanahusisha pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Fungu 45). Kamati ya Bajeti inaipongeza Wizara ya Fedha kwa kuongeza shilingi bilioni 6.23 kwenye Fungu 45 ili Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iweze kutimiza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti. Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maombi ya fedha ya Mafungu husika kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Wizara nyingine kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Tathmini ya ujumla ya mwenendo wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa

Bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha unaonesha kuwa siyo wa kuridhisha kwa baadhi ya Mafungu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Machi 2018, kati ya Mafungu nane yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, mafungu mawili tu yalikuwa yamepokea fedha zaidi ya asilimia 60 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa upande wa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mafungu yaliyopokea zaidi ya asilimia 60 ni; Fungu 22 – Deni la Taifa na Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kwa Mafungu yake hautoi tija kwa mafungu husika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejitahidi kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mafungu mbalimbali ya Serikali Kuu na mikoa kwa wastani wa asilimia 100. Hata hivyo, pamoja na mwenendo huu mzuri wa utolewaji wa fedha kwenye mafungu husika, bado utekelezaji wa majukumu ya mafungu haya unaathiriwa na bajeti isiyojitosheleza kutokana na ukomo wa bajeti uliowekwa na Serikali hapo awali wakati mafungu hayo yakiomba fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Aidha, kwa upande wa utoaji wa fedha za maendeleo kwa kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, hali si ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kati ya mafungu 47 ya Wizara mbalimbali yanayostahili kupata fedha za maendeleo ni mafungu 16 tu yamepata fedha zaidi ya asilimia 50. Hali hii pia tunaiona kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kwa baadhi ya mafungu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ukilinganisha na bajeti waliyoidhinishwa na Bunge. Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango iangalie namna bora ya kutekeleza majukumu yake na kutatua changamoto za utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Fungu 66 – Tume ya Mipango; itakumbukwa kuwa Tume ya Mipango (Fungu 66) ilianzishwa kwa Mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 1989

(iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002) ikiwa chini ya Ofisi ya Rais kwa lengo la kuwa Msimamizi Mkuu wa Mipango ya Serikali ikiwemo kubuni miradi ya maendeleo ya kimkakati pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo. Tume hii imeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa huru chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, kwa kuwa mfumo wa Serikali umebadilika ni vyema Serikali ikarudisha Tume ya Mipango pamoja na Fungu 66 chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kusimamia na kuendeleza shughuli zilizokuwa zinafanywa na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kulinda uhuru wa upangaji wa mipango na usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali ili kuondokana na hali iliyopo sasa ambapo Serikali imekuwa ikiegemea zaidi kwenye mapato na matumizi kuliko mipango ya nchi na hivyo kutokuwa na uwajibikaji mzuri katika masuala ya kibajeti (*checks and balances*).

Mheshimiwa Spika, Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi na Wakandarasi na Wazabuni. Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Serikali ilichukua hatua madhubuti ya kuhakiki na kulipa madeni mbalimbali, hatua ambayo inapongezwa sana na Kamati ya Bajeti. Hadi Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali imehakiki na kulipa jumla ya shilingi bilioni 939.5 kwa mchangano ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 618.9; wazabuni shilingi bilioni 81.2; watumishi bilioni 133.4; watoa huduma mbalimbali shilingi bilioni 77.2 na madeni mengineyo shilingi bilioni 27.5. Pamoja na ulipaji huo wa madeni ya watumishi bado kuna malalamiko ya baadhi ya watumishi kama Walimu, kwamba fedha walizolipwa ni pungufu ya madai halisi wanayoidai Serikali. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inakamilisha ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma mwaka 2009 mara baada ya kukamilika kwa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Katika utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 21, imeainishwa miradi mbalimbali iliyo katika hatua ya kufanyiwa upembuzi yakinifu ili itekelezwe kwa njia ya *PPP*. Miradi hiyo ni *Dar Rapid Transport Phase I*, Mradi wa Uzalishaji wa Madawa na Vifaa Tiba Muhimu, Ujenzi wa Reli ya Mchuchuma/ Liganga – Mtwara, Mradi wa Bandari na Kituo cha Biashara cha Kurasini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi muhimu, Kamati imebaini kuwa maombi mengi ya miradi inasuasua kutekelezwa kwa njia ya *PPP* kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, moja; Serikali kuchelewa kuwalipa wakandarasi wanaofanya upembuzi yakinifu kwa miradi hiyo (*feasibility study*) mfano Reli ya Mchuchuma/ Liganga hadi Mtwara; Dar es Salaam – Tanga – Moshi; na Moshi – Arusha – Musoma. Pili, kuchelewa kufanya maamuzi kwa miradi inayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia mfano Mradi wa Kituo cha Biashara cha Kurasini ambacho mwekezaji hivi sasa ameamua kuwekeza nchi ya jirani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha Kitengo cha *PPP* kilichopo Wizarani kinatekeleza jukumu lake kwa ufanisi la kuratibu na kusimamia maandiko na maombi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (*Contracting Authorities*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya *PPP Facilitation Fund*. Mfuko huu una jukumu la kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa maandiko kwa ajili ya kubainisha miradi mbalimbali inayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia na kuhifadhi fedha kwa ajili ya ushiriki wa Serikali kwenye miradi ya ubia.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji yaaani (Fungu 21). Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Fedha na Mipango ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 60, kwa ajili ya kufanya utafiti wa majaribio yaani (*pilot study*) kwa baadhi ya mitaa, vijiji, kata na shehia kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa *village empowerment* maarufu kama milioni 50, kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulilenga “Kutenga Kiasi cha Shilingi bilioni 50, kwa ajili ya Kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa yaani (*SACCOS*) katika vijiji husika”. Hata hivyo, fedha hizo zilizotengwa katika miaka yote na hakuna fedha yoyote iliyotolewa licha ya Serikali kuahidi kuweka utaratibu maalum wa utekelezaji wa miradi hiyo kupitia TAMISEMI. Kamati ingependa Bunge lako Tukufu lipewe taarifa ya utekelezaji wa mradi huo ikiwemo hiyo ya ‘*pilot study*’ iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Mchezo wa Kubahatisha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Bajeti ilishauri Serikali kufanyia mabadiliko katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41. Lengo la mabadiliko ilikuwa ni kuipa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) uwezo wa kukusanya mapato yatokanayo na michezo hii na pia kufanya marekebicho ya viwango vya tozo. Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni kutokana na ushauri huo wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa kuweza kukusanya shilingi bilioni 39.1ni sawa na ongezeko la asilimia 12 hadi kufikia mwezi Machi, 2018. Pamoja na kuwa michezo hii imekuwa kwa kasi sana na kuipatia Serikali mapato, Kamati inashauri Serikali kupandisha ada, tozo na kodi mbalimbali katika michezo hii kwa sababu kimsingi michezo hii sio ya kiuzalishaji na imekuwa na madhara makubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika Nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo inaongoza kwa kiwango cha chini cha

mapato ghafi katika michezo hii kuliko nchi nyingine. Mfano Kenya wanatoza asilimia 35, Rwanda wanatoza asilimia 13 na Uganda wanatoza asilimia 20 ya mapato ghafi. Aidha, Kamati inaitaka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kusimamia kikamilifu Sheria hii kuhakikisha kwamba wanaoshiriki katika michezo hii ni wale wanaofikisha umri wa miaka 18 kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa Kodi wa Majengo; mwaka 2015/2016, Serikali ilichukua jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo na mabango kutoka katika Serikali za Mitaa na kuipeleka Serikali kuu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na baadaye kuzirejesha mapato hayo katika halmashauri husika. Mwaka huo huo Serikali ilishusha makadirio ya makusanyo ya kodi kutoka shilingi bilioni 58.08 zilizokuwa zimekadiliwa na Serikali za Mitaa na kuwa Shilingi bilioni 47.6.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilifanya mabadiliko kupitia Sheria ya Fedha na kuondoa takwa la kurejesha fedha za makusanyo ya mabango na majengo kwa Serikali za Mitaa na badala yake kurejesha kulingana na mahitaji ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali imeweza kukusanya kodi ya majengo kwa ufanisi wa asilimia 61.08 ambapo kiasi ya fedha Shilingi 20.22 zilikuwa zimekusanywa. Baada ya Kamati kufanya tathmini ya mwenendo huu, nina masuala yafuatayo kiushauri kwa Serikali:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kurudisha chanzo hiki cha mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa sababu bado Mamlaka ya Mapato hawajawa na uwezo wa kutosha kukusanya chanzo hiki; na Pili, ni utaratibu wa kutumia Dhamana ya Serikali za Mitaa yaani (*Municipal Bonds*) katika kupata fedha za Maendeleo kwa Serikali za Mitaa utashindikana kwa sababu halmashauri hazitakuwa na uwezo wa kulipa riba pindi amana hizo zinapoiva; na

Tatu, Kamati inaishauri Serikali kutumia Wanafunzi wa Chuo cha Ardhi kufanya shughuli ya kufanya tathimini ya majengo wakati wa mafunzo ya vitendo ili kuongeza tija ya ukusanyaji wa mapato husika.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji na utoaji wa fedha kwa ajili ya Mifuko mbalimbali yenye vyanzo Mahususi. Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mbalimbali zilizokuwa na lengo la kubainisha vyanzo vya mapato mahususi kwa ajili ya Mifuko mbalimbali. Mfano asilimia 1.5 yaani kwa *bill of lading* wakati wa kuingiza bidhaa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Reli, na tozo ya Sh.100 ya mafuta kati ya tozo hiyo Sh.50 ni kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini (REA) na Sh.50 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Maji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 17(a) cha Sheria ya Uendelezaji wa Tasnia ya Korosho inatoa mgawanyo wa makusanyo ya ushuru wa usafirishaji wa korosho ghafi nje ugawanywe kwa asilimia 35 ziende Serikali kuu na asilimia 65 ziende kuendeleza zao la korosho nchini. Kamati imebaini kwamba pamoja na Sheria mbalimbali kuainisha matumizi ya fedha hizo kwenye maeneo ya kimkakati utoaji wa fedha hizo umekuwa ukichelewa na mara nyingi hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, mfano, Mfuko wa REA kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali iliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 263.7 ambapo kiasi kilichokuwa kimetolewa REA ni bilioni 261.3. Mfuko wa Uendelezaji wa zao la Korosho ulikuwa umepokea shilingi bilioni 10 tu kati ya shilingi bilioni 91, zilizokuwa zimekusanywa katika msimu wa mwaka 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia sheria mbalimbali za fedha, hususan zilizoanzisha Mifuko mbalimbali pamoja na Sheria ya Bajeti ili mapato husika yaende yakatumike kwenye shughuli zilizokusudiwa, kwa kuzingatia kuwa Mifuko hiyo ipo kisheria na Bunge lilishaidhinisha matumizi ya fedha husika kwenye Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukifuatilia Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali wa mwaka wa fedha 2016/2017, utaona kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya kiasi cha Shilingi trilioni 1.67 kama tozo ya ushuru uliokusanywa kwa niaba ya Taasisi zingine. Makusanyo hayo yanahusu tozo za barabara, tozo ya petroli, ada ya maendeleo ya maji, tozo ya maendeleo ya reli na tozo ya bandari. Hata hivyo, ilibainika kuwa, kati ya makusanyo yote hayo, kiasi cha shilingi bilioni 410, hazikuweza kuwasilishwa kwenye Taasisi husika kinyume na matakwa ya sheria. Kamati inaishauri Serikali kwamba pindi fedha zinapokusanywa na Mamlaka ya Mapato na kupelekwa katika Akaunti ya Mapato iliyoko Benki Kuu, fedha hizo zikitoka ziende moja kwa moja kwenye Mifuko husika na badala ya kusubiria tena kibali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kama inavyofanya sasa.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi katika kikosi cha kodi (*Task Force*). Kamati ya Bajeti ilikuwa na vikao mbalimbali na Sekta Binafsi ambapo kupitia vikao hivyo masuala mbalimbali yanayohusu changamoto ya kikodi zinazowakabili zilijadiliwa. Pamoja na mambo mengine Sekta Binafsi imekuwa ikilalamikia utendaji kazi wa Kikosi Kazi cha Kodi hasa kwa upande wa idadi ya wajumbe wa Sekta Binafsi wanaoruhusiwa katika kikosi hicho; Pili, ufinyu wa muda wanaopewa kujadili masuala ya kodi; na Tatu, mapendekezo mengi kutofanyiwa kazi na Serikali bila ya kutoa sababu maalum au mrejesho kwa wadau.

Mheshimwa Spika, ieleweke kwamba uwepo wa Sekta Binafsi ulikuwa ndio msingi madhubuti wa Serikali kukusanya mapato ili iweze kuhudumia wananchi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya muundo wa Kikosi Kazi hicho ili kuondoa upungufu uliojitokeza pamoja na kuangalia upya sera ya utozaji kodi katika mawanda mapana ya kiuchumi na ya kijamii na sio katika ukusanyaji wa mapato tu.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa Mapato ya Serikali. Katika muda tofauti tofauti Kamati imekuwa ikishauri Serikali

kuhakikisha kwamba inaendeleza Sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali lakini hali imekuwa siyo hivyo. Mfano Sekta ya mawasiliano kwa mujibu wa Taarifa ya TCRA inaonesha watu zaidi ya milioni 2.5 wameondoka katika mfumo wa usafirishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa fedha na bidhaa zinazotowza ushuru wa bidhaa kama pombe kali (*spirits*) zimeshuka kwa asilimia 30. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba sera zake za kikodi kwa sekta zinazokua ziwe zina lengo la kulea na kuendeleza sekta hizo na sio kukusanya kodi kiasi ambacho kinaathiri hata ukuaji wa sekta husika.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utawala wa Kodi (*Institute of Tax Administration*) kimechaguliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa kituo cha Umahili cha Masuala ya Masomo ya Kodi na Forodha (*Centre of Excellency*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuratibu na kuisimamia vyema shughuli za Chuo cha Utawala wa Kodi kupitia Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Hata hivyo, kwa sasa eneo la chuo hicho ni finyu na miundombinu yake haijawa ya kisasa ili kukiwezesha kukidhi ubora wa kimataifa katika masuala ya kodi na ushuru wa forodha. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti kwa chuo hiki ili kiweze kutanua na kujenga *Campus* mpya katika eneo la Chuo la Misugusugu pamoja na kununua vifaa vya kuboresha miundombinu ya chuo ili kukidhi vigezo vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kuchambua na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ambao wameorodheshwa hapo chini kwa kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt, Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa; Mheshimiwa Dkt, Ashatu K. Kijaji, Naibu Waziri

wa Fedha na Mipango; Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri kutoka kwa Wajumbe wa Kamati wakati wote wa mijadala ya makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wa Sekta Binafsi kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee tunaomba kukushukuru wewe binafsi, pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika; Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge; pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee tunapenda kuwashukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi, Ndugu Lina Kitosi; Kaimu Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Michael Kadebe; na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu nane (8), yaliyo chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kuwasilisha na taarifa yote hii basi iingie katika Hansard.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti Mheshimiwa Jitu Soni, tunakushukuru sana kwa kusoma vizuri sana maoni ya Kamati yenu.

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19. KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/18 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo inajumuisha Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kupitia na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Fungu 45). Kamati ilitekeleza jukumu hili na kufanya mashauriano na Serikali na mwisho kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu haya, Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Fedha na Mipango kati ya mwezi Machi na Aprili, 2018 Dodoma na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

2.0 MAPITIO YA UJUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2017/18, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote manane (8) yalidhinishwa kutumia jumla ya **Shilingi 11,676,591,286,252.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10.261,308,284,511.00** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mafungu yote na **Shilingi 1,417,433,000,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, mchanganuo wa fedha za matumizi ya kawaida ni kama ifuatavyo **Shilingi 72,533,604,000.00** ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 727,341,680,511.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 9,461,433,000,000** kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na Huduma nyingine. Kwa upande wa fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, **Shilingi 1,374,975,800,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 42,307,201,741.00** ni fedha za nje

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Februari Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 7,212,352,493,767.63** sawa na **asilimia 62.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,106,866,350,742.37** sawa na **asilimia 72** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 69,587,632,847** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 5** tu ya Bajeti.

2.2. Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

Mheshimiwa Spika, hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya mafungu yake manane kwa mwaka wa fedha 2017/18. Kamati imefanya uchambuzi katika mafungu manane yaliyo chini ya Wizara hii na kuona kuwa baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Vilevile, kuna mafungu ambayo hayakupatiwa fedha za kutosha hivyo kuathiri utendaji kazi wake. Hata hivyo, hali sio nzuri kwa upande wa utolewaji wa fedha za maendeleo kwenye mafungu yote Nane (rejea jedwali namba moja)

Mheshimiwa Spika, ukirejea **Jedwali namba 1**, utaona kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2018; kati ya Mafungu manane (8) yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, ni mafungu mawili tu yalikuwa yamepokea fedha zaidi ya asilimia 60 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge (Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo). Mafungu yaliyopokea zaidi ya asilimia 60 ni; Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 10 Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali yamepokea fedha chini ya asilimia 60 kwa kipindi husika. Kwa upande wa Fungu 7 - Msajili wa Hazina (17.25) na Fungu 21 – Hazina (21.26) hali ya utolewaji wa fedha kwa mafungu haya sio ya kuridhisha hata kidogo ukilinganisha na utekelezaji wa majukumu ya msingi wa mafungu haya. Katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo hakuna hata fungu moja ambalo limepokea Bajeti ya Maendeleo kwa zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kuwa mwenendo wa ugawaji wa fedha kwa baadhi ya mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango sio wa kuridhisha. Hii ni dhahiri kuwa utekelezaji wa shughuli nyingi za Wizara hii umeathirika kwa kiasi kikubwa ukizingatia kuwa mgawanyo na wajibu wa Serikali (*Government Instrument*) kwa Wizara ya Fedha na Mipango ni kutafuta na kusimamia ukusanyaji wa mapato pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kwa mafungu yake hautoi tija kwa mafungu husika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Mathalani, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la Kusimamia Mashirika ya Umma na imepokea asilimia 17.25 tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ni vizuri Bunge lijiulize kwa Bajeti hii, je Ofisi hii itawezaje kutimiza majukumu yake ya msingi? Kamati ya Bajeti inajuliza kuwa, kama Wizara ya Fedha na Mipango imeshindwa kuwezesha kuwa baadhi ya mafungu yake kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, itawezaje kuhakikisha mafungu ya Wizara nyingine kupata fedha za kutosha kutekeleza majukumu yao ya msingi? Kamati ya

Bajeti inaona kuwa bado kuna changamoto kubwa kwa Wizara hii kuweza kusimamia vizuri sera, sheria, kanuni na taratibu za fedha (Monetary Policy) na Sera ya Mapato na Matumizi (Fiscal Policy)

JEDWALI NAMBA 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/18

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI ILIYO DHIKISHWA 2017/18		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACH, 2018		ASILIMIA MATUMIZI YAKAWADA NA WAKWADELEO HADI MACH, 2018		ASILIMIA KIASI CHOTE KIUCHOTOLEWA (%)
		Matumizi ya kawaida	Mbendeleo	Matumizi ya kawaida	Mbendeleo	Matumizi ya kawaida	Mbendeleo	
50	Aina ya Matumizi Wizara ya Fedha na Mipango	55,089,643,000	11,570,500,000	41,171,372,242.56	3,799,510,000	74.80	32.84	53.63
21	Hazina	570,429,248,000	1,395,636,701,741	339,050,386,897.84	63,125,192,846.70	59.44	4.52	21.26
22	Deni la Taifa	9,519,322,300.00	-	6,821,053,221.47	-	71.69	-	67.88
13	Kitergo cha Ubhiti Fedha Haramu	1,515,586,000	-	869,078,757.39	-	57	-	57.00
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	1,386,817,511	-	800,399,408	-	57.71	-	65.00
07	Majili wa Hazina	104,917,488,000	2,000,000,000	17,695,190,675	750,000,000	16.87	37.5	17.25
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	45,960,888,000	3,600,000,000	36,323,843,086	1,171,000,000	79.08	32.53	57.43
45	Ofisi ya Taifa ya Uleguzi wa Hesabu ya Serikali	49,832,948,000	11,800,948,000	31,923,227,835	778,195,000	64.06	6.59	57.39

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2017/18		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI , 2018		ASILIMVIA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO HADI MACHI, 2018		ASILIMVIA KIASI CHOTE KILICHOTOLE WA (%)
		Matumizi ya kawaida	Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Maendeleo	
50	Aina ya Matumizi Wizara ya Fedha na Mipango	55,039,643,000	11,570,500,000	41,171,372,242.5 6	3,799,510,000	74.80	32.84	53.63
21	Hazina	570,429,248,000	1,395,636,701, 741	339,050,386,897. 84	63,125,192,84 6.70	59.44	4.52	21.26
22	Deni la Taifa	9,519,322,300,000	-	6,821,053,221,47 2.90	-	71.69	-	67.88
13	Kitengo cha Uchibiti Fedha Haramu	1,515,586,000	-	869,078,757.39	-	57	-	57.00
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	1,386,817,511	-	800,399,408	-	57.71	-	65.00
07	Msajili wa Hazina	104,917,488,000	2,000,000,000	17,695,190,675	750,000,000	16.87	37.5	17.25
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	45,960,838,000	3,600,000,000	36,323,843,086	1,171,000,000	79.03	32.53	57.43
45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali	49,832,948,000	11,800,948,000	31,923,227,835	778,195,000	64.06	6.59	57.39

2.2.1. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, Fungu hili lina jukumu kubwa la kuratibu na kusimamia shughuli za utawala (Wizara pamoja na taasisi zake), ununuzi wa umma, mali za Serikali, ukaguzi wa ndani serikalini pamoja na kuratibu na kusimamia huduma za kisheria. Kwa mantiki hii, fungu hili ndio kitovu cha Wizara ya fedha na Mipango. Hadi kufikia mwezi Machi 2018 fungu hili pamoja na umuhimu wake lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi 44,970,882,242.56** sawa na asilimia 67 ya Bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 41,171,372,242.56** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 3,799,510,000** ni fedha za maendeleo. . Kamati inaona kuwa kutolewa kwa fedha kidogo au kuchelewa kutolewa fedha kwa wakati kwa fungu hili kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi kwa Wizara ya Fedha na Mipango na hivyo kuathiri shughuli za kiutawala ndani ya Wizara pamoja na upelekaji wa fedha kwa mafungu ya Wizara nyingine. Kamati inaishauri kuwa, Wizara itekeleze vema mipango yake ili kufikia malengo iliyojiwekea ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mafungu mengine ya Wizara yanapata fedha za bajeti zao kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

2.2.2. Fungu 21- Hazina

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la hazina ni kuandaa na kusimamia sera ya fedha (monetary policy), sera ya mapato na matumizi (fiscal policy), kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na kusimamia na kudhibiti Deni la Taifa. Katika mwaka wa Fedha 2017/18 halikuweza kupokea fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, kwani takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2018 kati ya kiasi cha **Shilingi 1,395,636,701,741** kilichoidhinishwa na Bunge, fungu hili lilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 63,125,192,846.70 tu** (sawa na asilimia 4.51). Baadhi ya miradi haijatekelezwa kutokokana na kukosekana kwa fedha za maendeleo. **Jedwali Namba 2 linaonyesha mchanganuo hapo chini:-**

Jedwali Na 2: Utolewaji wa fedha za Maendeleo kwa Miradi ya Fungu 21

Na	Mradi	Bajeti		Fedha zilizotolewa	
		Ndani	Nje	Ndani	Nje
1.	Village empowerment Fund	60,000,000,000	-	0	-
2.	Regional Support on Budget Process	100,000,000	135,354,000	0	0
3.	Public Management Reform Programme (PFMRP)	1,200,000,000	1,000,000,000	0	328,080,000
4.	Global Fund Management Project	0	2,293,002,878	0	0
5.	Program Support to NAO		1,195,020,526	0	0
6.	PPP facilitation Fund	5,000,000,000	0	0	0
7.	Poverty Monitoring Master Plan (PMMP)	200,000,000	0	0	0

Chanzo Wizara ya Fedha na Mipango fungu 21

Mheshimiwa Spika, Kati ya miradi saba iliyoainishwa hapo juu ni mradi mmoja tu wa PFMRP ndiyo umepokea fedha wakati miradi iliyobaki sita (6) haijapokea fedha hata kidogo. Kamati ya Bajeti inashauri ihakikishe inapeleka fedha kwenye miradi husika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Hazina ndio inaratibu na kusimamia mifumo mbalimbali ya kibajeti. Hata hivyo, imekuwa na tabia ya kuanzisha na kusitisha mifumo mingi ya ukusanyaji, usimamizi, na ufuatiliaji wa masuala ya Bajeti ambayo imekuwa ikiigharimu Serikali fedha nyingi katika kuiandaa, kuifundisha na kuitumia. Kamati imebaini kuwa kuna mifumo mbalimbali ya ukusanyaji, usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya bajeti na programu mbalimbali ambayo haijahuishwa pamoja na hivyo kuongeza gharama na kero kwa wadau. Mfano, hapo awali tulikuwa na Mfumo wa **Strategic Budget Allocation System (SBASS)** na sasa tumehamia kwenye **Central Budgeting Management System (CBMS)**; Kulikuwa na Mfumo wa Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na Mabango wa Serikali za Mitaa uitwao **Local Government Revenue Collection System (LGRCS)** Baada ya ukusanyaji wa mapato kuhamia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), nao wakaanzisha mfumo mpya wa **Property Rate Management**

System (PRMS). Hivi sasa, Serikali inaandaa Mfumo mwingine wa ufuatiliaji wa umasikini **Poverty Monitoring System (PMS).** Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezakano wa kuhuisha mifumo iliyopo ili kupunguza gharama na kukidhi mahitaji ya wadau kwa muda mrefu badala ya kubadilisha mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2017/18 Bunge liliidhinisha kiasi cha **shilingi 60,000,000,000** kwa ajili ya kufanya majaribio ya programu ya uwezeshaji wananchi vijijini kupitia TAMISEMI. Hata hivyo, hadi mwezi Machi 2018 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa na Serikali. Aidha, Serikali iliahidi kuweka utaratibu maalum utakaotumika katika kuchagua vijiji hivyo ili kutekeleza programu hiyo. Kamati haijulishwa kuhusu utoaji wa fedha hizo kupelekwa kwenye maeneo husika. Hivyo inashauri Serikali kutekeleza program hii ikiwa pamoja na kutoa fedha hizo na kukamilisha utaratibu huo haraka utakaozingatia usawa kwa Mikoa yote, hali ya umasikini, aina ya shughuli na ushirikishwaji wa vyombo vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kupata taswira itayakowezesha program hii kutekelezwa kwa ufanisi.

2.2.3. Fungu 22 – Deni la Taifa

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini umuhimu wa kuwepo kwa kitengo cha Usimamizi wa Deni la Taifa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango kikiwa na jukumu la kuhakikisha kinatunza na kusimamia taarifa muhimu za madeni (Public Debt Database) pamoja na kusimamia kikamilifu ulipaji wa madeni ya ndani na nje (Domestic and External Debts). Takwimu zinaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari 2018, Serikali ilikuwa imelipa jumla ya madeni **Shilingi Trilioni 5.54** kati ya fedha hizo **Shilingi Trilioni 4.094** ni madeni ya ndani na **Shilingi Trilioni 1.446** ni madeni ya nje. Kulingana na Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (*Debt Sustainability Analysis*) unaonyesha Deni letu ni himilivu kwa **asilimia 34.4** ukilinganisha na ukomo wa asilimia 56. Hata hivyo ukilinganisha makusanyo ya Ndani yanayotokana na kodi na malipo ya Deni la Taifa utaona kuwa, mpaka mwezi Desemba

2017 makusanyo ya Ndani yalikuwa **Shilingi Trilioni 7.678** na Malipo ya Deni Mpaka Februari ya **Shilingi Trilioni 5.54** utaona kwamba kiasi kikubwa cha makusanyo ya fedha za ndani kinakwenda kulipa Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Napenda Bunge lako tukufu lifahamu kuwa deni la Serikali limeongezeka kwa asilimia 16.2 katika kipindi cha miezi 12 yaani kuanzia mwezi Machi 2017 hadi mwezi Machi 2018. Licha ya kuwepo kwa mikakati mbalimbali ya kudhibiti ongezeko la deni la Serikali, bado mikakati hiyo haijaweza kuwa na matokeo chanya. Miongoni mwa mikakati hiyo ni Mkakati wa Ushirikiano wa Maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza Mkakati wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework-DCF*) wenye lengo la kupanua wigo wa upatikanjaji wa mikopo na misaada yenye masharti nafuu na kuongeza mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja. Aidha, Serikali ifanye mazungumzo na wahisani mbalimbali wakiwemo wale wa *'Non Paris Club'* ili kuona namna ya kuweza kupunguziwa au kusamehewa Deni hilo na hivyo kutoa nafuu kwa mapato ya ndani kuweza kugharamia Bajeti ya Serikali.

2.2.4. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu

Mheshimiwa Spika, kitengo cha udhibiti wa fedha haramu (*Financial Intelligence Unit*) kimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu ya Mwaka 2006 (*The Anti-Money Laundering Act*). Kifungu cha Sita cha Sheria hiyo kinaelezea majukumu na kazi za Kitengo hicho ikiwa pamoja na kufuatilia ufadhili wa kigaidi. Pamoja na majukumu haya makubwa, kitengo hiki bado kinatengewa bajeti ndogo na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mathalani, Katika mwaka wa fedha 2017/18 kitengo kilitengewa **shilingi 63,000,000** tu kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa mbali mbali za miamala shuku (suspicious transations) inayohusu fedha haramu na ufadhili wa kigaidi.

Mheshimiwa Spika, kitengo hiki ni muhimu pia katika kudhibiti upotevu wa fedha kupitia njia haramu, kwani utafiti wa taarifa

ya *Illicit Financial Flow 2011* maarufu kama Ripoti ya Mbeki inaonyesha kwamba Nchi za Afrika kwa mwaka zinapoteza kiasi cha takribani **Dola za Marekani Billioni 50** kupitia njia haramu. Kamati inashauri fungu hili liongezewe bajeti yake ili litekeleze majukumu yake vizuri.

2.2.5. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

Mheshimiwa Spika, Tume ya pamoja ya Fedha imeanzishwa kwa mujibu Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majukumu ya Tume hiyo yameainishwa katika Ibara ya 134(2) ambayo ni pamoja na kutunza akaunti ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuchambua mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa masuala ya Muungano pamoja na kutekeleza majukumu mengine itakayopangiwa na Rais. Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi milioni 800.399** kati ya **shilingi bilioni 1.386** iliyoidhinishiwa (Sawa na asilimia 58 ya fedha yote). Kutokana na majukumu yake ya Msingi Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inatoa fedha iliyopangwa kwa tume hii ili iweze kukamilisha majukumu yake ya kimsingi kama yalivyoainishwa kwenye Katiba.

2.2.6. Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370; Ofisi hii ina jukumu la kusimamia na kulinda mitaji na uwekezaji wa Serikali katika mashirika na taasisi za umma. Pamoja na majukumu mengine Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwenye mashirika ya umma kwa niaba ya Serikali. Takwimu zinaonesha hadi kufikia Mwezi Februari, Ofisi hii imekusanya mapato yatokanayo na asilimia 15 ya mapato ghafi kiasi cha **Shilingi bilioni 498.2** kati ya **Shilingi bilioni 524.6** zilizopangwa kukusanywa katika mwaka wa Fedha 2017/18 (sawa na asilimia 94.9 ya lengo). Pamoja na Ufanisi huu mkubwa bado Wizara ya Fedha na Mipango imetoa kiasi kidogo tu cha fedha (asilimia 17.25 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge) kwa ofisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18, Fungu hili lilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 95.0** kwa ajili ya kusaidia Mashirika ya Umma yenye matatizo ya Kimtaji. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi februari mwaka huu, Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 12.998** zilikuwa zimepokelewa. Hii ni changamoto kubwa kwa Serikali katika kuyawezesha mashirika yake ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kamati inaikumbusha Serikali kuwa '***Ukitaka kukusanya mapato zaidi lazima uwekeze zaidi sio kutegemea mapato bila ya kuwekeza***'. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa kukusanya asilimia 15 ya Pato ghafi bila kuangalia gharama za uzalishaji kwa kuwa kwa kufanya hivyo kuna baadhi ya mashirika yameanza kujiendesha kwa hasara na hivyo kuwa mzigo kwa Serikali hasa kwa yale ambayo yanategemea ruzuku kutoka kwa Serikali.

2.2.7. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Idara hii kwa kuweza kusimamia na kuboresha mfumo wa malipo Serikalini ***Integrated Financial Management system (IFMS)***. Aidha, Kamati inasisitiza Idara hii kuhakikisha inaendelea kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Fungu hili limepokea kiasi cha asilimia 57.43 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge. Kama ilivyojitokeza kwenye mafungu mengine, maoteo ya mahitaji ya fedha kwa mafungu mbalimbali hayakuzingatia mahitaji halisi na majukumu ya kazi ya mafungu husika, hivyo ukomo uliowekwa umeathiri shughuli za utekelezaji wa mafungu husika.

Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi uliidhinishwa jumla ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 73.63** kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 44.51** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC), **Shilingi Bilioni 17.31** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi Bilioni 11,80** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **shilingi Bilioni 8.00** na **shilingi 3,800,948,000** ni fedha za nje.

Ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi 12,000,000,000** pamoja na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zikiwa kama ruzuku ya Serikali kiasi cha **shilingi 32,519,192,267**.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **shilingi Bilioni 37.36** kutoka Hazina. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 27,505,331,083.85** ni kwa ajili ya OC sawa na **asilimia 73.6** ya bajeti iliyotengwa (ruzuku ya Serikali), **shilingi 9,084,318,726** kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 52.5** ya makadirio na **shilingi 778,195,000** tu ambazo ni fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni **asilimia 20** ya makadirio ya fedha za nje na **asilimia 6.6** ya bajeti nzima ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2018, Wizara ya Fedha na Mipango ilikuwa haijaweza kutoa kiasi chochote cha fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fungu hili. Kufuatia changamoto hiyo, Ofisi hii imeshindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo iliyopangwa katika mwaka 2017/18; mathalani kushindwa kukamilisha ujenzi wa majengo mapya ya Ofisi katika mikoa iliyolengwa. Hapo awali Serikali ilikubali kutoa kiasi **shilingi 8,000,000,000** kila mwaka ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa majengo mawili. Hata hivyo, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa mpaka mwezi Machi 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli, hadi kufikia mwezi Februari 2018, Ofisi hii imeweza kukusanya maduhuli yenye jumla ya **shilingi 9,555,780,296** ikiwa ni sawa asilimia 80 ya makadirio ya mwaka. Kamati inaipongeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukusanyaji huo wa maduhuli na ikiwezekana kuongeza juhudi ili kuvuka lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Ofisi hii katika kukusanya maduhuli na kusimamia ukaguzi wa Wizara na taasisi za umma, bado mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo na Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sio wa kuridhisha na haukidhi utekelezaji wa

majukumu ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Suala hili linasababisha Ofisi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kulingana na viwango vya kimataifa vya kiukaguzi.

3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19.

3.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2018/19 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 12,106,390,621,500** kwa mafungu yote manane (8). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,813,501,149,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,295,212,539,500** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha kiasi cha **Shilingi 313,677,166,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 495,343,983,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 10,004,480,000,000** ni kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa na Huduma nyingine. Aidha kwa upande wa fedha za Matumizi ya Maendeleo, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 1,295,212,539,500**.

Jedwali Namba 2. Maombi ya Fedha Kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo Chini Wizara kwa Mwaka 2018/19.

Fungu	Matumizi Mengineyo (OC)	Mishahara	Miradi ya Maendeleo	Jumla
50	22,632,514,000	34,390,413,000	28,790,817,000	85,813,744,000
21	295,550,354,000	242,567,027,000	1,247,611,267,500	1,785,728,648,500
22	10,004,480,000,000	9,226,140,000	-	10,004,480,000,000
13	2,015,586,000	0	248,363,000	2,263,949,000
10	1,580,142,000	574,933,000	-	2,155,075,000
07	102,229,786,000	2,362,279,000	1,650,000,000	106,917,488,000
23	38,816,734,000	7,908,675,000	3,200,000,000	49,925,409,000
45	32,518,867,000	16,647,699,000	13,712,092,000	69,106,308,000
Jumla	10,499,823,983,000	313,677,166,000	1,295,212,539,500	12,106,390,621,500

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi haya yanahusisha pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Fungu 45) ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) kipengele (a) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ya Bunge ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2018/19. Ofisi kwa mwaka wa fedha 2018/19 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa mwaka wa fedha 2018/19 imeidhinishiwa fedha zake kama walivyoomba kwenye mapendekezo ya bajeti yao yenye jumla ya **shilingi 69,106,308,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 16,647,6999,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, **shilingi 32,512,867,000** ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, **shilingi 6,227,649,907** ni fedha kutoka ukaguzi wa Wakala/ Taasisi na Mashirika ya Umma na **shilingi 13,712,092,000**.

Mheshimiwa Spika, Hatua hii ilifikiwa baada ya mashauriano na Wizara ya Fedha na hivyo kuongeza kiasi cha **shilingi 6,232,325,000** kwenye Mfuko husika na kufikia kiasi hicho cha fedha. Kamati ya Bajeti inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua hii muhimu. Aidha, Kamati bado inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha Mfuko huu, unapatiwa rasilimali fedha za kutosha zinazoendana na mahitaji halisi ya Mfuko ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 pamoja na maombi ya Fedha ya mafungu husika kwa Mwaka wa Fedha 2018/19; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

4.1 **Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Mafungu yaliyochini ya Wizara ya Fedha na Wizara nyingine kama yalivyoidhinishwa na Bunge.**

Mheshimiwa Spika, tathmini ya ujumla ya mwenendo wa utowaji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/18 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha unaonesha kuwa sio wa kuridhisha kwa baadhi ya mafungu. Hadi kufikia Mwezi Machi 2018, kati ya Mafungu manane (8) yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, mafungu mawili tu yalikuwa yamepokea fedha zaidi ya asilimia 60 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa upande wa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mafungu yaliyopokea zaidi ya asilimia 60 ni; Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 10 Tume ya Pamoja ya Fedha. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kwa mafungu yake hautoi tija kwa mafungu husika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejitahidi kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa mafungu mbalimbali ya Serikali Kuu na Mikoa kwa wastani wa asilimia 100. Hata hivyo, pamoja na mwenendo huu mzuri wa utolewaji wa fedha kwenye mafungu husika, bado utekelezaji wa majukumu ya mafungu haya unaathiriwa na bajeti isiyojitosheleza kutokana na ukomo wa bajeti uliowekwa na Serikali hapo awali wakati mafungu hayo yakiomba fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Aidha, kwa upande wa utoaji wa fedha za maendeleo kwa kipindi cha Mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, hali sio ya kuridhisha. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya mafungu 47 ya Wizara mbalimbali yanayostahili kupata fedha za maendeleo ni mafungu 16 tu yamepata fedha zaidi ya asilimia 50. Hali hii pia tunaiona kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa baadhi ya mafungu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ukilinganisha na Bajeti waliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inataka Wizara ya Fedha na Mipango iangalie namna bora ya kutekeleza majukumu yake na kutatua changamoto za utekelezaji wa Bajeti.

4.2 Fungu 66 – Tume ya Mipango

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Tume ya Mipango (Fungu 66) ilianzishwa kwa Mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 1989 (iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002); ikiwa chini ya Ofisi ya Rais kwa lengo la kuwa Msimamizi Mkuu wa Mipango ya Serikali ikiwemo kubuni miradi ya maendeleo ya kimkakati pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo. Tume hii imeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa huru chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali katika awamu ya tano kwa sasa Tume ya Mipango imeunganishwa na Wizara ya Fedha na Fungu 66 limefutwa na kujumuishwa chini ya Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango. Kamati inaona kufutwa kwa fungu hili ni kinyume na Sheria hasa ukizingatia kwamba, Tume hii ilikuwa ni ‘*think tank*’ ya Serikali na ilikuwa pamoja na majukumu mengine ni kuhakikisha kwamba Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inafikiwa. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kurudisha Fungu hili na ikiwezekana kuanzisha Chombo maalumu chini ya Ofisi ya Rais kitakachoshughulikia Mipango ya Taifa. Nchi nyingi Duniani zimefanikiwa kuwa na nguvu kubwa ya uchumi kwa kuwa na Tume za Mipango zenye nguvu kubwa ya ushawishi wa mipango na utekelezaji pamoja na kupewa kipaumbele kwenye maamuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, kwa kuwa mfumo wa Serikali umebadilika ni vema Serikali ikarudisha Tume ya Mipango pamoja na Fungu 66 chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, kwa lengo la kusimamia na kuendeleza shughuli zilizokuwa zinafanywa na Tume ya Mipango. Hatua hii, itasaidia kulinda uhuru wa upangaji wa mipango na usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali ili kuondokana na hali iliyopo sasa amabpo Serikali imekuwa ikiegemea zaidi kwenye mapato na matumizi kuliko mipango ya nchi na hivyo kutokuwa na uwajibikaji mzuri katika masuala ya kibajeti (checks and balance)

4.3 Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi na Wakandarasi na Wazabuni.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2015/16 Serikali ilitokua hatua madhubuti ya kuhakiki na kulipa madeni mbalimbali, hatua ambayo inapongezwa sana na Kamati ya Bajeti. Hadi mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imehakiki na kulipa jumla ya Shilingi Bilioni 939.5 kwa mchanganuo ufuayao; Wakandarasi (**Shilingi Milioni Bilioni 618.9**), Wazabuni (**Shilingi Bilioni 81.82**), Watumishi (**Bilioni 133.84**), Watoa Huduma (**Shilingi Bilioni 77.259**) na Madeni mengineyo (**Shilingi Bilioni 27.595**). Pamoja na ulipaji huo wa madeni ya Watumishi bado kuna malalamiko ya baadhi ya Watumishi kama Walimu kwamba fedha walizolipwa ni pungufu ya madai halisi wanayoidai Serikali. Kamati inaendelea kuishauri Serikali ni kuhakikisha inakamilisha ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba.

4.4 Ulipaji wa Kodi (*Paying Taxes*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya UNCTAD ya Mwaka 2017 inayohusu Mazingira ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara, Tanzania inashika nafasi ya 137 kati ya nchi 186 na ina mizania ya asilimia 54.04. Moja ya vigezo vianvyotufanya tusifanye vizuri ni suala la ulipaji wa Kodi ambalo tumeshika nafasi ya 154. Kamati imefanya utafiti na kuona kuwa ili tuwe na vigezo bora vya kufanya vizuri katika ulipaji wa kodi, mambo yafuatayo hayana budi kufanyika:- **Kwanza**; kuharakisha kutoa maamuzi ya Kodi kwa Mashauri ambayo yako kwenye Baraza la Rufaa la Kodi, mfano katika mashauri 320 yaliyosajiliwa katika Baraza la Rufaa (*TRAT-Tax Revenue Appeals Board*) ni kesi 99 tu zimetolewa maamuzi sawa na asilimia 31 ya kesi zote; **Pili**; kuihuisha sekta isiyo rasmi katika mfumo wa kodi ili iweze kulipa kodi stahili na **Tatu**; kupunguza utitiri wa kodi, tozo na ada usiokuwa na tija kwa wakulima na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya, ni muhimu Serikali ikazingatia kanuni mbalimbali za kikodi kama vile *“Best Judgement Rule”* ambayo inamtaka mtu anayefanya

marekebisho ya makadirio ya Kodi (*Adjutment of tax Assesment*) aangalie mambo makuu yafuatayo:- **Kwanza**, aina ya biashara zinazoshabihiana; **Pili**, taarifa alizowasilisha anayefanyiwa marekebisho na:- **Tatu**, ni mazingira ya soko katika ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, maofisa wengi wa Kodi wanaofanya tathmini kwa wafanyabiashara (*tax assessment*) wamekuwa hawafuati kanuni hizi na hivyo tathmini wanazofanya zimekuwa za viwango vya juu kuliko uwezo au faida ya biashara husika hali inayosababisha wafanyabiashara wengi kufunga biashara, kukwepa kulipa kodi, kurudi kwenye sekta isiyo rasmi au kuhamia nchi jirani na hivyo kupelekea ukusanyaji hafifu wa mapato ya Serikali.

4.5 Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria ya Ubia Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma mwaka 2009 mara baada ya kukamilika kwa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Katika utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 21, imeanishwa miradi mbalimbali iliyo katika hatua ya kufanyiwa upembuzi yakinifu ili itekelezwe kwa njia ya PPP; Miradi hiyo:- *Dar Rapid Transport Phase I*, Mradi wa uzalishaji wa Madawa na Vifaa Tiba Muhimu, Ujenzi wa Reli ya Mchuchuma/ Liganga -Mtwara, Mradi wa Bandari na Kituo cha Biashara cha Kurasini. Pamoja na hatua hizi muhimu, Kamati imebaini kuwa maombi mengi ya miradi inasuasua kutekelezwa kwa njia ya PPP kwa sababu zifuatazo:-

Moja; Serikali kuchelewa kuwalipa wakandarasi wanaofanya Upembuzi yakinifu wa miradi hiyo (*feasibility study*) mfano Reli ya Mchuchuma/ Liganga hadi Mtwara, Dar es Salaam-Tanga-Moshi na Moshi-Arusha-Musoma;

Pili, kuchelewa kufanya maamuzi kwa miradi inayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia mfano mradi wa Kituo cha Biashara cha Kurasini ambacho muwekezaji hivi sasa ameamua kuwekeza nchi ya jirani. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha Kitengo cha PPP kilichopo

Wizarani kinatekeleza jukumu lake kwa ufanisi la kuratibu na kusimamia maandiko na maombi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa njia ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (Contracting Authorities).

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya '*PPP Facilitation Fund*'. Mfuko huu una jukumu la kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa maandiko kwa ajili ya kubainisha miradi mbalimbali inayoweza kutekelezwa kwa njia ya ubia na kuhifadhi fedha kwa ajili ya ushiriki wa Serikali kwenye miradi ya ubia.

4.6 Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. (Fungu 21)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango ilitenga kiasi cha **Shilingi 60,000,000,000** na katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara imetenga tena **Shilingi Bilioni 60,000,000,000** kwa ajili ya kufanya utafiti wa majaribio (*pilot study*) kwa baadhi ya mitaa, vijiji, kata na shehia kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama **Shilingi 50,000,000** kwa kila Kijiji. Mradi huu ulilenga "*Kutenga Kiasi cha Shilingi 50,000,000 kwa Kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika*". Hata hivyo, fedha hizo zilizotengwa katika miaka yote hakuna fedha yoyote iliyotolewa licha ya Serikali kuahidi kuweka utaratibu maalumu wa utekelezaji wa mradi huo kupitia TAMISEMI. Kamati ingependa Bunge lako tukufu lipewe taarifa ya utekelezaji wa mradi huu ikiwemo '*pilot study* iliyofanyika.

4.7 Michezo ya Kubahatisha

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Bajeti ilishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura 41 Lengo la mabadiliko ilikuwa ni kuipa Mamlaka ya Mapato (TRA) uwezo wa kukusanya mapato yatokanayo na Michezo hii na pia kufanya marekebisho ya viwango vya tozo.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni kutokana na ushauri huo wa Kamati. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuweza kukusanya **Shilingi Bilioni 39.11** sawa na ongezeko la asilimia 12 hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Pamoja ya kuwa michezo hii imekuwa kwa kasi sana na kuipatia mapato Serikali, Kamati imeishauri Serikali kupandisha ada, tozo na kodi mbalimbali katika michezo hii kwasababu kimsingi michezo hii sio ya kiuzalishaji na imekuwa na madhara makubwa kwa jamii. Katika Nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ndio inayotoza kiwango cha chini kwenye mapato ghafi ya michezo hii kuliko nchi nyingine. Mfano Kenya wanatoza asilimia 35, Rwanda wanatoza 13 na Uganda wanatoza asilimia 20 ya mapato ghafi. Aidha, Kamati inaitaka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kusimamia kikamilifu Sheria ili kuhakikisha kwamba wanaoshiriki katika Michezo hii ni wale waliofikisha umri wa miaka 18 kama sheria inavyotaka.

4.8 Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2015/16 Serikali ilichukua jukumu la ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na mabango kutoka katika Serikali za Mitaa na kuipelekea Serikali kuu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na baadae kuyarejesha mapato hayo katika halmashauri husika. Mwaka huo huo Serikali ilishusha makadirio ya makusanyo ya kodi hiyo kutoka **shilingi 58,008,196,553** zilizokuwa zimekadiliwa na Serikali za Mitaa na kuwa **Shilingi 47,672,784,729** Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilifanya mabadiliko kupitia Sheria ya fedha na kuondoa takwa la kurejesha fedha za makusanyo ya mabango na majengo kwa Serikali za Mitaa na badala yake kurejesha kulingana na mahitaji ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imeweza kukusanya kodi ya majengo kwa ufanisi wa **asilimia 61.08** ambapo kiasii cha **Shilingi 20,229,39 0,000** kilikuwa kimekusanywa. Baada ya Kamati kufanya tathmini ya mwenendo huu ina masuala yafuatayo ya kuishauri Serikali; Kwanza kurudisha chanzo hiki katika mamlaka ya Serikali za mitaa kwa sababu bado Mamlaka ya Mapato hajawa na

uwezo wa kutosha kukusanya Chanzo hichi na Pili ni utaratibu wa kutumia Dhamana za Serikali za Mitaa (*Municipal Bonds*) katika kupata fedha za Maendeleo kwa Serikali za Mitaa utashindikana kwasababu Halmashauri hazitakuwa na uwezo wa kulipa riba pindi amana hizo zinapoiva na Tatu Kamati inaishauri Serikali kutumia Wanafunzi wa Chuo cha Ardhi kufanya shughuli ya kufanya tathmini ya majengo wakati wa mafunzo ya vitendo ili kuongeza tija ya ukusanyaji wa mapato husika.

4.9 Ukusanyaji na utoaji wa fedha kwa ajili ya mifuko mbalimbali yenye vyanzo Mahususi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mbalimbali zilizokuwa na lengo la kubainisha vyanzo vya mapato mahususi kwa ajili ya mifuko mbalimbali. Mfano asilimia 1.5 ya *Bill of lading* wakati wa uingizaji wa bidhaa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Reli, na tozo ya Shilingi 100 ya mafuta kati ya tozo hiyo shilingi 50 ni kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini (REA) na Shilingi 50 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Maji. Aidha, kifungu cha 17A cha Sheria ya Uendelezaji wa Tasnia ya Korosho inatoa mgawanyo wa makusanyo ya ushuru wa usafirishaji wa korosho ghafi nje ugawanywe kwa asilimia 35 ziende Serikali kuu na asilimia 65 ziende kuendeleza zao la korosho nchini. Kamati imebaini kwamba pamoja na Sheria mbalimbali kuainisha matumizi ya fedha hizo kwenye maeneo ya kimkakati utolewaji wa fedha hizo umekuwa ukichelewa na mara nyingine hazitolewi kabisa. Mfano, Mfuko wa REA katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 263,700,000,000** ambapo Kiasi kilichokuwa kimetolewa ni **Shilingi 261,300,000**. Mfuko wa Uendelezaji wa zao la Korosho ulikuwa umepokea **Shilingi 10,000,000,000** kati ya **Shilingi 91,150,303,392.92** zilizokuwa zimekusanywa katika msimu wa mwaka 2016/17. Kamati inaishauri Serikali kuzingatia sheria za mbalimbali fedha, hususan zilizoanzisha mifuko mbalimbali pamoja na Sheria ya Bajeti ili mapato husika yaende yakatumike kwenye shughuli zilizokusudiwa, kwa kuzingatia kuwa Mifuko hiyo ipo kisheria na Bunge lilisha idhinisha matumizi ya fedha husika kwenye mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukifuatilia Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ya mwaka wa fedha 2016/17, utaona kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya kiasi cha **Shilingi 1,671,096,919,536.3** kama tozo na ushuru uliokusanywa kwa niaba ya Taasisi nyingine. Makusanyo hayo yanahusu tozo za barabara, tozo ya petroli, ada ya maendeleo ya maji, tozo ya maendeleo ya reli na tozo ya bandari Hata hivyo, ilibainika kuwa, kati ya makusanyo yote hayo, kiasi cha **Shilingi 410,448,166,098.44** hakikuweza kuwasilishwa kwenye taasisi husika kinyume na matakwa ya sheria. Kamati inaishauri Serikali kwamba pindi fedha zinapokusanywa na Mamlaka ya Mapato na kupelekwa katika Akaunti ya Mapato iliyopo Benki Kuu, fedha hizo zikitoka ziende moja kwa moja kwenye mifuko husika na badala ya kusubiria tena kibali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kama inavyofanya sasa.

4.10 Utaratibu wa Serikali kufikisha mapendekezo na maoni ya Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi, Bunge lako limekuwa likipitisha mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki bila kuwa na nafasi ya kushirikishwa na kutoa mapendekezo yake kupitia Kamati zake za Kibunge. leleweke kwamba, pamoja na mapendekezo hayo kuletewa Bungeni kupitia sheria ya Fedha (*Finance Bill*), bado Bunge linakuwa halina mamlaka ya kubadili au kupendekeza mabadiliko hayo katika sheria hiyo kwa kuwa tayari Serikali za Nchi wanachama zinakuwa zimeisharidhia na kuamua kwa niaba ya nchi zao. Kamati ya Bajeti kwa nyakati tofauti imekuwa ikiomba fursa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha mapendekezo hayo mbele ya Kamati ili yajadiliwe kwa niaba ya Bunge kwa kuwa yanahusika katika kuongeza au kupunguza Mapato ya Serikali, hata hivyo Kamati haijawahi kupewa fursa hii. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba si kanuni za Bunge wala Sheria ya Bajeti inayoipa Mamlaka Kamati ya Bajeti kupitia mapendekezo hayo kabla ya kupelekwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba utaratibu na mchakato wa maoni na mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ni jukumu la nchi husika na sio la Afrika mashariki na hakuna Sheria inayomzuia Waziri wa Fedha na Mipango kushirikisha Bunge kabla ya kuyafikisha katika ngazi ya Jumuiya hiyo. Kamati ya Bajeti imefanya utafiti na kuona kuwa, utaratibu huu uliopo sasa una mapungufu makubwa matatu:- kwanza; Bunge, kutokuwa na Mamlaka ya kufanya mabadiliko kwenye vifungu vya Sheria ya Ushuru wa Forodha; Pili; Sekta binafsi nchini kuathiriwa na mabadiliko yanayofanyika katika Sheria hiyo ; Tatu, kutozingatiwa vizuri kwa usalama wa kiuchumi (*economic intelligence*).

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inaliomba Bunge lako tukufu liridhie na kutoa maelekezo kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwasilisha maoni na mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili yajadiliwe na Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Bunge kabla ya kuwasilishwa kwenye Jumuiya na hatimaye Kamati iweze kuwasilisha Taarifa yake kwa manufaa ya Bunge na wananchi wote kwa ujumla.

4.11 Utendaji Kazi wa Kikosi Kazi cha Kodi (*Tax Task Force*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikuwa na vikao mbalimbali na Sekta Binafsi ambapo kupitia vikao hivyo masuala mbalimbali yanayohusu changamoto za kikodi zinazowakabili zilijadiliwa. Pamoja na mambo mengine Sekta Binafsi imekuwa ikilalamikia utendaji kazi wa Kikosi Kazi cha Kodi hasa kwa upande wa idadi ya wajumbe wa Sekta Binafsi wanaoruhusiwa katika kikosi kazi hicho; Pili, ufinyu wa muda wanaopewa kujadili masuala ya kodi na Tatu, mapendekezo mengi kutofanyiwa kazi na Serikali bila ya kutoa sababu maalum au mrejesho kwa wadau.

Mheshimwa Spika, ieleweke kwamba uwepo wa Sekta Binafsi inayokuwa ndio msingi madhubuti wa Serikali kukusanya mapato ili iweze kuhudumia wananchi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya muundo wa Kikosi

Kazi hicho ili kuondoa mapungufu yanayojitokeza pamoja na kuangalia upya sera za utozaji kodi katika mawanda mapana ya kiuchumi na kijamii na sio katika ukusanyaji wa mapato tu.

4.12 Uendelezaji wa Sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa Mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika muda tofauti tofauti Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuhakikisha kwamba inalea na kuendeleza Sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali lakini hali imekuwa si hivyo. Mfano Sekta ya mawasiliano kwa mujibu wa Taarifa ya TCRA inaonyesha watu zaidi ya **milioni 2.5** wameondoka katika mfumo wa usafirishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki. Aidha, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa fedha na bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kama pombe kali spirits zimeshuka kwa asilimia 30. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba sera zake za kikodi kwa Sekta zinazokuwa ziwe zina lengo la kulea na kuendeleza sekta hizo na sio kukusanya kodi kiasi ambacho kinaathiri hata ukuaji wa Sekta husika.

4.13 Chuo cha Utawala wa Kodi (*Institute of Tax Administration*)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utawala wa Kodi (*Institute of Tax Administration*) kimechaguliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa kituo cha Umahili cha Masuala ya Masomo ya Kodi na Forodha (*Centre of excellency*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Chuo cha Utawala wa Kodi kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hata hivyo, kwa sasa eneo la chuo ni finyu na miundombinu yake haijawa ya kisasa zaidi ili kukiwezesha kukidhi ubora wa kimataifa katika masuala ya kodi na ushuru wa forodha. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya chuo hiki ili kukiwezesha kujitanua na kujenga kampasi mpya katika eneo la chuo la Misugusugu pamoja na kununua vifaa na kuboresha miundombinu ya chuo ili kikidhi vigezo vya kimataifa

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini na Makamu Mwenyekiti, kwa ushirikiano anaonipatia. Pia, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kuchambua na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajuka, Mb
7. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb
9. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
13. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
19. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt

Ashatu K. Kijaji Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri kutoka kwa Wajumbe wa Kamati wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na wadau wa Sekta Binafsi kwa ushirikiano walloutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa Ilijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu manane (8) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Jitu Vrajlal Soni (Mb)
MAKAMU MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
04 Juni, 2018

SPIKA: Sasa tunaingia katika uwanja wa uchangiaji wa hoja iliyo mbele yetu iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango. Kama nilivyokuwa nimeahidi mwanzo tutaanza na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hata hivyo, naomba kwa ruhusa yako kabla sijasema ninayotaka kusema, nitoe shukrani za dhati kabisa kwako wewe mwenyewe, Katibu wa Bunge na timu yenu ya wafanyakazi wa Bunge kwa jinsi mlivyokuja kutufaraji huko Kakonko. Wewe mwenyewe umesafiri kilometa 816 hadi Kakonko, tunakushukuru sana. Umeonesha mapenzi makubwa sana na kwa kweli familia inashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee pia naomba niwashukuru Wabunge wote, lakini hasa wale Wabunge 27 waliokuja Kakonko pale, tunawashukuru sana kwa kuja Kakonko, kwa kuja kutuhani.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako nimeagizwa pia na familia ya marehemu kwako wewe mwenyewe, mengine nitakwambia tukiwa faragha, lakini mama yake mzazi, kaka zake na mke wake wanashukuru sana, sana kwa kazi iliyofanywa na Bunge, kwa jitihada iliyofanywa na Bunge hadi kufikisha mwili wa marehemu Mheshimiwa Bilago nyumbani kwao. Tunasema ahsante sana na Mungu awape nguvu na afya tele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende kwa Wizara, kwanza, naunga mkono hoja hii, hoja muhimu sana. Pia niwape hongera ya kazi Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kijaji; Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na timu yote ya Wizara bila kumsahau Mkurugenzi Mtendaji wa TRA wanafanya kazi nzuri, hongereni sana, mazingira haya ni

mapya, wachape mwendo, tuko vizuri na wao wako vizuri. Sisi Wabunge wengi tunawapa hongera ya kazi, tunawatakia kazi njema katika mazingira haya mapya, hakuna kukata tamaa, ni kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina machache, nina mambo matatu hivi, nitakuwa na hili la Wazabuni, nitazungumzia *TRA* Kasulu, nitazungumzia miradi ya *PPP* na mwisho kama muda utaniruhusu nitazungumzia soko la bidhaa, *commodity exchange market* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hili la malipo ya Wazabuni, nashauri *sincerely* hili jambo nimesoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 24 mpaka 26 amezungumzia malipo ya wazabuni. Hata hivyo, lipo tatizo kubwa kati ya madai ya Wazabuni, muda wanaotoa huduma zao, uhakiki wa madeni haya na hadi hawa watu kulipwa jamani.

Mheshimiwa Spika, hivi inawezekanaje Mzabuni analisha shule zetu za sekondari na zingine za msingi hizi za shule maalum, anawezaje kukaa anadai Serikali miezi 11? Huu uhakiki maana yake nini? Nafikiri wenzetu wa Wizara ya Fedha hii waichukue k ama changamoto, hawa *suppliers* wetu waki-*supply*, nitoe mfano tu mdogo, kwa sababu kuna wapiga kura wangu walitoka Kasulu, Buhigwe na Kibondo kuja hapa na nikakutana nao; wanadai TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu wa TAMISEMI amewaandikia Hazina madai mbalimbali ambayo yameshahakikiwa. Madai hasa hasa ya Wazabuni wa elimu na wiki jana hiyo barua mwenyewe nimebahatika kuiona kwa sababu ilikuwa ni *pressure* kubwa sana. Inawezekanaje Mzabuni adai Serikali miezi 11. Naomba sana kupitia Wizara hii na wenzake Serikalini, warekebishe utaratibu, kweli wafanye uhakiki, tujiridhishe kwamba madeni haya ni halali, lakini Wazabuni wenye madeni halali walipwe kwa wakati jamani. Inachukua muda mrefu sana, sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Jimbo langu la Kasulu peke yake Wazabuni wanayodai elimu, wanadai elimu zaidi ya shilingi milioni 500 na wamesubiri zaidi ya miezi kumi na kwa bahati nzuri kile kitabu cha madai mwenyewe nimekiona. Naomba sana wenzetu wa elimu mjaribu ku-*fast track*, wafanye uhakiki kweli, tujiridhishe na madeni, lakini hatimaye madeni haya yalipwe.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika madeni ya Mawakala wa mbolea. Hilo limekuwa sasa ni kizungumkuti. Mawakala hawa tangu niko Kamati ya Kilimo miaka miwili iliyopita tuliletewa orodha na orodha ilikuwa inahakikiwa basi tuombe Mheshimiwa Waziri wale ambao wameridhika kwamba wana madai halali ya pembejeo walipwe basi fedha zao.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wale mnaoongeaongea hapo hasa kule kushoto yaani watu wako sokoni kabisa, kule mwisho kule, nawasikia kule mwisho yaani wana mikutano ya hadhara kabisa. Tunawaombeni sana tumsikilize mchangiaji. Endelea Mheshimiwa.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu wa dakika moja, mbili huo tafadhali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia juu ya hawa wazabuni ambao wame-*supply* mbolea. Nakumbuka tangu kwenye Kamati ya Kilimo limejadiliwa jambo hili na Waziri wa alituletea orodha ya wanaodai, lakini kukawa kwamba linafanyiwa uhakiki. Ni jambo jema, lazima tujue nani hasa tunamlipa, lakini wale waliohakikiwa tafadhali sana, wale ambao wamejiridhisha kwamba hawa ni wadai halali walipwe fedha zao, muda umekuwa mwingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii sintofahamu ya Mabenki kuwatisha, kuuza mali zao, nadhani haijengi heshima ya Serikali, nina uhakika wala hata haijengi heshima ya Chama

cha Mapinduzi. Naomba sana, wazabuni halali walio-*supply* huduma ya pembejeo na kadhalika walipwe baada ya kuwa wamefanya uhakiki na kuwe na *timeframe* kwamba wazabuni hao wanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni jambo kidogo ambalo liko *local*, sisi Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kibondo na Kakonko, Wilaya ya Kasulu na Buhigwe hatuna ofisi za *TRA*. Naomba kupitia kwa Mheshimiwa Waziri sina uhakika kama anaijua Buhigwe, Kasulu na Kibondo iliko sina uhakika. Haiwezekani *TRA* waendeleo kukaa kwenye vijumba vya kupanga panga...

SPIKA: Mheshimiwa Nsanzugwanko huna uhakika kama Mheshimiwa Waziri anapajua Buhigwe?

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, eehhh! Maana yake angekuwa anapajua pengine angekuwa ameshajenga Ofisi ya *TRA*, ndivyo ninavyofikiri hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana watujengee Ofisi za *TRA* angalau wenzetu wa Wilaya ya Kakonko na Kibondo wanaweza kuwa na *TRA* moja pale Kibondo wakai-*share* na sisi Kasulu na Buhigwe tukawa pia na Ofisi ya *TRA*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anajua sisi Halmashauri ya Mji wa Kasulu tumeshatoa Kiwanja bure kwa ajili ya kujenga Ofisi za *TRA*. Sasa kile kiwanja kinakuwa chaka, kinakuwa pori, ningeshauri sana kupitia yeye na Mkurugenzi Mtendaji wa *TRA* nadhani ananisikia hapa watujengee Ofisi ya kisasa ya *TRA*. Mji wa Kasulu na Mji wa Kibondo ni miji inayokua kwa haraka sana, inahitaji huduma za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ambalo napenda nilisemee ni hii miradi ya *PPP*; nimesoma kwenye kitabu cha bajeti, umezungumzia *PPP* karibu kurasa tatu, lakini katika maelezo ya Waziri haoneshi *exactly* ni mradi gani wa *PPP* ambao Serikali ume-*finalize* sasa unatekelezwa hakuna hata mmoja, ni maelezo tu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya PPP tangu tumeitunga ndani ya Bunge hili ni zaidi ya miaka 10 sasa. Sasa ningependa pengine Waziri atakapokuja atueleze ni miradi ipi hasa wamei-finalize ya PPP ambayo inakwenda kutekelezwa na pengine ikibidi pia waitofautishe kati ya miradi ya huduma na miradi ya uzalishaji. Nawiwa sana hii PPP tungejielekeza kwenye miradi ya kilimo na ufugaji maeneo ambayo tuna uhakika yatazalisha fedha ili tuweze kupata fedha zingine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa niliseme, ni hii *commodity exchange market*. Waziri ameileza sana ukurasa wa 63 mpaka ukurasa wa 65, hili ni jambo geni. Kwanza ningeomba kupitia kwako pengine Wabunge wote tungepitishwa kwenye somo hili, hii *stock exchange* ni kitu gani? Kuna maelezo mengi sana pale na baadhi ya Makampuni ambayo yamekuwa *registered* kwa ajili ya kuhudumia hii *commodity exchange*.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wabunge wenyewe tungepata semina kubwa tukaelewa maana ya jambo hili. Ni jambo kubwa sana na nchi zingine zinatumia jambo hili kwa ufanisi mkubwa sana, lakini hapa bado ni kitu kipya, sisi wenyewe Wabunge hatukielewi vizuri, ningeshauri kupitia kwako tuwe na semina ya Bunge zima kuhusu hiki kitu kinachoitwa *commodity exchange market*. Ni kitu muhimu sana, lakini sina uhakika kama kinafahamika vizuri. (Makoff)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa sababu Wizara hii ya fedha ndiyo wanagawa rasilimali fedha, naomba niendeleo kuwakumbusha na hili nitalisema sana hata kwenye bajeti kuu, miradi ile ambayo tumeshaanza nayo itekelezwe, ikamilike.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyakanazi ile uliyopita kutoka *Airport* mpaka Kakonko ndiyo inaitwa barabara ya Nyakanazi, umeiona, hipitiki. Sasa kwa sababu nakumbuka tangu mwaka jana ni moja ya miradi ya vielelezo...

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nsanzugwanko nakushukuru sana.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Miradi ya vielelezo naomba itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii. (*Kicheko*)

SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na Mheshimiwa Nsanzugwanko kuhusiana na barabara ya Nyakanazi tokea nimekuwa Mbunge hapa nasikia Kigoma-Nyakanazi toka nimekuwa Mbunge kipindi cha kwanza, kwa kweli watu wa Kigoma mnaonewa inabidi tuwasaidie, mpigiwe debe, mpo porini sana, mmetengwa. Nadhani Wizara watasaidia kidogo, ilikuwa mara ya kwanza kufika Kigoma kwa kweli mko nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye Wizara hii; naamini Wizara hii ya Fedha na Mipango ni Wizara ya Fedha na Mipango, lakini kwa mtazamo wangu naona wamejikita zaidi kwenye fedha kuliko kwenye mipango na kwa kuwa wao ni Wizara ya Fedha na Mipango walipaswa wawe ni Dira kubwa ya Taifa ili kulingoza namna gani ya kupata hizo fedha halafu kisha wakusanye, lakini Wizara hii katika utendaji wao wamekuwa kama vile ambavyo wanataka wamkamue ng'ombe ambaye hawamuandalii mazingira mazuri ya kutoa maziwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayosimamia Dira ya Taifa, Wizara hii ndiyo inasimamia Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa, lakini kwa bahati mbaya toka Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani kuna mipango mingi ambayo inatekelezwa na Wizara hii ni ile ambayo haipo kwenye Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi siyo Mchumi, *I am Theologian by professional*, inanichanganya kidogo kwamba sasa hiyo mipango ni ipi wanayoisimamia kwa sababu tunakuwa na *priorities*, tunaweka mikakati, lakini mwisho wa siku tunapokuja kwenye utekelezaji wanaleta vitu vingine kabisa ambavyo havikuwepo kwenye mpango wa nchi, wanaanza kufanya vitu ambavyo havipo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, hakuna mtu anayekataa *move* ya kuhamia Dodoma, lakini haikuwepo kwenye Mpango wa Miaka Mitano, *it was more of a political than economical*, imetulete shida, tunahangaika, hatukuwa na Ofisi, imechanganya mambo mengi sana katika kuendesha nchi yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango...

SPIKA: Sasa hapo Mheshimiwa Msigwa unamgusa Spika.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, najua hapo umeguswa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena, hatukatai kuhamia Dodoma lakini hatukuwa na mpango huo, hela tumeitoa wapi? Ntoa mifano kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine ambao naweza kusema, mipango hii ambayo inafanywa ambayo haikuwepo kwenye mpango wa nchi, inaleta tabu katika nchi yetu. Nitoe mfano mmoja wa haraka haraka, kwa wastani TRA wanasema kwa sasa hivi wanakusanya wastani wa trilion 1.3 mapato kwa mwezi. Hata hivyo, mapato haya ukiangalia wao wamekuwa kama Wakala tu, hela nyingi wanazokusanya siyo za kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wanachukua *wharfage*, wanachukua hela zote za halmashauri, *property tax* kwa mfano za majengo wamechukua, wamechukua zile *VAT refundable*, wamechukua mpaka zile *levy* za korosho, wamechukua hela nyingi ambazo siyo za kwao halafu wanapita mitaani, barabarani kwa wananchi kisiasa

wanasema sasa hivi tumedhibiti mapato yanakuwa mengi. Wakati huo huo hizo hela walizotunyang'anya kwenye halmashauri zetu mnazi-*ground* halmashauri, hazifanyi kazi vizuri, yaani hadi hela za *REA* nazo wanasema za kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamezi-*ground* halmashauri, sasa leo hiyo mipango una-*match* vipi mipango na jinsi ambavyo wanakusanya hizo pesa. Matokeo yake katika halmashauri wameshindwa kupeleka wataalam wazuri, wameamua tena ku-*centralize* ambapo ni mipango iliyoshindikana toka tumepata uhuru, tulijaribu tukakwama.

Mheshimiwa Spika, kwenye Majukwaa wanasimama kwamba wanakusanya pesa nyingi, lakini zile pesa ambazo wametunyang'anya kwenye halmashauri hazirudi kwa sababu hakuna mipango mizuri. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri katika mipango yake angeishauri Serikali hii kwamba kupeleka watendaji katika halmashauri ambao hawana weledi, ambao wameenda kisiasa kunaharibu utendaji wa kazi kwa sababu nchi hii mtu akiwa Mwanasiasa anaaminika kwamba anajua kila kitu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku moja Katibu aliyeondoka Dkt. Kasilillah alisema hapa Wabunge tukianza hapa kuzungumzia masuala ya *nuclear* tutataka tuchangie hata kama hatuyajui. Pia tunaamini kwamba mtu akiwa mwanasiasa anajua kila kitu na nategemea Wizara ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango ingekuwa ndiyo dira ya kuishauri Serikali hii. Tumekuwa na mipango mingi ambayo iko nje ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia wakati wa Dkt. Kikwete, Dkt. Kikwete ameondoka hapa tunakusanya *900.0 billion* *900.0* ambazo hakukusanya hizi hela za wengine. Inaonesha yeye *system* zake zilikuwa zinafanya kazi vizuri lakini wao wame-*intefere* maeneo mengine yote, wanataja pesa kubwa hii lakini bado utekelezaji haupo. Sasa wanatangaza hizo pesa zote zipo zinakusanywa, kwa nini kwenye pesa za maendeleo pesa hazirudi kwenye maeneo yetu tunapotoka

kama hizi pesa zote wanazikusanya? Mfano mzuri, kwenye kitabu cha Kamati wamezungumza mpaka Disemba, 2017 Serikali ilikuwa imekusanya *7.6 trillion* na mpaka Februari, 2018 walilipa deni la nje triloni 5.5 maana yake tulibakiwa na triloni mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaendeshaji hii nchi kwa utaratibu huo kama hela zote tunazokusanya tunalipa madeni na bado kwenye kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri ukisoma ukurasa wa 96 amezungumza na hawa wamesema, anasema kwamba deni bado linahimilika lakini mzigo mkubwa bado anabeba mwananchi wa Tanzania. Wakitoka nje kisiasa wanasema kila kitu kipo safi, tunapongezana hapa, mtumbwi unazidi kuzama, kiuhalisia tuna-*suffocate*, hakuna *oxygen* katika nchi hii bado tunazama. Kila mtu anaamua anavyotaka, tutapigiana makofi hapa lakini hela hamna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye kila Wizara kama ni Wizara zipo zimepata pesa zaidi ya asilimia 50 na kitu ni chache sana, zote ziko chini ya kiwango. Kama tunakusanya mapato hayo Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa nini Wizara zote zinapata pesa chini ya kiwango? Haya ni masuala ambayo anatakiwa atujibu na ningeomba katika suala hili anijibu hela halisi ambayo anakusanya kodi ya *TRA* bila kuchanganya na hizi nilizomtajia, *wharfage* zile za Halmashauri, sijui *VAT refundable* za watu wengine ambazo wanashika ni shilingi ngapi? Tujilinganisha na Serikali iliyopita na ya sasa kama tunakwenda pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine kama nilivyozungumza, mipango mingi anayotekeleza sasa hivi Mheshimiwa Waziri haikuwepo kwenye Mpango wa Miaka Mitano. Hatukuwa kwenye mpango wa miaka mitano kwamba *we will move from Dar es Salaam to Dodoma*, kwenye mpango wa miaka mitano hatukuwa na *standard gauge, where are we getting the money?*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hizi hela ukiangalia kiutaratibu wamekopa mikopo ya *commercial* ambayo ni

very expensive. Tunakopa mkopo kwa sababu *commercial* unakopa mkopo, unaanza kulipa mkopo huo mapema kabla ya ule mradi wa *longterm* haujaanza kuzalisha sasa ku-*service* huu mkopo tuta-*service* kupata hela, itatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atupe majibu hapa. Ukiangalia Ethiopia au Kenya wao walipata *concession loan* ambayo ukikopa wale watu watamaliza ule mradi, halafu wakishamaliza ule mradi, unapoanza kufanya kazi ndipo unaanza kulipa. Ni kitu gani kimesababisha wasiende kwenye mikopo hiyo, wameenda kwenye mikopo hii ya *commercial loan*? Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango ningeomba anijibu. Kwa hiyo, kuna mipango mingi ambayo tunafanya lakini haikuwepo kwenye utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tumeenda kwenye mambo ya *Stiegler's gorge* hapa, tatizo la Tanzania siyo kwamba tuna tatizo la umeme, tatizo ni kuuhamisha umeme ulipo kwenda kwa walaji. Hizo *megawatts* zote tunazoitaka tunataka tuzifanyie nini? Ambapo tutachukua hela ya sasa, kwenye *longterm loan* ambazo zinakuwa ni mzigo kwa Watanzania wakija hapa wanasema mkopo bado unabebeka. Haya ni mambo siyo suala tuje tushangiliane hapa. Bado nam-*challenge* Mheshimiwa Mpango yeye ndiye dira ya nchi yetu. Hii mamlaka inatoka wapi ya kwamba wanaleta mipango ambayo haipo kwenye mipango ya miaka mitano? Haya ndiyo yanayotuchanganya, yanatuchanganya kama Taifa hatuelewi tushike lipi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yote yaliyofanyika, sasa hivi nimezungumza hapo mwanzo kwamba, tumefika mahali tuna-*centralize* kila kitu ambapo hayo mambo yalishindikana hapo mwanzoni, sasa hivi halmashauri zote tumezi-*ground* tunarudi kule kule ambako tulishindwa. Ilitumika pesa nyingi sana kuunda Serikali za Mitaa, kuzi-*empower* Serikali za Mitaa tulitumia pesa nyingi sana hizi *D by D* leo tena tumerudi kule kule kitu kinafanyika Dar es Salaam, kila kitu wanataka kifanyike sijui Dodoma ambako tumezi-*ground* Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hii mipango inekuwa ina-*empower* watu wa kule chini inge-*empower* watu wa chini waone kama wana-*own*, wame-*complicate*. Naamini na elimu yangu ndogo hii niliyonayo, elimu hai-*complicate* mambo, elimu ina-*simplify* mambo, lakini ukiangalia mipango yote tunapiga mapambio mengi kwenye vyombo vya habari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jana wakati nasoma *report* hapo nimesikia kwenye *report*wenzangu walifanya siwa-*challenge* lakini nilishangaa wanashangaa mtu analipwa milioni 96 (Dola 40,000) tunashangaa mtu analipwa eti Dola 40,000, *this is poverty mentality*. Yule mtu kwanza ameingia mkataba na wale watu, zile hela siyo za kwetu, akilipwa milioni 96 kwanza atalipa kodi milioni 30 si zitakuja hapa nchini, tuna hasara gani sisi? Kodi milioni 30 zitakuwa hapa nchini, tutawaaminisha Watanzania kwamba mtu akilipwa milioni 40 kama ni laana, *that is poverty mentality*.

Mheshimiwa Spika, watu wangelipwa hela zaidi ya hizo ilimradi hawavunji sheria, sasa kwa mfano, waki-*import expert* ambaye huwezi kumpata tena ni wa gharama utamlipa Sh.200,000 tunazolipana lipana hapa? Wachezaji wa mpira wanalipwa hela nyingi kwa sababu ya *professionalism* walizonazo, sasa tusifike mahali tunakuwa *sadist*, tunawachukia watu wanapolipwa hela nyingi badala ya ku-*encourage* watu walio chini walipwe zaidi, sisi tunasema analipwa zaidi, kwa hiyo ashuke chini, *are we serious?*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwa ujumla, *I am Theologian anyway I am not an economist* lakini nataka kusema Mheshimiwa Mpango atuongoze, atusaidie...

SPIKA: Yaani hakuna hata taarifa hata katika uongo huo jamani?

WABUNGE FULANI: Aaaaah! (Kicheko/Makofi)

SPIKA: Tayari? ya pili? Oohhh! basi Bwana kumbe ndiyo maana hawakukupa taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, umeshindwa kuvumilia kidogo?

SPIKA: Tayari imeshakwisha. Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, tafadhali.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Wizara hii kubwa, Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kabisa niungane na waliopita kuzungumza japo kwa ufupi au hata kuitaja barabara ile inayokwenda Kigoma kutoka Nyakanazi kwamba ni barabara muhimu na ni barabara ambayo nilipata fursa na mimi kwenda kwenye msiba ule wa kumsitiri Mwalimu wetu, Mbunge mwenzetu Mwalimu Bilago, nikaona mazingira yalivyo, nikaona barabara ilivyo kwa kweli inahuzunisha na inatia huruma sana.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba ni miongoni mwa barabara zile ambazo siku za mvua magari yanazama kwenye mito ikisubiri siku mbili au tatu wananchi wapate kupita kwa ajili ya kufika Kigoma na maeneo mengine ya kule. Kwa hiyo, ni vyema Wizara ya Fedha barabara ile waingalie kwa jicho la huruma sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ukiangalia kitabu cha Kamati ukurasa wa 26 kumezungumzwa hizi milioni 50 kila kijiji, lakini ikiwa Serikali ya Awamu ya Tano hii inakwenda ukingoni tena tunakwenda kwenye mwaka wa tatu sasa, Waziri wa Fedha anakuja hapa kutuaminisha kwamba sasa kumetengwa jumla ya bilioni 60 ambazo zinakwenda kufanya utafiti yaani *pilot studies* kwa ajili ya kuona kwamba vipi tutafanikisha mpango huu wa milioni 50 kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kwamba, kwa miaka mitatu sasa bado tunakwenda kwenye *pilot studies*,

kwenye kufanya *research* kuona vipi tutafanikisha utoaji wa fedha hizi, lakini tukumbuke kwamba milioni 50 kila kijiji ni ahadi ya Rais na imo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hii inamaanisha kwamba wananchi Watanzania tuliwadanganya. Tuliwadanganya kwa sababu kama hadi leo miaka mitatu fedha hii haijatoka ina maana hakuna dalili na bado tunakwenda kufanya *study*, bado hakuna dalili ya Watanzania kupata fedha hii na ni wazi kwamba huu ulikuwa ni usanii wa kisiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu mfumo wa kodi ambao mara nyingi tumekuwa tukiuliza na umekuwa ni wenye utata kwa kiasi kikubwa sana. Naomba nitoe maelezo kwamba mifumo ya kodi kwenye bandari hizi za Afrika Mashariki inatofautiana sana kutokana na *interest* za nchi na tozo ambazo zimo katika kila nchi ambayo inahusika na Bandari hizo husika. Kwa mfano, *container* ambalo lina futi 20, ina uzito sawa, thamani sawa, bandari ya Dar es Salaam wanatoza dola 240 wakati bandari ya Mombasa wanatoza dola 70 tu, hii ni tofauti kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kontena ambayo urefu wa futi 40, bandari ya Dar es Salaam wanatoza dola 420, wakati bandari ya Mombasa wanatoza dola 105, hii ni tofauti. Gari ambayo ina thamani ya dola 10,000 bandari ya Dar es Salaam wanatoza 1.6% wakati Bandari ya Mombasa inatoa 0.8% hii ni tofauti kubwa. Kuonesha kwamba utofauti huu haupo tu baina ya Bandari ya Zanzibar ambayo kila siku inakandamizwa, inaonewa kwa sababu tu ya mfumo huo wa kodi lakini suala hili haligusi bandari nyingine za Mombasa na bandari nyingine ambayo ziko ndani ya Afrika Mashariki na Kati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini, nitakachokizungumza hapa, tumekuwa tukiuliza mara nyingi kwamba, vipi mifumo hii ya kodi ambayo inaenda kuua uchumi wa Zanzibar, inaenda kuua bandari ya Zanzibar, lini itapatiwa ufumbuzi na lini Wanzanzibari wataachwa

waendeleze masuala yao ya biashara bila kulazimishwa kwamba eti wafuate mfumo wa *TANCIS*,kwa sababu tofauti hii zipo kila mahali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamikia suala hili sana, nataka nioneshe sisi kama Wabunge kutoka Zanzibar kwa sababu sisi Wabunge kutoka Zanzibar Jimbo letu ni kama Zanzibar. Kwa sababu kama Mbunge siwezi kuzungumzia suala la maji Jimboni kwangu, siwezi kuzungumzia suala la kilimo jimboni kwangu, kwa hiyo, jimbo langu ni Zanzibar sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia masuala hapa, hata leo tumezungumzia masuala ya kodi ya umeme. Sisi tumeuziwa umeme na *TANESCO* lakini tumeuziwa kwa bei ambayo si sahihi. Tumekuwa tukilalamikia, Serikali kupitia Wizara ya Fedha inatuambia tunazungumza. Tumekuwa tukizungumzia tozo za bandari haziko katika mazingira sahihi kwa bandari ya Zanzibar. Kodi zile zinaua bandari ya Zanzibar, tumeambiwa suala hili tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza masuala ya vyombo ya moto, tumelalamika sana, leo ni vitu vya ajabu sana, leo mtu kutoka Burundi, mtu kutoka Kongo, mtu kutoka Zambia anaingia Tanzania na gari lake, anatumia miezi miwili kwa kujaza tu fomu pale mpakani, halafu anaweza kuongeza tena miezi miwili lakini mtu kutoka Zanzibar huu ni uonevu, udugu uko wapi? Mtu kutoka Zanzibar hana uwezo wa kuleta gari Tanzania Bara akaweza kutumia. Huo udugu wa damu uko wapi?

Mheshimiwa Spika, kila siku tunasema udugu wa damu, tunadumisha, tunadumisha ndio ni sahihi, hakuna anayekataa umoja lakini umoja uwe na nia njema. Tukizungumza haya tunaambiwa tunazungumza, tutazungumza mpaka lini? Miaka 54 ya Muungano, kero hizi zimeanza muda mrefu zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku akija Waziri wa Fedha tutazungumza, akija Waziri mwingine yoyote, tunazungumza,

tunazungumza mpaka lini? Juzi hapa tumelalamikia masuala ya Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Leo tumeona kwenye kitabu kwa ajili ya Tume ya Pamoja ya Fedha inafanya kazi gani? Mheshimiwa Mpango kwenye hotuba yake amesema kabisa kwamba, tayari tume ile imekamilisha kufanya utafiti. Sasa hii fedha iliyotengwa hapa ya nini? Maana amesema mshahara ni *zero points*.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna mshahara *zero points* sasa ile bilioni ngapi uliyoitenga imo kwenye kitabu ni ya kazi gani kama watu wamekamilisha utafiti na hii akaunti itaanzishwa lini ili tuone sasa kuna *equality* kwenye masuala ya mgawanyo wa fedha za muungano. Kuna *equality* katika makusanyo ya fedha za muungano, tujue nani anahusika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yote haya tunaambiwa tunazungumza. Huu unaoendelea unaitwa ulaghai wa kisiasa ambao hakika kila siku unaendelea kudumaza na kuu maendeleo ya upande mmoja wa Muungano. Kwa sababu hizi zote ambazo nimezizungumza hapa hizi ndizo *channel* za maendeleo katika Taifa, katika nchi. Zanzibar ni nchi ya visiwa inajitegemea kimaendeleo ina Serikali yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuendeleo kuangalia, Mheshimiwa Mpango aje atujibu sasa haya masuala ya kodi bandari na tozo. Leo Zanzibar pale unasafirisha hata vitenge 10, kanga 10 au tano, *TV* moja ya kuja kuangalia mwenyewe ukija pale unapigwa *difference*. Leo wafanyabiashara wote soko lote, tulilokuwa pengine lingekuwa soko linaloenda kuchukua bidhaa Zanzibar kuleta maeneo ya Tanzania Bara miko tofauti leo wamehamia Uganda.

Mheshimiwa Spika, tukitoka hapo nje tu hapo wajasiliamali wapo wanasema hili shati linatoka Uganda hili, shati hili linatoka Kongo, kitenge hiki kinatoka wapi, wale wote walikuwa wanakuja Zanzibar wanachukua bidhaa na kuleta Tanzania Bara kuuza, leo soko lile wafanyabiashara wa Zanzibar limekufa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme mwisho leo tunaambiwa hapa bidhaa zinazotoka na inasikitisha sana maji, kama kuna maji Zanzibar yanayozalishwa na kiwanda kilichopo Zanzibar hayaruhusiwi kuuzwa Tanzania bara. Inaashiria nini? Tulipiga marufuku sukari wakasema Zanzibar haitoshi. Hivi vifaa vyote, bidhaa zote zinazouzwa Tanzania Bara, zinazozalishwa Tanzania Bara ndio zikavushwa Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, sio kweli huu ni usanii wa kisiasa ambao kimsingi haukubaliki, lakini tukisema tunazungumza hivi tunazungumza na nani? Tunazungumza na mtu ambaye hana mamlaka, mtu ambaye hana uwezo wa kusema, mtu ambaye wanaenda kuzungumza naye asubuhi jioni wanamwona mpuuzi wanasema achana naye yule. Sisi tunaendelea na mambo yetu, hili haliwezekani.

SPIKA: Mheshimiwa Juma, lugha unazozitumia kidogo.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, samahani sitorudia tena

SPIKA: Hawa wanaozungumza ni watu wazima na akili zao sasa, waheshimu tu kwa mazungumzo yao. Endelea tu Mheshimiwa.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante nitajirekebisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze hayo kwa masikitiko makubwa nikijua kwamba Wizara ya Fedha na Mipango itakuja na majibu ya haya sasa kuona kwamba vipi tunaenda kutatua hizi changamoto ambazo tumezitungumza hapa, kwa nia njema kabisa na kwa nia njema kwa nchi hizi. Hizi *story* za kwamba tunazungumza, tunazungumza *at least* zifikie mwisho sasa tuone kwamba maendeleo haya yanakuwa kwa Tanzania nzima na sio upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar haina pa kwenda, Zanzibar hatulimi mahindi, Zanzibar hatulimi nyanya, Zanzibar

hatulimi, yote tunatumia kutoka Tanzania Bara na yanaingia vizuri tu, lakini leo kinachozalishwa Zanzibar unaambiwa lazima tukifikie kiwango hiki, lazima tutoe hiki. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kombo Juma Hamad. Ulipokuwa unachangia nilikuwa najitahidi sana Mheshimiwa Ally Keissy asisimame nikawa nahakikisha kabisa hatapata nafasi maana yake, ulikuwa unalitibua tayari.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kuna maboksi mawili ya mitandio kutoka Uturuki yaliingia huku juzi.

SPIKA: Hapana Mheshimiwa Keissy, maana Mheshimiwa Juma ulikuwa unachokoza nyuki. Mheshimiwa Leah Komanya tafadhali.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote napenda kupongeza Wizara ya Fedha kwa kazi wanazofanya ikiwemo za upelekaji fedha katika Serikali za Mitaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 32 Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Ugani na Ununuzi 75 kwa ajili ya mafunzo ya kutumia mfumo wa malipo wa Serikali *EPICOR*. Hata hivyo, mafunzo haya hayatakuwa na tija kama Serikali haitarekebisha upungufu uliomo katika mfumo wa *EPICOR*, kwa sababu mfumo huu unatumia *cash basis*. Kwa hiyo *LPO* sasa hivi zinaandaliwa kwa kutumia *cash* tu, asilimia kubwa ya *LPO* zinatumiwa nje ya mfumo, kwa hiyo dhana zima ya *internal control* au udhibiti wa ndani haipo.

Mheshimiwa Spika, upungufu mwingine pia upo ikiwemo *asset management* bado hazijawekwa humo,

naishauri sasa Wizara ione namna inavyoweza kutekeleza kuweza kuingiza *package* ambazo zinazopungua katika mfumo mzima wa *EPICOR*.

Mheshimiwa Spika, nishauri pia Wizara ijitahidi kuweka mfumo ambao utaweza ku-*link* mifumo mbalimbali kama *PLANREP* ili sasa taarifa mbalimbali ziweze kutoka katika mfumo wa *EPICOR* badala ya taarifa nyingine kutengenezwa nje ya mfumo ama taarifa baadhi za ufungaji wa hesabu zikafanyikia nje ya mfumo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze Wizara kwa namna inavyopeleka fedha za elimu bila malipo, inapeleka vizuri, nimeangalia katika kitabu cha *CAG* hoja iliyopo ni ndogo tu shilingi bilioni moja haikupeleka na upungufu huu ulitokana na Wizara yenyewe kule ya Elimu ambako kulikuwa kuna utofauti wa takwimu. Kwa hiyo, naipongeze kabisa kwa namna inavyopeleka fedha za elimu bila malipo. Niipongeze pia Wizara kwa kupeleka fedha za ujenzi wa vituo vya afya au kuboresha vituo vya afya. Vituo vyetu sasa hivi vilivyoboreshwa vina hadhi nzuri kiasi kwamba wananchi sasa hivi wana mvuto wa kwenda hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia kwa namna inavyopeleka halmashauri ruzuku za matumizi ya kawaida. Kumekuwa hakuna na matatizo ya upelekaji wa ruzuku za kawaida, lakini tukumbuke kwamba ruzuku hizi zilipunguzwa kutoka asilimia 100 mpaka 40. Ukiangalia pale pale mahitaji ya halmashauri yako pale pale, stahiki za watumishi ziko pale pale, mtumishi anatakiwa aende likizo, mtumishi anatakiwa agharamiwe masomo.

Mheshimiwa Spika, kwa kupunguza hiyo asilimia kutoka 100 mpaka 40 kumekuwa na changamoto kubwa sana inayozikumba halmashauri katika upungufu wa fedha. Pamoja na hayo halmashauri zilitegemea sasa wangetumia fedha za mapato ili kuweza ku-*accommodate* shughuli za idara zinazopata ruzuku.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ilizokumba halmashauri ni mapato mengine kuchukuliwa na Serikali Kuu na mapato mengine kupunguzwa. Kwa mfano, Mkoa wa Simiyu ushuru wa pamba ulipunguzwa kutoka asilimia tano hadi tatu kwa ajili ya *standardize* bei ya pamba. Halmashauri za Mkoa wa Simiyu zaidi ya asilimia 60, bajeti yake inatumia ushuru wa pamba.

Mheshimiwa Spika, changamoto zimeendelea kuzikumba halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Ukiangalia kazi ziko pale pale, Waheshimiwa Madiwani wako pale kwa mujibu wa Sheria, wanahitaji kulipwa, wanahitaji kufanya ziara, lakini saa hizi Madiwani hao wamekuwa wakikopwa fedha kwa muda mrefu zaidi hata ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao hao Madiwani tunategemea wakasimamie miradi ya maendeleo. Ukiangalia sasa hivi Serikali imejikita kutumia *force account* hilo ni jambo jema. Hapo hapo ukiangalia *force account* hiyo Wahandisi wengi wemeenda *TARURA*. Kwa hiyo, Madiwani ambao ni Wenyeviti wa *WDC* wanapaswa kusimamia ile miradi. Changamoto ukiangalia wenyewe kwanza hawana fedha wamekopwa, halafu wanaenda kusimamia *force account* ambayo kwa kiasi kikubwa ina-*involve cash*, pale Serikali ifanye tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha wafanye *review* kwa sheria ambazo tumezipitisha. Kwa mfano wa kupunguza rukuzu ya matumizi ya kawaida kutoka asilimia 100 hadi asilimia 40, kuondoa vyanzo vya mapato, wafanye *review* waangalie ni athari gani zilizopo katika halmashauri. Ikiwezekana sasa halmashauri hizi ziweze kupewa fidia, kama ilivyofanyika 2013 baada ya kupunguza vyanzo vilivyokuwa kero kwa wananchi, halmashauri zilipatiwa fidia mpaka leo hiyo fidia inaletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee kuhusu upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo, nikijikita katika

ruzuku ya uendelezaji wa mitaji za Serikali za Mitaa *LGCDG* au inavyojulikana kwa *CDG*. Ni miaka mitatu sasa hivi fedha hiyo imekuwa haipelekwi, fedha hiyo ni ya Wafadhili lakini sio asilimia 100. Kuna sehemu ambayo ni fedha ya mapato ya ndani ambayo inajulikana, kama *Local* kuna *foreign* na *Local*. Hata hivyo, ukiangalia hata zile fedha za *local* hakuna fedha iliyopelekwa katika miradi ya *CDG*. Kama wafadhili hawaleti je, Serikali ambayo inakusanya kwa nini haipeleki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali sasa ione namna inavyoweza kuinusuru miradi hii iliyotekelezwa kwa fedha ya *CDG* kwa sababu kila mwaka tunaopanga wananchi lazima waibue miradi na kuianzisha kwa ule mfumo wa *C-matching*. Kwa hiyo, miaka mitatu tumekuwa tukilimbikiza magofu, magofu, magofu kiasi kwamba tunawapelekea wananchi wanakuwa hawana imani sasa na Serikali waanza kupoteza imani kwa Serikali. Wananchi sasa hivi wametokea kuiamini sana Serikali ya Awamu Tano, sasa tusiwakatishe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya TAMISEMI ilifanya kikao iliwaita Waheshimiwa Wenyeviti na Wakurugenzi kwamba, waainishe miradi inavyoweza kutekelezwa ambayo inaweza kumalizwa na fedha ya *CDG* ili sasa iletwe, lakini mpaka ninavyoongea sasa hivi fedha haijaletwa. Tukumbuke halmashauri zingine ziliitisha Mabaraza Maalum, wakatamia fedha ili kuweza kupitisha miradi ambayo sasa inaweza ikatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tuone namna tunavyoweza kui-*rescue* hii miradi, mingine ina miaka 10, mingine ina miaka mitano na kama Mfadhili haleti fedha kwa nini tunaendelea kubajeti? Nashauri kama mfadhili hajaonesha nia ya kuleta basi kwenye hicho kifungu tuweke *token figure* ili mfadhili atakapoleta tufanye *supplementary budget*, kuliko kuendeleza kulimbikiza magofu, watoto wetu hawana madarasa, zahanati zetu hazijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Leah umegusa nyoyo za Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli fedha hizi za *CDG* muhimu kweli kweli, sana sana, vinginevyo Wabunge sijui keshokutwa tutakwenda kusema nini.

Basi tutaendelea na uchangiaji wakati wa jioni, orodha yote ambayo ninayo hapa nitaanza na Mheshimiwa Masoud Abdalah Juma, atafuata Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Mlinga utafuata na wengine. Wote ambao mpo kwenye orodha mtapata nafasi jioni ya leo.

Mheshimiwa Mchungaji alikuwa anasema kuhamia Dodoma umekuwa ni mpango wa dharura akawa amenigusa kweli. Mimi ninavyojua kutoka mwaka 1973 kwa Ilani zote za Chama cha Mapinduzi ambacho kimechaguliwa *all along* hakuna Ilani ambayo haikutaja habari ya kuhamia Dodoma hata moja. Waliokuwa hawaweki ni wale ambao walikuwa hawataki kuhamia Dodoma, kwa hiyo, walikuwa hawakipi kitu hicho *preference*. Hakuna mpango ambao ni wa muda mrefu *constantly* ukitaja *all the time* kama wa kuhamia Dodoma na hautekelezwi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hiki ni kitu kimekuwepo *throughout*. Ndio maana mpaka leo bado ile sheria ya kusema kwamba, Dodoma ni Makao Makuu haijaja. Ndio hiyo tunasema safari hii Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, katika Sheria zitakazosomwa mara ya kwanza safari hii Bunge hili hiyo lazima iwepo. Isipokuwa hiyo, safari hii hakuna sheria hata moja itasomwa kwa mara ya kwanza. Tulishasema, tukasema, sasa safari hii ni utekelezaji. Mwambie kabisa *AG*, kabisa, kama hiyo kitu haiko safari hii hakuna sheria itakayosomwa mara ya kwanza safari hii, kwa hiyo Bunge la mwezi Oktoba, halitakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge tunaahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni. (*Makofi*)

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lllisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni*)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea tulikuwa tumeshamtangaza toka asubuhi Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salimu tuanzishie *session* ya jioni.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wataala* aliyetujalia uzima na afya njema katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani katika kumi hili la *Maghfira* ikiwa ndio siku ya 19 na nikimwona rafiki yangu Mheshimiwa Ally Keissy ametulia kweli kweli leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tulitegemea makubwa kutoka Wizara ya Fedha. Tulitegemea fedha ambazo Waheshimiwa Wabunge tunazipitisha sisi katika maeneo mbalimbali fedha hizi za maendeleo zitakuwa zikitolewa, lakini imekuwa ni kizungumkuti; haifahamiki, hali ni mbaya, tatizo limekuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo katika Wizara mbalimbali hazitolewi kwa wakati hata zikitolewa basi inakuwa ni pungufu sana na inaonekana hadi sasa ni chini ya asilimia 40 ya fedha za maendeleo katika maeneo mbalimbali ya Wizara ambazo tumezipitisha. Hili ni janga kubwa, ni tatizo kubwa, tatizo ambalo wananchi mategemeo yao waliyokuwa na huyo yameondoka. Mheshimiwa Waziri wa Fedha atuambie tatizo hasa ni nini kwake Wizara ya fedha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye *volume II Treasury* mambo ambayo waliyojipangia katika maeneo mbalimbali, ukienda kwenye *book four*, nimwambie Waziri wa Fedha, kama kuna tatizo la vyanzo vya fedha, hana fedha ripoti ya Spika ambayo imewekwa juzi Jumamosi pale Mezani kuna fedha ambazo zilipatikana kwenye uvuvi wa bahari kuu, hivyo ni vyanzo, kuna mambo tayari yapo kwenye ripoti ya

Tume ya Spika aliyoiunda, vyanzo vya kutoka bahari kuu kuna matrilioni ya fedha, hebu aingie atafute fedha tatizo nini, mbona haeleweki, hasomeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu wastaafu, hali ya wastaafu ni mbaya sana, wastaafu wetu kwa kipindi kilichopita walikuwa kwenye kima cha chini kutoka Sh.50,000 hadi Sh.100,000 baadhi yao walio wengi, lakini ahadi yetu kwa wastaafu kwa hivi sasa inaonekana kama Serikali haina dhamira ya dhati kuboresha hawa wastaafu wetu ambao wastaafu walikuwa ni watumishi wetu, walifanya kazi kwa uadilifu kwa muda wa kipindi kirefu lakini hali zao za maisha ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii ukiangalia Waziri hana jambo ambalo la kushika zaidi akasema kwamba labda wastaafu hawa wataweza kupata maslahi yaliyo mazuri ukurasa 104 kaeleza mengi, lakini kasema tu kuna moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, wastaafu wetu katika kada mbalimbali hali zao ni mbaya sana. Nitoe mfano mmoja, wakati wastaafu kwenye Jeshi la Wananchi kuanzia cheo cha *private* hadi *Brigadier General*/Jeshini mafao yao yanakuwa ni madogo sana mbali ya hao wengine, hawa walifanya kazi, walikwenda kwenye vita, vita va Kagera, walikwenda Msumbiji na kwingineko, leo wanayafungua mageti kwa watu binafsi inaumiza kweli kweli hasa kuanzia cheo cha *private*, *Brigadier General*/hata hawa walinzi wetu hatuwathamini hawa walinzi wetu walipigana vita na Kagera, waliokwenda kuokoa Msumbiji hata hilo? Mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, mwenzake Waziri aliyepita Mheshimiwa Saada Mkuya aliweza kufanikisha kupandisha hizi *pension* za wastaafu kwa kila mwezi, hebu naye ajiandae, aandae mazingira mazuri apandishe hizi *pension* za wastaafu za kila mwezi kwa sababu hali imekuwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aangelie vilevile katika suala la wastaafu pale wanapostaafu, kwanza mafao yao wanacheleweshewa sana, lakini yeye amesema kwamba wataandaaa mazingira, mazingira hayapo kwa sababu gani kumekuwa na kudhulumiwa, kumekuwa na kunyonywa kwa wastaafu kwa muda mrefu hata ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mbalimbali zimekuwa zikisema kwamba mafao ya wastaafu wanapunjwa.

Mheshimiwa Spika, watu wamefanya kazi kwa uadilifu, wamechoka hata mafao yao, ripoti za CAG zipo kibao, nyingi sana ripoti mbalimbali kwamba mafao ya wastaafu wanapunjwa tangu mwaka 2013, angalieni ripoti za CAG, jinsi wastaafu wanavyonyonywa na kupunjwa. Kumbe wazee wetu maskini kwa sababu ya Serikali wanawadhulumu na kuwapunja tatizo nini? Mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme pale ambapo mstaafu anafariki. Anapofariki mstaafu wanafamilia wanafungua mirathi, lakini niseme tu kwamba inakuwa na milolongo mikubwa sana kuzipata zile haki. Familia inapofungua ile mirathi wakifika pale mahakamani ndani ya muda mfupi sana Hazina wanaambiwa kwamba hicho kitu faili lake halionekani. Baada ya mwezi mmoja kufa faili lake halionekani na hayo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mzee Bobali, baba yake mdogo Mheshimiwa Bobali hapa, muda mrefu tangu amestaafu huu ni mwaka wa kumi na hajapata mafao yake, ni tatizo kweli wanaofariki na wao mafaili yao wanaambiwa hayapo. Kwa kweli wastaafu wametupwa, wanaonewa hili ni jambo kubwa sana na jambo ambalo kwamba halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwamba hakuna kitu kinachoumiza kwamba watu hao walitumika katika hali nzuri sana wakati wakiwa na nguvu lakini wameachwa Mheshimiwa Waziri atuambie tatizo ni nini alionalo na ahadi

ya Serikali kwa wastaafu, kuna kipi kikubwa zaidi ambacho wanawapelekea mpaka leo wanakuwa maskini sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niache hilo, pale Hazina kuna bwana anaitwa nadhani Kasekwa, yule huyu ni mtu mmoja ambaye namwamini sana, kwa hiyo yale mafao ambayo yakitengenezwa na bila shaka hapa atakuwa yupo. Huyu aungane na wale na wenzake, ashauriane na wenzake ili hayo mambo yaende vizuri, ni mtu mmoja mzuri sana nadhani anakuwa ni Katibu Mtendaji si ndio ana cheo fulani pale, nina imani kubwa kwamba hili jambo wataweze kulifanya vile ambavyo inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linawaumiza sana ni suala zima la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. *Volume four* ukurasa wa 24, *Poverty Eradication Department, subvote 81,000, item 6508* hapa wameweka. Wanaweka nini humu na hawatekelezi, huku ni kudanganyana bure. Najua ikifika wakati wanakuja kifungu hicho kimeafikiwa na ni cha mwisho kifungu hicho kimeafikiwa ohh, waoo, hamna kitu, hawatoi fedha wanadanganya, wananchi wanasubiri kwa muda mrefu na hawajatoa hizi fedha, wanaandika kwenye vitabu, lakini hakuna kitu, tatizo nini, bora muwaambie tu kwamba, ni kweli hizi fedha hazipatikani sababu ni moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Spika, ni ahadi kweli ya Mheshimiwa Rais, akishasema jambo, jambo hilo ni lazima litekelezwe, Mheshimiwa Waziri tatizo lake nini, kama hana vyanzo hata juzi Kamati ya Gesi imesema kuna mabilioni mengine hayo chukua fanyieni kazi, mbali ukiachia leo uvuvi wa bahari Kuu, nawashangaa.

Mheshimiwa Spika, nawauliza Serikali kuna nini huko mwaka huu, hayo ndiyo maisha, mbaya mzunguko wa fedha hakuna, kila tunaposema tuna vyanzo fulani wachukue vyanzo fulani wavifanyie kazi hawataki, sasa wanataka ushauri kutoka wapi na sisi ndio Wabunge wao, tena Wabunge, Wabunge kweli, shauri yenu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, randama hii hapa, wameeleza katika hii randama, ukurasa wa 119 mpaka 120, wameweka hii maelezo yao waliweka hapa, naombeni sana sisi ni Wabunge waelewa sana, wasitufanye hivi, Wabunge wote ni waelewa sana humu, waandae mazingira basi hizi fedha milioni 50 kwa kila kijiji wametenga bilioni 60, hizi kila mwaka wanatenga, lakini fedha hizi wananchi wanalalamika Wabunge wanasema labda jambo hili limewashinda Waheshimiwa Wabunge, tunawaambia lakini Serikali sio wasikivu, Serikali haitaki kusikia.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa hili tena leo Ramadhani kumi la *maghfira* hili, anajua Mheshimiwa Ashatu nazungumza hivi taratibu sana, kama ingekuwa miezi mingine ningesema maneno mengine, wajitahidi sana waandae mazingira hizi fedha zitolewe, hali ni ngumu sana .

Mheshimiwa Spika, nimalizie jambo moja dogo, kwani kuna tatizo gani katika hali ya maisha wanayoiona Watanzania na mzunguko wa pesa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa deni bado himilivu, tuendelee kukopa, sawa na utalam wake mimi siko huko, lakini kwa nini kwenye hotuba yake ya mwaka jana alituambia hapa kwamba nia yake ni kuandaa mazingira, wale wanaokula mlo mmoja kutoka asilimia 9.7 sasa waende mpaka asilimia 5.5, hotuba yake ya mwaka jana hiyo, ni maelezo yake, lakini mbona wanaokula mlo mmoja wameongezeka, umaskini umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, sasa alichokisema mwaka jana hajakisimamia Mheshimiwa Waziri, sisemi kama yeye ni mwongo lakini hakusema kweli, simwambii kwamba mwongo hapana, siwezi na Ramadhani hii, lakini hakusema kweli kwa sababu haya ni maandishi yake kwamba tutahakikisha katika bajeti zinazofuata wanaokula mlo mmoja wataondoka katika asilimia 9.7 mpaka asilimia tano, leo maskini wameongezeka, hiyo asilimia aliyosema haipo, wanaokula mlo mmoja wengi, wengine hakuna mlo, maisha magumu, hali mbaya kupita kiasi, tukisema kuna vyanzo chukueni...
(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Masoud wewe takwimu yako unaitoa wapi, ya Waziri hiyo ya kwako wewe kwamba umaskini umeongezeka.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, kwa wananchi, nenda Kongwa, nenda Mpwapwa, nenda Dar es Salaam , nenda Mbeya, nenda Iringa kusanya watu upate hiyo, tunaangalia takwimu yake ambayo ametupa awamu iliyopita, sisemi kwamba ni muongo lakini jambo limemshinda fedha ziko wapi, tatizo nini? Hamueleweki! Nawashangaa mwaka huu! Kama kweli Serikali sikivu andaeni mazingira basi msikie.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya fedha ni tegemeo kubwa sana kupita kiasi, Watanzania wote wako na sikio kuangalia Wizara ya Fedha itafanya nini kuboresha maisha ya Watanzania. Leo maisha ya Watanzania yamekuwa ni ombaomba walio wengi, kila siku umaskini unaongezeka, uchumi unakua umaskini unaongezeka nchi gani duniani hakuna uwiano baada ya uchumi kuongezeka...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Umaskini umeongezeka na uchumi unaongezeka...

SPIKA: Mheshimiwa Masoud tayari muda hauko upande.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mwaka huu, haya tutawaona! (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muwe mna-*rely* kwenye *statistics*, yuko mama wa *National Bureau of Statistics* hapo anatusikiliza, ukisema hiki kimeongezeka unasema kufuatana na tafiti iliyofanywa na taasisi fulani, hii nimeitoa kwenye *reference* fulani. Hata hivyo tunakushukuru Mheshimiwa Masoud.

Sasa namwita Mheshimiwa David Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa lugha nyepesi kabisa adui namba moja wa maendeleo ya Taifa hili ni Wizara ya Fedha na Mipango. Adui namba moja na nina sababu, sababu namba moja Wizara ya Fedha inashindwa kutoa fedha ambazo zipo kisheria namba moja.

Mheshimiwa Spika, hili nalisema, nenda kwenye ripoti ya Mkaguzi, angalia fedha ambazo Wizara kwa kupitia *TRA* wamekusanya na ambazo wamepeleka na zile ambazo hawajapeleka, hawapeleki fedha. Leo ukienda kuangalia watu wa korosho wanalalamika, wamekuja watu wa Bodi ya Korosho kwetu wamelalamika juu ya Wizara ya Fedha wamekusanya bilioni 91, wamepelekewa bilioni 10, fedha yao halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *railway development levy*, hakuna hata senti iliyopelekwa kule, angalia kila kifungu Wizara ya Fedha wana sababu moja tu wanasema siku hizi uhakiki, yaani Serikali hiyo moja kigezo chao ni uhakiki na ndio kichaka cha kujifichia kutokupeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hapa wanakuja wanalia fedha hakuna na fedha zao ambazo zipo kisheria, wao jukumu lao ni kuchukua, kukusanya na kurudisha kule, hawafanyi wanalitakia mema Taifa hili, *the answer is no*, hawataki mema Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya maendeleo angalia kilimo chini ya asilimia 10, miradi ya maendeleo; viwanda ambavyo ndio tunahubiri, Wizara ya Viwanda na Biashara asilimia tisa, leo uchumi wa Taifa ambao tunalia kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda

unapeleka asilimia tisa na Wizara hawawezi kuleta majibu hawa na tunawaona. Pia wana sababu za ajabu, maagizo kutoka juu, maagizo gani, yaani huko juu ni wapi mbinguni yaani ambako sisi kama Taifa hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, hivyo tuulizane swali dogo, unapoagizwa kutoka juu, hivyo mtu anayekuagiza kuvunja sheria *you need to know one thing*. Leo mpo ninyi, kesho utawala utakuja awamu nyingine, itakuja Awamu ya Sita atakayekuwa *responsible* ni ninyi Mawaziri kwa sababu sisi hatutamgusa Mheshimiwa Rais ana kinga Mheshimiwa Rais yoyote yule awe ni Mheshimiwa Dkt. Magufuli, afanye chochote kibaya ana kinga, ninyi hamna kinga tutawachukulia hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa haya ndio ambayo yanapelekea haya madudu kuendelea kufanyika na tumekuwa tukishuhudia kila wakati, sasa kuna maamuzi ambayo Wizara inayafanya ambayo sisi kama Taifa ndiyo tunaingia hasara, kwa mfano unajua unapojenga reli ya *standard gauge* ni jambo jema na sisi kama wananchi hatupingiki tunakubaliana na hilo jambo, lakini unapoamua kukopa mkopo wa kibiashara kwenda kuhudumia reli ambayo malipo yake ni baada ya miaka 20 ni kuliingizia Taifa hasara, yaani unatumia *current asset to finance the long term liability*, ni nini ninachokisema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikopo ya mabenki wanakupa muda wa *grace period* ya miezi sita, mradi wako hujakamilika unaanza kulipa fedha, lakini ukitumia *concessional loan* ni watu wanakwenda kwenye mradi, wanatekeleza mradi, mradi unakwisha, baada ya mradi kuisha unapewa muda fulani miaka mitatu, baada ya hapo ndio unaenda kuwalipa. Sasa leo hii miradi ni mema Kwa Taifa lakini tutaanza kulipa kabla miradi haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 20 ndio mradi ile *pay back period* yake kuanza kutoa faida ndio unaanza

kuiona, unajua matokeo yake ni nini? Hakuna maendeleo yatakayoendelea kufanyika, ndio maana leo tukija humu ndani kilimo wanalia, afya wanalia, elimu wanalia, maji wanalia, hakuna mradi unaofanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa haya wanaosimamia ni Wizara ya Fedha, sijawahi kuona Wizara ambayo inashindwa kuelewa kama Wizara ya Fedha na hii inabidi uwe mkali sana, bila kuisimamia Wizara ya Fedha kupeleka fedha hizi zote tunazosema hapa ni ngonjera, kwa sababu kila kilichoandikwa mwisho wa siku lazima kitafsiriwe na fedha iende pale. wanatamka mapato yameongezeka, sisi tunashangilia huko mtaani, haya tuonyesheni hela basi, hazionekani.

Mheshimiwa Spika, ILeo unakwenda angalia tu mfano mdogo tu deni la Taifa ndani ya miezi 12 wamekopa trilioni saba, hilo deni limeingia kwenye deni la Serikali, trilioni saba, haya waambieni hili deni la trilioni saba hela zake basi tuonyesheni na zile mlizokusanya ndani tuonyesheni vilevile tuone hii miradi na utekelezaji wake mnafanyaje wanakwambia tu hili ni himilivu kwa asilimia 34.4 ukomo wetu ni 56%, hawazungumzii *tax to GDP* yaani makusanyo ya kodi *against* pato la Taifa, tuko kwenye 14.5%, ndio ambayo tuko sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa duniani kote siku hizi watu walishaacha kutumia mfumo wa *debt to GDP* siku hizi watu wanatumia mfumo wa kodi kwa pato ghafi la Taifa. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Silinde hivi kweli unamfundisha Dkt. Mpango, uchumi?

MHE. DAVID E. SILINDE: Namfundisha vizuri!

SPIKA: Endelea bwana. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana umenielewa. Tunakumbushana, ni Mwalimu lakini ni mwananadharia. Mimi nayaishi haya maisha *practically*. Hii ndiyo changamoto inayo-face nchi. Maprofesa wengi wamefeli kwenye uongozi duaniani kote walipokabidhiwa. Kwa sababu hivi vitu, unajua kuzungumza na kutekeleza ni vitu viwili tofauti. Sasa hilo tumezungumza, tunaona hali halisi. Sasa kuna mambo mengi ambayo hawa wanasimamia, leo wanasimamia rufaa za kodi, angalia kule, kuna rufaa kibao; lakini wanasema ili tumsikilize mtu tupokee ombi lake lazima ulipe moja ya tatu ya kodi. Ndiyo kazi ya Wizara ya Fedha, yaani ni kukandamiza.

Mheshimiwa Spika, angalia mikakati yao Wizara ya Fedha. Mikakati yote ni kodi, kodi, ongezeko la kodi. Hakuna mahali popote wanayoweza kukuonesha namna watakavyozalisha ama namna ya watakavyotengeza mkakati wa wale watu wetu kwenda kulipa kodi. Hawa ndio wanaosimamia, sisi tunawahoji kila siku. Kuna majibu mengine tunayavumilia, lakini kiukweli wanataka kuvuna mahali ambapo hajawapanda, ndiyo kitu kibaya sana ambacho hawa watu wanacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo wanalo, ni kutokutaka kuelewa. Kama walichokipanga wao wameshakupanga, maelezo yote tutakayotoa ndani ya Bunge hakuna jambo lolote watakalolisikia. Hilo ndilo tatizo. Wizara ya Fedha ina kiburi cha hali ya juu, sijawahi kuona katika nchi hii!

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa hapa awali, wamejikita kwenye fedha, kwenye mipango ni kama hamna. Hiyo ndiyo imekuwa changamoto katika nchi hii kwa miaka mingi. Yaani inapofika suala la mipango, waulize hawa Mipango, ndiyo hii mipango inakuja mambo mapya. CAG ameshatoa mapendekezo mengine, wao wenyewe wanayakimbia. Haya yote ni kwa sababu wanashindwa kutusikiliza, wanashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Spika, ubaya sana kwenye hizi nchi, inafika mahali watu wanawaachia haya nendeni basi

tuwaone, mtafikia wapi? Mtashindwa! Sasa ninachofahamu, Mheshimiwa Rais anahitaji kushauriwa vizuri. Yeye ni binadamu, hata kama kuna wakati ana-*push* jambo ukimwelewesha usiku atalala peke yake, atasema lakini lile jambo Mheshimiwa Waziri Mpango alinimbia kweli. Sasa ile akikwambia tu “ nimesema kuanzia leo, toa hela hizi peleka huku.” Unasema sawa mzee. Hakuna Taifa la namna hiyo! Lazima umwambie hapana Mheshimiwa Rais. Nitatekeleza hilo jambo lako, lakini lazima tufuate utaratibu. Ni mambo ya kawaida. Hata Mbinguni kule kwa Mungu ili uende Mbinguni lazima ufuata utaratibu, hakuna dunia inaendeshwa bila utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo yaliyotufikisha leo hapa. Ni kwa sababu mambo mengi na fedha nyingi, zinakwenda bila utaratibu. Mwisho wa siku wanasema mali bila daftari huishia bila habari. Kwamba unaweza ukakusanya mali nyingi, lakini kama unashindwa kurekodi, kuwa na mipango, yaani hutafanya kitu chochote. Miaka mitano; imebaki miwili, itakwisha, mtakuja na *the same story*. Mtaishia kupiga kelele tu kwamba tumetekeleza; tuonesheni mlíchokitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 50 kila kijiji, ipo kwenye rekodi hapa; leo mwaka wa wangapi? Wa tatu huu, ndiyo bajeti ya tatu; tumebakiwa na bajeti mbili tu. Wanatenga, lakini hawajapeleka hata shilingi mia. Ipo kwenye taarifa yao. Walitenga shilingi bilioni 59, wakasema tunakwenda kwenye *pilot study*; hawajapeleka hata shilingi mia. Mwaka 2017 wakatenga shilingi bilioni 60, hawajapeleka hata shilingi mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tukija tukiwahoji tunaonekana tunakosea, lakini ni kweli hizi takwimu wameziandika wenyewe; wanaotudanganya ni wao wenyewe; lakini yote hii ni kwa sababu wanaamini sisi hatuelewi. Sisi tunajua, tunaweza kuwa katika ujinga wetu tunaelewa kidogo, lakini kwenye hiki cha ujinga kinatoka kwa wananchi. Wewe unafika Jimboni mtu anakuuliza, Mheshimiwa Mbunge shilingi milioni 50 hazijaja hapa kwa

sababu wewe Mbunge ni mzembe, lakini unajua kabisa ni kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kasema hela itakuja. Namwuliza hela iko wapi? Anakwambia hela itakapopatikana. Si mmetuelezaa hela zipo nyingi huku! Sasa hilo ndiyo tatizo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Rehani.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nataka nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Silinde amesema kwamba Serikali inatumia kichaka cha uhakiki kama kujificha. Kwa faida ya Bunge, mimi *professional* yangu ni Mtawala. Elimu ya juu nilisoma Utawala na ya juu zaidi nikasoma Sheria za Upatanishi na Usuluhishi. Kwa hiyo, migogoro hapa ni kaburi lake.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uhakiki wa Watumishi Serikalini, hata wale wanaoenda kuhakikiwa wanajiandaa jinsi ya kukwepa ule uhakiki. Kwa hiyo, mnaweza ukazungumza uhakiki kwamba Serikali haimalizi uhakiki, mkumbuke hata wale wanaoenda kuhakikiwa na wale waliowaingiza wale watumishi hewa, kwa sababu wanajua wakigundulika na wenyewe watakuwa matatani, kwa hiyo wanajiandaa jinsi gani ya kukwepa huo uhakiki. Kwa hiyo, wasiituhukumu Serikali tu wakasema uhakiki hauishi. Sisi watawala tunaelewa uhakiki maana yake ni nini na changamoto zake ni zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili ambalo nilikuwa natamani sana kulizungumza leo kwa kupata nafasi hii, nchi yetu mwanzo ilikuwa nchi ya wakulima, wafanyakazi

na wafanyabiashara. Kuna kundi lingine limeongezeka kubwa sana. Sasa hivi nchi yetu ni ya wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wacheza kamari. Bahati nzuri imezungumzwa, sasa hivi wanafunzi wote wa Vyuo Vikuu wakipata mikopo wanajazana kwenye vituo vya kucheza kamari.

Mheshimiwa Spika, pia wazee wetu wakipata *pension* wanaenda kucheza kamari; wake zetu, zamani sisi enzi zetu wakati tunaoa, unaambiwa ili uwe na maisha mazuri, ukipata kahela kako mpelekee mkeo akatunze. Ukimpelekea mke, ukija kuchunguza simu zake, unakuta meseji za Biko na Tatu Mzuka. Madereva wa Bodaboda wote, yaani vijana wote tunavyozungumza sasa hivi, wote wanacheza kamari. Hili ni janga la Taifa. *Gaming Board* watafute namna gani ya kuliratibu.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kamari ni makubwa kuliko biashara nyingine. Rafiki yangu Mheshimwia Musukuma hapa alikuja na zao lake mbadala kwa ajili ya kutuletea uchumi tukalikataa, tukasema lina madhara, lakini ninavyokwambia kamari madhara yake ni makubwa kuliko bangi au kuliko hata viroba. Kwa hiyo, tutafute utaratibu wa kuendesha kamari, lakini siyo kama sasa hivi inavyoenda.

Mheshimiwa Spika, labda tu kwa watu ambao hawajui madhara ya kamari; kwanza, imevunja nguvu kazi za nchi yetu. Zamani ilikuwa ukienda vijijini unawakuta vijana wanacheza *pool table*. Sasa hivi *pool table* haipo, vijana wote kwenye *betting* maana kamari zenyewe ziko nyingi, zimeongezeka, mara kuna Tatu Mzuka, Biko, sijui Mkeka *Bet*, sijui nini *bet*, yaani ziko nyingi kweli kweli na zinaongezeka kwa kasi, umeona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nguvu kazi ya vijana imepotea. Vijana wote wanaamini watakuwa matajiri, kwa sababu matangazo yale ambayo tumeyaruhusu kiholela sasa hivi inawafanya vijana wengi wawe na tama. Mtu anasema nitapata kesho, nitapata kesho. Kwa hiyo, akipata kihela kidogo, kwenye kamari.

Mheshimiwa Spika, madhara mengine ni *addictive*. Mtu yeyote anayecheza kamari hawezi kuacha. Nao walivyokuwa wataalam, anakupa Sh.5,000/= leo umeshinda. Ukishinda Sh.5,000/= hiyo huwezi kuacha, hata ucheze shilingi milioni 20 hutaacha. Kwa hiyo, inasababisha hiyo *addictive*, wenyewe wanaita uteja.

Mheshimiwa Spika, lingine madeni. Watu sasa hivi wanaenda kukopa kwenye *Vicoba* ili wacheze kamari. Kwa hiyo, inasababisha Taifa la watu kuwa na madeni. Ndiyo maana hata ukienda kwenye *Vicoba* mikopo hailipiki, watu wanakopa kwa ajili ya kwenda kuchezea kamari. Hivyo, malengo ya Taifa letu yanapotea kwa sababu wengi wanaweka malengo kwa kutegemea kamari.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga ukiona kuna Mbunge yeyote anacheza kamari, tupate jina tumpeleke maadili. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Sawasawa. (*Kicheko*)

SPIKA: Endelea Mheshimiwa.

MHE. GOODLUCK A MLINGA: Kwa hiyo, ndiyo hivyo. Ninachoomba *Gaming Board* watafute utaratibu wa kuendesha haya mazoezi ya kamari, lakini siyo kwa mfumo huu. Watafute mfumo mwingine. Wametoa matangazo; kuna tangazo wamelitoa zuri, lakini hilo tangazo linapita kwa watu kiasi gani? Maana yake wanasema, usitumie fedha yenye malengo mengine kuchezea kamari. Hebu niwaulize, leo hii Tanzania nani ambaye ana pesa ambayo haina malengo imekaa tu? Kila pesa tunayoipata ina shughuli, ada za shule, nini na vitu vingine, lakini watu wanaishia kwenye kamari.

Mheshimiwa Spika, kuna mwanafunzi mmoja alijinyonga juzi juzi hapa kwa sababu alitumia pesa ya ada kwenye kamari na akaliwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wakati ana *wind-up* atuambie ni namna gani *Gaming Board* watatafuta utaratibu wa kuendesha kamari bila kusababisha matatizo ambayo yanatokea sasa hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, wakati Serikali yetu ya Awamu ya Tano inaingia madarakani, tulikubaliana Serikali nzima tubane matumizi yasiyo na tija ili hiyo pesa tuipeleke sehemu nyingine ya maendeleo. Kweli tulifuta safari za nje kama Bunge, sasa hivi hatuendi nje. Taasisi za Serikali zilitoa fedha zao kutoka kwenye mabenki ya biashara wakapeleka Benki Kuu. Pia pakatolewa maelekezo kuwa tutumie huduma zinazozalishwa na taasisi za Serikali. Hata matibabu ya nje yalizuliwa. Mpaka mtu aende kutibiwa nje inatakiwa utaratibu mrefu na ionekane kuna haja ya muhimu kabisa huyu mtu kwenda kutibiwa nje.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea, Benki Kuu ya Tanzania ndiyo taasisi inayotumia fedha nyingi katika matibabu bila msingi wowote. *BoT* Mfanyakazi akiwa na mafua anaenda kutibiwa Uingereza au India. Wanatumia fedha nyingi na wamesahau kuwa hizi fedha ni za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zetu za Serikali zimewekewa utaratibu maalum kwa ajili ya kupatiwa matibabu. Tunaitumia *NHIF*, hata Bunge tulikuwa tunatumia *Private Company* sasa hivi tumeingia *NHIF*, *BoT* wanatumia *Private Insurance* gharama ya matibabu ambayo wangeitumia *NHIF* shilingi bilioni moja wanatumia shilingi bilioni 12 kwa mwaka. Angalia ufsadi wa hali ya juu uliopo. Shilingi bilioni moja kwa shilingi bilioni 12 kwa sababu watu wana maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, wanasema wao hawawezi kwenda *NHIF* kwa sababu haina matibabu nje ya nchi. Sasa naomba niulize, wao wanasema taasisi yao ni nyeti, Usalama wa Taifa wako *NHIF*, Bunge tuko *NHIF*, *PCCB* wako *NHIF*. Mke wa Rais aliugua, alilazwa Muhimbili, lakini *BoT* hawakubali. Wanasema wao taasisi yao ni nyeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tulikubali hadi matezi dume tulipimwa kwenye *Dispensary* ya Bunge hapa hatukuona tatizo, lakini wao mtu akiugua kidogo wanataka kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, naomba ulisimamie hili. Kuna ufisadi mkubwa katika mchakato huu wa *BoT* kwenda kupata matibabu kwa kutumia *Private Insurance*.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri mpaka atakapokuja na majibu ya haya niliyoyatoa. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, endapo Mheshimiwa Mlinga unachokisema ni kweli, kwamba wametoka kwenye *one billion* sasa watumia shilingi bilioni 12 hawa *BoT*, nakuagiza Mwenyekiti wa *PIC* kuiita Bodi ya *BoT* ndani ya wiki moja na *Management* yake, wajieleze kwa nini wanafanya matumizi ya aina hiyo kwenu? Maana yake, ni kwamba baada ya hiyo wiki moja mtaripoti kwangu kwamba ni kitu gani kinachondelea. Hatuwezi kufanya mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Salum Rehani, hayupo eeh? Mheshimiwa Mendrad Kigola.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza nianze kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imeweza kufanya kazi kwa ufanisi mzuri sana. Bahati nzuri taarifa tuliyoisoma ipo wazi. Pale walipo-*perform* vizuri wanasema na pale wanapojua hawaja-*perform* wanasema. Huo ndiyo tunasema uwazi. Ndiyo maana kila mmoja anasema labda kwenye kilimo amepeleka asilimia kadhaa, ipo wazi; kuliko asingesema vitu ambavyo ame-*perform*. Kwa hiyo, nimempongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa uwazi huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Wizara ya Fedha ndiyo moyo wa Serikali, ndio moyo wa maendeleo ya nchi hii na ndiyo inayo-*control* mapato yote ya nchi hii. Ili Serikali i-*perform* vizuri, lazima Wizara ya Fedha ikae vizuri. Tunajua kwamba ili Serikali ifanye vizuri lazima makusanyo ya kodi yakae vizuri. Kuna Mbunge mmoja alisema kwamba Wizara hii inataja kodi tu, lazima itaje kodi tu kwa sababu isipotaja kodi haiwezi kupata fedha ya kuendesha shughuli za Kiserikali.

Kwa hiyo, nasema waendeleo kutaja kodi tu ili na wananchi waelewe kwamba lazima wananchi walipe kodi ili Serikali ifanye vizuri kwenye miradi ambayo tunahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuangalia, wameeleza vizuri kwamba wanataka kupunguza umaskini. Nataka nijikite vizuri sana kwenye kupunguza umaskini. Wanataka wafanye ufuatiliaji kwenye vijiji ili waangalie umaskini umepungua *percent* ngapi? Tuna changamoto nyingi sana vijijini.

Mheshimiwa Spika, nataka niombe Wizara ya Fedha, lazima isimamie vizuri kuhakikisha kwamba mahitaji ya wananchi kule vijijini kweli yanapungua. Nataka nitoe mfano mdogo tu, tukisema kupunguza umaskini kwa wananchi, lazima tuhakikishe miradi ile inayolenga wananchi inafanyika kusanifu na kwa bei inayojulikana. Wengine wanasema, Serikali isifanye uhakiki, wanasema kila siku ni kuhakiki. Nasema kuhakiki kuongezeke kwa sasabu unaweza ukaona Serikali imelipa fedha nyingi sana lakini mradi wenyewe hauonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Serikali ikawa inatoa fedha nyingi, halafu mradi ule hauonekani. Kwa mfano, wanachimba kisima cha maji vijijini, wananchi hawajapata maji, lakini fedha zinaonekana zimetumika pale. Hii haitakubalika hata siku moja. Zamani miaka mitano iliyopita, unaweza ukaona wananchi wanahitaji maji pale kijijini, wanasema kwamba Mkandarasi ametumwa na Serikali, labda Wizara akachimbe kisima cha maji. Maji hajapata, unaenda kuangalia gharama kubwa pale zimetumika na wananchi hawajapata maji. Hii kweli itakubalika? Hii haiwezi kukubalika. Lazima tuone *impact*. Kama fedha zimetumika kwa ajili ya kuchimba kisima, basi wananchi wapate maji pale. Hilo lazima Serikali ihakikishe inafuatilia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto kubwa sana. Kwa mfano miradi ya maji. Naiomba Serikali, miradi ya maji mpaka sasa hivi kama tunapunguza umaskini, basi tupunguze kwenye mradi ya maji, tuhakikishe wananchi wetu

wote wamepata maji. Kuna Wakandarasi wengine bado wanadai fedha hazijalipwa. Kwa mfano, hata kwenye Jimbo langu, kuna kata moja ya Sawala, Mkandarasi sasa hivi kuna miezi sita alishasaini mikataba lakini mpaka leo hajapata fedha na mradi ule umesimama na wananchi wanataka *impact* ya maji. Kama tunapunguza umaskini, basi tuwapelekee maji.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingine wananchi wanatembea kwa mguu kilomita nne au kilomita tatu wanatafuta maji. Sasa tusipokijita vizuri, hata hii *perception* ya kusema tunapunguza umaskini, tutakuwa hatujapunguza umaskini. Wananchi wanataka wapate maji. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wananchi wanataka kupata maji. Miradi ile ya maji ambayo tumetenga kwenye bajeti, basi wapeleke tuhakikishe inafanyika kwa ufanisi kama ilivyopangwa ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kwenye makusanyo. Serikali ijitahidi kufanya makusanyo. Lazima kwanza itengeneze urafiki na wafanyabiashara, *TRA* watoe elimu ya kutosha ili kuhakikisha kwamba kila mtu anayelipa kodi asione kama adhabu, aone ni wajibu wake kulipa kodi. Ili ajue kwamba ni wajibu wake kulipa kodi, lazima utaratibu wa ulipaji kodi uwe mzuri. Kuna *point* moja nimeipenda sana kwamba Wizara ya Fedha kushirikiana na *TRA* wanataka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila mtu anayelipa kodi asikwepe. Hiyo nimeipenda, huo ni mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba kila mtu analipa kodi, hiyo ni njia mojawapo. Hata hivyo, lazima tuhakikishe kwamba wale walipa kodi, tunajenga urafiki nao, tunawapa elimu, ili kila mmoja nayelipa kodi asione kama adhabu.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya fedha zile zinazopelekwa kwenye Halmashauri za maendeleo. Naishauri Serikali kwa sababu wanapeleka *quarterly*, sijajua *system* ya kupeleka, lakini fedha ziende kwa muda unaotakiwa, *on time*. Unaweza ukaona Mkandarasi ameingia mkataba labda wa mwaka mmoja. Usipopeleka fedha *on time* kama mkataba unavyosema, matokeo yake ukichelewesha fedha,

inatokea Mkandarasi baadaye anaanza kuidai Serikali, baadaye ule mradi bei inaongezeka, Serikali inaanza kulipa riba.

Mheshimiwa Spika, mradi wa shilingi bilioni moja baadaye inakuja kusomeka hata shilingi bilioni tano. Kwa hiyo, naiomba Serikali ipeleke fedha kwenye miradi mikubwa, kwenye Halmashauri kwa muda uliopangwa. Hii itasaidia sana kuhakikisha miradi ile inakwisha *on time*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nataka niipongeze Serikali kwenye *point* moja. Serikali kufikiri miradi mikubwa ya kimaendeleo ndani ya nchi yetu ndicho kinachotakiwa. Hatuwezi kuwa tunafikiri miradi midogo midogo tu halafu tunasema nchi itafikia uchumi wa kati, haiwezekani hata siku moja. Lazima ifikiri miradi mikubwa ambayo inajenga uchumi ndani ya nchi yetu. Kwa mfano, ule mradi wa umeme wa Rufiji ni mradi ambao utatutoa katika hali ya umaskini. Kwa sababu ule umeme tunaweza kuuza hata nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Malawi watanunua, Zambia watanunua na nchi nyingine za *East Africa* wanaweza wakanunua umeme kutoka pale. Ndiyo nchi yetu itapata fedha za kigeni, ndiyo tutafikia uchumi wa kati. Ukisema kwamba unataka kufikia uchumi wa kati, wewe una *plan* kulimalima mboga, bustani na kadhalika, uchumi wa kati utaufikia wapi? Lazima tuwe na miradi ya kimkakati ambayo inaleta uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *point* nyingine ambayo nimeiona, Serikali kufikiria kujenga reli, hiyo ni *point* kubwa ana katika nchi zinazoendelea. Hata ukienda Ulaya utakuta kuna reli zimejengwa *standard*. Kwa mfano, sasa hivi kuna *standard gauge*, ni kitu cha msingi sana. Kwa hiyo, nataka niwaambie, kama tuna-*plan* uchumi, lazima tufikiri vitu vya kiuchumi ambavyo vinaleta hela kubwa ili uchumi wa kati ufikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengine wanakatisha tamaa, wanasema Serikali sijui haifanyi kazi. Sasa hivi

tunaingia kwenye vitu vikubwa ambavyo ni pigo kubwa kwa uchumi ili kuinua uchumi wa nchi yetu. Tukitaka kupata fedha nyingi, lazima tufikiri vitu ambavyo vinaweza vikatuingizia. Hata wawekezaji wanapokuja, wanauliza vitu vya msingi. Kwa mfano, atauliza barabara, miundombinu ya umeme, maji, hospitali; wafanyakazi wakiugua wanatibiwa wapi? Hivyo ndivyo vitu wanavyouliza wawekezaji. Wewe huna barabara, umeme, maji wala hospitali halafu unasema unatafuta mwekezaji, utampata wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inapobuni vitu vya msingi lazima tui-*support* na sisi Waheshimiwa Wabunge. Bila kui-*support* Serikali kwa vitu vya msingi hatutaendelea hata siku moja. Kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akaze buti, afikiri vitu vya msingi ili nchi yetu iweze kusonga mbele. Hatuwezi kuwa tunarudi nyuma kila siku, Waheshimiwa Wabunge tauliza maswali madogo madogo ambayo Serikali inaweza kutatua kwa muda mfupi sana. Kwa hiyo, tunafuta maswali sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, hatupendi sisi Wabunge tukifika hapa tauliza masuala ya maji, tauliza kuhusu barabara ndogo ndogo, zahanati ndogo ndogo; Serikali inakuwa imeshatatua. Sasa ili kutatua lazima tujifunge mkanda. Bila kujifunga mkanda, kujibana vizuri hatuwezi kuendelea hata siku moja. Lazima Serikali ibane vizuri lakini ilete maendeleo, tuone *impact*. Siyo Serikali ibane halafu tuwe na njaa, hapana. Ubane vizuri, tunakula lakini tuhakikishe kila mmoja anafanya kazi kwa nafasi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la utendaji kazi. Unaweza ukaona *document* moja inapelekwa kwenye ofisi, inazunguka miezi mitatu. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *document* isizunguke. Mtu anatoka Halmashauri kule anafuatilia *document* hapa, inachukua siku mbili au tatu. Hii haiwezekani, unaweza ukaona gharama za ufuatiliaji wa *document*, inataka kukaribia mradi unaofuatiliwa. Hii inakuwa ni *system* mbaya sana. Kwa nini tusitafute *system*, mtu yuko Halmashauri kule, ana-*lodge document* yake mtaalam huko anasoma kwenye *computer*, analipa

malipo, *simple*. Anaona hiki kipande nimeelezwa vizuri, ana *document...* (*Hapa microphone ilikata*)

Muda umeisha?

MBUNGE FULANI: Aah, endelea.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Niendeleee, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu yuko Halmashauri kule ana-*search* tu *document* kwenye *computer*, mtaalam huku anasoma. Akishasoma ana-*reply within the minute*, yule kule atakuwa ameshaiona. Akishaiona, basi inajibiwa. Sasa mtu anaanza kufuatilia wiki moja, mbili, anafuatilia *document*. Hii inarudisha nyuma maendeleo. Kwa hiyo, nataka nihamashe wafanyakazi, hasa wale wa Idara ya Fedha, kwenye hili wasimame vizuri, wasilimbikize kazi ambazo hazina msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni wastaafu. Kuna Mheshimiwa Mbunge aliuliza asubuhi kwamba wastaafu wao bado wanadai, wanalipwa kiasi kidogo sana. Wale wastaafu ni wa kuwaheshimu, wamefanya kazi nyingi sana mpaka sasa hivi nchi imefika hapa. Wewe mtu amestaafu, alifanya kazi nzuri, kwa nini usimlipi haki yake vizuri? Lazima tuhakikishe wale wazee ambao na wenyewe wanatuombea na sisi tufanye kazi vizuri, tuwalipe stahili zao kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mstaafu unamlipa Sh.50,000/=. Kama sheria inasema alipwe Sh.100,000/=:, mlipi Sh.100,000/= yake. Kama inasema Sh.200,000/= mlipi Sh.200,000/= yake, sasa mzee amestaafu anafuatilia mafao kuna watu wengine hawajapata mafao mpaka leo inachukua miezi mitatu na zaidi na mtu anastaafu yuko kwenye *system*. Kwa nini anastaafu leo, kesho humlipi hela yake? Mtu yuko kijijini, kwa mfano yuko Mufindi, afuatilie Dodoma au Dar es Salaam wakati *system* inasoma. Kwa nini asilipwe *on time*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono Serikali, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mendrad Kigola. Baada ya muda atafuata Mheshimiwa Deo Sanga. Kabla ya Mheshimiwa Deo Sanga, nimekuona Mwenyekiti wa PAC sasa umeshaingia. Mwenyekiti wa PAC, ametoka tena! Basi wajumbe wa PAC mpo hapa, mpo si ndiyo?

MBUNGE FULANI: *Yes!*

SPIKA: Nimesema Kamati yenu ifanye kazi kabla ya Jumatatu, kuanzia keshokutwa Jumatano mna-*ample time*, Alhamisi, Ijumaa mwite Bodi ya BoT na Senior Management yake, kabla ya kukaa na BoT na Senior Management Team ya BoT muwe mmekaa na Mheshimiwa Mlinga kuhusu hili jambo aliloeleza na muwe mmekaa na National Health Insurance Fund, mmenielewa? Mnakaa na Mheshimiwa Mlinga, mnakaa na NHIF halafu sasa ndiyo mnawaita hawa BoT.

Baada ya kufanya kazi yote hiyo, haraka sana mtaniletea majibu ya kazi yenu ili niweze kumwandikia Mheshimiwa Rais, ili kama wao hawawezi ku-*reverse immediately* baada ya mkataba wao kwisha, tuhakikishe basi mkubwa wa nchi anaingilia kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuwapa fidia wananchi wangu wa Jimbo la Makambako. Nawashukuru sana, kwa dhati kabisa kwa sakafu ya moyo wangu, nawashukuru sana, wamefanya kazi nzuri. Kwa sababu fedha hizi wamezidai kwa muda mrefu, lakini kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais imetekelezwa. Narudia tena kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaposhukuru, kuna ombi tena kuhusu fidia nyingine. Pale Makambako kupitia Wizara ya Ujenzi, wana eneo ambalo waliomba, tuwaombe wananchi kwa ajili ya kujenga *One Stop Centre* katika Kijiji cha Idofili, kilometa tano tu kuingia Mjini Makambako ukitokea barabara ya Iringa. Katika eneo hilo, vile vile kunatakiwa kulipwa fidia ili waanze kujenga *One Stop Centre*. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika hitimisho lake, basi aseme neno ili roho za wananchi wangu wa Jimbo la Makambako waweze kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tuna Liganga na Mchuchuma. Imezungumzwa kwa muda mrefu sana kuhusu uchumi wa Liganga na Mchuchuma. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Fedha, atuambie ni nini kinachokwamisha Liganga na Mchuchuma isitekelezwe au isianze? Kwa hiyo kwenye hitimisho pia nitaomba nipate majibu, tatizo ni kitu gani ambacho kinafanya isianze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumejenga zahanati nyingi sana katika nchi yetu ambayo magofu haya ni mengi ikiwepo Jimbo la Makambako. Makambako tuna zahanati ya vijiji zaidi ya 13 ambazo wananchi, Waheshimiwa Madiwani, Serikali, Mfuko wa Jimbo pamoja na mimi Mbunge wao tumejenga zahanati hizi. Ombi langu kwa Wizara ya Fedha, tuone sasa ni namna gani kwa nchi nzima na kupitia hata Halmashauri yangu ya Makambako tuzimalize zahanati hizi ili zianze kufanya kazi kusogeza huduma kwa wananchi wetu na hasa akinamama na watoto. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wacha!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, jambo lingine napenda sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, nipate majibu hasa ya miradi ya maji 17 nchini ikiwepo na Makambako kwa fedha za kutoka Serikali ya India kwa mkopo nafuu. Maana mpaka sasa hatuelewi kazi hii inaanza lini. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri pia katika miradi hii 17, mmojawapo upo Njombe, Makambako,

Wanging'ombe na mahali pengine Zanzibar kule kuna mradi mmoja nadhani. Basi ni vizuri Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini miradi hii itaanza ili wananchi waweze kupata huduma hii ya maji kama ilivyokusudiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, katika Wizara mbalimbali ambazo tumekuwa tukichangia hapa ndani, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, nami naomba niseme Mheshimiwa Waziri. Namwomba Waziri wa Fedha, fedha hizi za miradi mbalimbali basi ziende kwa wakati ili shughuli zilizopangwa kule kwenye Halmashauri yetu ziweze kwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri, kupanga ni kuchagua. Kuna watu walizungumzia habari ya kununua ndege, habari ya reli, habari ya huo umeme kwamba huo umeme wa kutoka Bonde la Rufiji hauna manufaa na reli haina manufaa. Niseme kwamba Bunge lililopita la mwaka 2010 - 2015, Waheshimiwa Wabunge walisema hapa, ni nchi ya ajabu hii kutokuwa na ndege zake yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Serikali imetii kupitia Mheshimiwa Rais wetu, maana alikuwepo Bungeni hapa wakati ule akiwa Waziri, leo ametii, amenunua ndege katika nchi yetu, tunasema kwa nini amenunua ndege, hazina manufaa. Tukiwa hapa Bunge la mwaka 2010/2015 tulizungumzia hapa, ni nchi gani haina reli? Reli hii ya kati ni reli ambayo imepitwa na wakati, tunataka *standard gauge*. Mheshimiwa Rais ametii, amekubali, sasa ametafuta fedha tunajenga reli ya *standard gauge*. Kupanga ni kuchagua ndugu zangu, ni lazima tusiwe vigeugeu, tuiunge mkono Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulizungumzia hapa kwamba wawekezaji wanashindwa kuja ni kwa sababu umeme hautoshi. Leo ufumbuzi umeme kutoka Bonde la Rufiji, tunasema ule mradi haufai. Sasa tunajikatisa tamaa wenyewe kwa wawekezaji wanaokuja kwamba kumbe umeme kule haupo. Tuunge mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano juu ya mipango mizuri ambayo ipo. Kwa

hiyo, Mheshimiwa Waziri Mpango na Wizara yake na Watendaji wake, achape kazi asonge mbele. Mipango ni mizuri sana. Kwa hiyo, sisi tuko nyuma yako, tunamuunga mkono kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamesema hapa, Mheshimiwa Waziri amekuwa muwazi, ameeleza kila jambo; hili liko hapa, hili bado hivi, hili liko hivi. Tunamuunga mkono, achape kazi, asonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa ajili ya muda, nianze kwa kuunga mkono hoja. Naomba nianze na kipengele cha kwanza kinachogusia rasilimali fedha. Najua kwa kupitia Taarifa ya Kamati, ukurasa wa tatu na wa nne kwa ujumla wake naomba kipengele hiki muhimu tukione kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tatu ule, kipengele hiki kinagusa hilo suala la rasilimali fedha, anasema: "Baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Vile vile kuna mafungu ambayo hayakupewa fedha za kutosha, hivyo kuathiri utendaji kazi wake." Hilo ni eneo la fedha.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, tunaambiwa, kama Wizara ya Fedha na Mipango imeshindwa kuwezesha kwa baadhi ya vifungu vyake kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, itawezaje kuhakikisha mafungu ya Wizara nyingine kupata fedha za kutosha?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rasilimali fedha, najua Wizara hii ni muhimu. Kama yenyewe tu inapata shida

eneo la fedha, vipi kuhusu Wizara nyingine? Naomba hilo liangaliwe sana. Nalisema hilo kwa maana ya suala hilo hilo la rasilimali fedha, kuna huu mradi wa *LGDG* ambapo kwa nia njema kabisa, Serikali ilikuwa imekusudia kwa wakati mmoja kutoa fedha ili kumaliza miradi viporo, lilikuwa ni jambo jema sana. Kwa mfano, kule kwangu kwa kupitia ruzuku y a Serikali, kwa kupitia *TAMISEMI of course*, lakini Wizara ya Fedha iki-*facilitate* hilo jambo, kuna zaidi ya Sh.923,475,000. Fedha hizi zilikuwa zimelenga maeneo ya elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, leo mashaka yangu ni kwamba tunakwenda karibu robo ya mwisho na bahati mbaya fedha hizi ambazo Serikali ilikuwa imekusudia kupeleka huko katika wilaya na maeneo mbalimbali, kwa bajeti hii inayokuja, hakuna sehemu fedha hii inasomeka. Kwa hiyo, nilichokuwa naomba kwa namna yoyote ile, tuhakikishe fedha hizi zimekwenda huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, kuhusu suala la rasilimali fedha, napongeza kwamba kwa kupitia Taarifa ya Kamati kuna maeneo mbalimbali yanazungumzia suala la Wizara kuendelea kufanya mazungumzo ili ama kupunguziwa au kusamehewa madeni. Najua hilo likifanyika, litaendelea kutoa nafasi ya fedha za ndani zinazopakana kugharamia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, najua na nakubaliana na wale wote na Wizara tunaomba Mheshimiwa Waziri alielewe vizuri, nakubaliana na maelezo yaliyotoka kwenye Kamati kwamba ukitaka kukusanya mapato zaidi, ni lazima uwekeze zaidi, siyo kutegemea mapato bila kuwekeza. Kwa hiyo, naendelea kuomba namna yoyote ile ambayo itatusaidia kwenda kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, katika hili niendeleo kushauri, najua ndugu zetu wa *TRA* lengo ni kuhakikisha nchi inapata fedha kwa kupitia kodi. Bado nashauri namna rafiki, najua suala la kudai kodi siyo jambo jepesi, linataka kusukumana, lakini kwa kupitia namna rafiki, bado

inaweza ikamfanya mtoaji wa kodi akaona umuhimu wa kutoa kodi ikienda sambamba na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, eneo la mafao ya wastaafu na mirathi, naona hili katika Taarifa ya Wizara, ukienda ule ukurasa wa 39 na 40, najua kimetengwa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kulipia michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 716.1 sawa na asilimia 71 kilikuwa kimetengwa.

Mheshimiwa Spika, nasema suala hilo ni jema Mheshimiwa kwa maana ya kujali mafao ya wastaafu na mirathi. Niendeleo kuisitiza Mheshimiwa Waziri, wafanyakazi hawa, wastaafu hawa ni uti wa mgongo wa Taifa hili, ni watu ambao waliitumikia nchi hii kwa uzalendo mkubwa. Inapofika sehemu mtu kastaafu, ni wajibu wa Serikali kuendelea kumwanganalia mtu huyu. Nashauri sana hilo liendeleo kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo Mheshimiwa, kuna suala la uhakiki wa madeni ya watumishi na Wakandarasi na Wazabuni pia. Eneo hili la madeni najua mara ya mwisho Serikali ilitoa kiasi cha fedha kwenye kuonesha jitihada za kuanza kupunguza madeni ya wafanyakazi. Nafahamu kwa ujumla wake, katika eneo hili kule Mkoani kwangu Katavi, eneo tu la madeni ya watumishi kuna takribani Sh.501,918,296/= ambapo humo ndani pia tuna madeni yanayowagusa Wazabuni, kuna Watumishi wasiokuwa Walimu na kuna Walimu.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba, ili kuendeleo kutoa tija kwa watu wetu, eneo hili la madeni ya Watumishi na Wazabuni kama ambavyo imesomeka katika maeneo mbalimbali, nilikuwa naomba liendeleo kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, najua kuna suala linazungumziwa kuhusu kupuangua kwa mfumuko wa bei. Kati ya vipengele vilivyoongelewa kuhusu suala la kupungua

kwa mfumuko wa bei, limeongelewa suala la kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula kama baadhi ya vitu vilivyosaidia kupunguza mfumuko wa bei. Narudi kwenye *point* ile ile ya msingi, tunapofarijika na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, mtu wa kawaida ambaye hana elimu ya uchumi, anatamani kuona kumbe kama hili linachangia kwenye kufanya mfumuko wa bei usiwepo lakini yeye aliyeshiriki kuzalisha chakula kwa namna gani anapata moja kwa moja mafao ya yeye kukizalisha chakula. Nikilisema hilo, tafsiri yangu tuendeleo kuangalia namna ambapo huyu mzalishaji wa chakula na yeye anapata manufaa ya moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, najua lugha zote hizi zinazoongelewa hapo, tunaambiwa kwamba kutoka mwaka 2017 kwa maana ya mfumuko wa bei ilikuwa 5.3, napongeza hilo, lakini kwa maana ya 2018 umeshuka mpaka 3.8. Huu mfumuko wa bei na kushuka kwake ni jambo jema, lakini naendelea kuishauri Serikali yangu, namna pekee ya mtu wa kawaida kuliona hilo, usomeke kwenye mifuko yake. Ikisomeka kwenye mifuko, tunakuwa tunaimba wimbo mmoja, wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, najua kwa maana ya malengo ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2018/2019, umeandaliwa kwa kuangalia dira ya 2025, lakini kuna malengo endelevu ya 2030. Ukija katika ukurasa wa 85 kwa maana ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa maana hii ya malengo ya mpango wa bajeti, inasema hivi:

“Baadhi ya vitu ambavyo wamezingatia ni pamoja na masuala mtambuka kama vile jinsia, watu wenye ulemavu, mazingira, UKIMWI, makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi na masuala ya lishe kwa jamii pamoja na maelekezo na ahadi zilizotolewa Kitaifa.”

Mheshimiwa Spika, niendeleo kushauri. Kama kumbe bajeti hii malengo na mipango yake inazingatia suala hilo; masuala ya walemavu, masuala yanayogusa UKIMWI, nilikuwa naomba suala hili liendeleo kusomeka. Walengwa

kwa maana ya walemavu wafike sehemu wakutane na kile ambacho mipango inaelekeza kwamba watu hawa wameguswa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, eneo la UKIMWI naomba niendeleo kushauri, mara nyingi na watu wengine wamekuwa wakiliongelea hili. Wakati tukitenga fedha kwa ajili ya kusaidia masuala ya watu wenye maambukizo na vinginevyo, nashauri eneo la watu wazima kutumia sehemu kubwa ya fedha na walengwa wakawekwa pembeni, jambo hili naliona halina tija. Kwa hiyo, naomba niendeleo kuisitiza, wakati tunazungumzia suala hilo tujaribu kuendelea kuangalia kwamba walengwa, fedha sehemu kubwa iende ikawaguse walengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nami niendeleo kupongeza kama nilivyosema mwanzo. Naunga mkono hoja. Nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Nilitarajia kwenye Wizara kama hii wenzetu wa Kamati ya Bajeti wangukuwa ndio wachangiaji wengi. Kwa sababu ndiyo mmekaa na Wizara hii mwaka mzima kwa niaba yetu; na tulipanga wachumi wengi, wahasibu wengi, na ni ambao tuliadini kufuatana na maandishi yenu kwenye CV zenu kwamba mna *degree* hizo, sasa matokeo yake siwaoni. Majina yote niliyonayo ni ya akina Mzee Sanga na wengine. *(Kicheko/Makofi)*

Itabidi tuiangalie upya hii Kamati, nanyi ndio mnakaa masaa mengi kuliko Kamati nyingine yoyote. Hicho mlichokuwa mnakiangalia mwaka mzima kiko wapi sasa? Mnatuangusha sana. Nyie ndio mnatakiwa mchambue sasa mtuambie, *what is happening?* Kwa hiyo, mlikuwa mnakaa tu huko mnakunywa chai halafu hamna kitu!

Haya Mheshimiwa Lwakaratare halafu Mheshimiwa Riziki ambao wala sio Wajumbe wa hizo Kamati, tuendeleo. *(Makofi)*

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nitoe pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Bilago kwa kuondokewa na mpendwa wao. Pia pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote hususan Chama cha CHADEMA. Pia namwomba Mwenyezi Mungu aweze kumsimamia na kuweka mkono wake kwenye *operation* ya Mheshimiwa Lissu ambayo inasemekana ni ya mwisho ili iweze kufanyika vyema na aweze kupona na kuweza kuungana nasi pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zangu ni mbili ambazo nimetumwa na wananchi wa Bukoba *Town*, ambazo kimsingi zinawagusa Watanzania wote kwa ujumla wao. La kwanza ni suala la *property tax*. Siku chache zilizopita, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ni shemeji yangu, alitoa ufafanuzi mzuri sana kuhusiana na nyumba ambazo zinapaswa kulipa *property tax* na *categories* ambazo zimepangwa.

Mheshimiwa Spika, kuna nyumba ambazo kimsingi, kiutaratibu zilipangiwa kulipa Sh.10,000/= ambazo ni nyumba zilizopo kwenye *squatters* ambazo ni *unsurveyed* na nyumba za ghorofa ambazo zipo katika maeneo hayo. Nyumba hizi za *squatters* ni Sh.10,000/= na nyumba za ghorofa ambazo zipo kwenye sehemu ambazo haziko *surveyed* na wala hazijafanyiwa *evaluation* ni Sh.50,000/=. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ninayoileta hapa, wananchi wa Bukoba wanaamini wanatapeliwa na *TRA*, kwa sababu hivi sasa *TRA* inatoza karibu *almost* nyumba zaidi ya asilimia 70 za ndani ya Mji wakidai kwamba zimefanyiwa *evaluation*; wakati utaratibu uliotumika kuzungumzia hicho kiwango ambacho kinasemekana kilifanyiwa *evaluation* ni kwamba taratibu za Sheria ya Uthamini hazikufuatwa.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba ni watu wameunda kikundi wakawaendea wataalam ndani ya Halmashauri husika. Wanakwenda kwenye nyumba mbalimbali, wao wana-*dictate terms* wana-*dictate* zile *rates* kwamba hii nyumba thamani yake shilingi milioni 50, hii ni

shilingi milioni 100 bila kufuata Sheria ya Uthamini. Kwa hiyo, hivi sasa ni *disaster* na naamini iko katika maeneo mbalimbali ya miji mbalimbali hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, watu wamebambikiwa *rates* ambazo siyo sawasawa na thamani ya nyumba; na nyumba zenyewe ziko vichochoroni. Mbaya zaidi tunajua Sheria ya Uthamini lazima iwe shirikishi, aidha na Uongozi ulioko katika eneo hilo la mitaa, eneo ambalo watu wenyewe, wahusika wenye nyumba hizo, wanapaswa washirikishwe, wanapaswa wataarifiwe. Sasa watu wamekuwa wanakutana na bili za TRA wakishangaa zinatoka wapi, kwa sababu wakati wa zoezi la *evaluation* hawakushirikishwa wala hawajui lilifanyika lini? Kwa hiyo, huu mimi naweza nikausema ni utapeli wa hali ya juu na kwa kweli wananchi wa Bukoba *Town* wamenituma kwamba wanataka maelezo yenye misingi iliyosimamiwa na Sheria ya Tathmini.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo, kwa kuwa kule kuna watafiti wengi, hivi sasa zoezi tunalolifanya, tunakusanya *data* za nyumba ambazo *evaluation* imefanyika kinyemela na baada ya kukusanya hizo *data* tutatafuta ushauri wa hatua gani ya kuchukua na hata ikibidi kuipeleka TRA Mahakamani, kusimamisha zoezi hili mara moja kwa sababu halikufuata utaratibu wa kufanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nyumba zinazotozwa hela, unakuta mtu ni mzee kabisa amestaafu, anaambiwa ile nyumba ambayo masikini amejenga katika mazingira magumu kwa hela ya pensheni mtu anaambiwa atoe Sh.150,000/= kwa mwaka, atazitoa wapi? Kuna nyumba watu wengine wamerithi kutoka kwa wazazi wao ambao wameshafariki, unakuta amebaki mjane, wote hao wanatozwa hela kwa *rates* ambazo kwa kweli ni *unaffordable*, hawana uwezo wa kuzilipa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na majibu aliyoyotoa Mheshimiwa Waziri, namshukuru alitoa majibu ambayo yamesimama vizuri, lakini kwa mazingira ya Bukoba *Town* ni kwamba lile zoezi la *evaluation* ambalo wanadai ndiyo

linasimamia *rates* ambazo zinatozwa na TRA, zoezi halikufanyika katika taratibu za kisheria. Namwomba Mheshimiwa Waziri anapo-*wind-up* azungumzie Bukoba, tutakwenda hivyo au twende na *route* ya kutafuta haki mbele ya vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo kimsingi nalo linalalia huko huko, ni kwamba Mheshimiwa Waziri amekuwa katika takwimu zake na katika vyombo vya Habari na taarifa zinazotolewa na TRA kwamba wanakusanya vizuri, hongera kwa hilo. Kwa mtu anayekusanya vizuri, vilevile kuwepo na vielelezo na taswira na mazingira ya kuonesha anakusanya vizuri lakini pia analipa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa katika bajeti ya Wizara kwa kuwa nimo ndani ya Kamati, kwa nini fedha hazitoki? Mbona Wakandarasi wengi wanadai? Mbona Wakandarasi wanasaini mikataba nje ya wakati? Naomba kabisa Mheshimiwa Mpango, asione haya, pesa inakwenda wapi? Nieleze linalozungumzwa, mimi sina minong'ono, wanasema yeye anabana mno, mpaka *penalty*. Pesa hazitoki. Zina mlango mmoja wa kuingia, lakini wa kutoka ni mwembamba kama ule tunaoambiwa wa kwenda Mbinguni. Kwa nini pesa haitoki? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilifikiria labda hapa tukiwa pamoja na Kambi ya Upinzani na wenzetu wa CCM, kama anatuonea haya, hebu wakiwa kwenye *caucus* huko wazungumze, wanong'one, kwa nini pesa haitoki? Kwa hiyo, maendeleo ambayo tutaendelea kuyazungumza kimsingi yanakuwa ni maendeleo ya vitu, siyo ya watu. Watu wamechacha ile mbaya, maisha hayatamaniki.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanakula mlo mmoja pamoja na kwamba wengine hawakufunga Ramadhani, lakini inabidi wafunge kwa sababu hela haiko katika mzunguko. Watu wa Bukoba wanauliza hela iko wapi? Hela nyingi inayokusanywa, inakwenda wapi? Naomba atupe majibu hapa. Kama ataona hapa kuna soo, wakikutana

huko, najua *caucus* watakutana, hebu awaeleze Wabunge wenzetu wa CCM hela inakwenda wapi? Mbona matatizo! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili sambamba na hilo kuhusu madeni, nawazungumzia wapiga kura...

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Lwakatare. Pokea taarifa.

TAARIFA

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba siyo Watanzania wengi kwamba wanakula mlo mmoja. Watanzania wote tunakula mlo mmoja, ila tunakula mara tatu. Kwa sababu asubuhi uji, mchana ugali, jioni ugali. Kwa hiyo, mlo ni ule ule mmoja, lakini tunakula mara tatu. (Kicheko/Makofi)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, nimepokea na kukupongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia *specifically* madeni ya Wakandarasi wa Mji wa Bukoba na Mkoa wa Kagera ambao wamenituma. Tunazungumzia kwa mfano, Wakandarasi wa Mradi wa REA ambao tunaambiwa mpaka leo wanadai. Kimsingi, bahati nzuri wale Wakandarasi wakubwa wana watu wa kuwazungumzia. Nataka kuzungumzia kwenye *local content*, niite *local content* basi ya miradi hii, kwamba kuna ma-*supplier* wadogo wadogo ambao wanakuwa wanawa-*supply* hawa Wakandarasi wanaowadai. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina ma-*supplier* zaidi ya 20 hapa ambao wamem-*supply contractor* aliyekuwa anasimamia na kuendesha mradi wa REA katika Mkoa wa Kagera. Hawa watu wanadai zaidi ya Sh.1,300,000,000/= hawajalipwa. Wengine majuzi Benki zimetangaza kuwafilisi na kunadisha nyumba zao. Kuna mama mmoja alikuwa ana-*supply* vyakula kwa wafanyakazi wa Kampuni hii, yule mama ameukimbia mkoa kwa sababu ya madeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka watueleze haya madeni yanalipwa lini? Kwa sababu yasipolipwa yana-*affect* hata wengine ambao wapo chini wanao-*supply* vitu mbalimbali kwa hawa Wakandarasi. Kuna bwana mmoja ambaye mpaka katika kituo chake cha mafuta ameshindwa kununua mafuta mengine kwa sababu alikuwa *supplier* wa huyu Mkandarasi, anadai mamilioni ya hela.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapo-*wind-up* atueleze kwa sababu haya madeni hayawa-*affect* hawa Wakandarasi wakubwa tu, yanawa-*affect* hata ma-*supplier* wadogo ambao kimsingi ndio wapo wengi kule chini. Ndiyo maana *circulation* ya hela inakuwa haipo na watu wanaishia kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo naomba Mheshimiwa alifafanue, ni hiki kitu ambacho kinaitwa uhakiki. Nashangaa na nitaomba kwa kweli nipewe *tuition* kidogo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. Mheshimiwa Riziki Lulida, atafatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru nami kunipatia hii nafasi ya kuchangia hoja iliyokuwa mezani. Kwanza nakupongeza kwa kazi kubwa uliyofanya kwa kuunda Tume ya Bunge kuangalia udhaifu uliojitokeza katika makinikia pamoja na uvuvi. Hii imeleta faraja kubwa katika Bunge letu, kuwa sasa hivi Bunge linafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mwanzo lilikuwa Bunge ambalo unaona kabisa lipo lipo lakini naona sasa hivi umeliamsha dude ndani ya Bunge na Bunge liko vizuri. Nakuomba tena, tunataka *Bunge Live* ili hayo unayoyaunda watu wayasikie kule mtaani. Wananchi, wapiga kura wanataka kusikia nini unazungumza, Wabunge wako wanafanya nini? Hii kazi

itasaidia kuweza kuleta uelewa kwa wale watu, watakuwa wanajua kinachoendelea ndani ya Bunge. Hoja za Wabunge wao zinazungumzia nini? Tukikaa humu ndani wananchi hawaoni hayo unayoyafanya. Kwa hiyo, ningeshukuru sana na hilo nalo ungeliamsha ingeleta tija zaidi. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa. (Makofi)

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, naona kuna hoja nzito ya wafanyabiashara, wakulima dhidi ya kuwa na mahusiano mabaya na mabenzi. Benki zimeamua kuwakandamiza wafanyabiashara hasa wakulima. Tumeona katika miaka miwili wakulima wako katika hali ngumu sana, wamelima mazao, lakini baada ya kulima mazao Serikali imewasimamishia maendeleo yao kwa kutokununua mazao yao. Matokeo yake benki hazikai chini kuangalia nini tatizo la hawa wakulima? Matokeo yake sasa hivi kila benki inataka kuuza mali za wakulima, mali za wafanyabiashara. Nafikiri Mheshimiwa Waziri akae chini na watu wa benki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imepunguza riba kubwa sana kwa benki nyingine, nafikiri ni kama 9%, lakini benki hizo badala na wao kupunguza riba, wameongeza riba imekuwa kubwa sana. Imekuwa kubwa kiasi kwamba hakuna mfanyabisahara wa kawaida ambaye anaweza kukidhi haja. Ukiweka pesa wanaweka *percent*, ukitoa pesa wanaweka *percent* na ndani yake kuna udhaifu mkubwa. Nafikiri hata na maeneo haya ya benki yaangaliwe kuna nini? Kama Benki Kuu imepunguza riba, kwa nini bado wao wanaongezea mzigo mkubwa kwa wananchi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hali hii inakatisha tamaa kwa wakulima. Nataka nikupe mfano, nachukua mfano wa wakulima wako wa Kibaigwa. Pale palikuwa na wafanyabiashara wakubwa wa mazao, miaka mitatu wamekutana na *crisis* za mvua na pametokea mafuriko makubwa, wao bado wanaendelea na *interest*, lakini hawaangalii kuwa je, wenzao ambao wamekutana na mafuriko ambayo siyo wao, ni mipango ya Mwenyezi Mungu,

wangekaa chini wakapunguza riba ile ili na wao waweze kufanya biashara. Matokeo yake wanawakandamiza na kutaka kuuza mali zao bila kuangalia nini tatizo.

Mheshimiwa Spika, Kenya, Waziri wa Fedha na watu wa benki wamesimama na wanafanya biashara. Nami nina imani kuwa Mheshimiwa Waziri ananisikia, atasimama na benki na kuangalia wafanyabiashara wakubwa wanaathirika vipi na mikopo ya benki ili kuweza kuisaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia *TRA*. Ukiona mahali ngoma inachezwa sana, basi haikawii kuharibika. *TRA* walileta *EFD machine*. Kuna siku nilifika katika *petrol station* karibu mara mbili, nikifika wananiambia mashine haifanyi kazi. Nikauliza kwa nini haifanyi kazi? Hela zinaendelea kuchukuliwa, lakini zile hela ambazo zinatakiwa ziingie katika Serikali hazingii. Nataka nijue idara ya *ICT* ya *TRA* inafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mpaka Mbunge amekuja kuliona hili suala humu ndani, baada ya siku ya pili tumeona mashine zinafanya kazi, hii ni hujuma. Hujuma kama hamuisimamii itakuwa ni hujuma kubwa sana. Kwa vile *ICT Department* ndiyo inaweza kuingiza *data* ndani ya *program* ya Serikali na kuingizia pato Serikali, lakini kama *ICT Department* ikicheza na ma-*hackers* kwa kufunga hizi *EFD Machines* hizi pesa zote badala ya kuingia katika Mfuko wa Serikali zitaingia katika mifuko ya watu wengine ambao sisi hatuwajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijulize swali, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kumaliza ku-*wind up* aniambie *Department* yake ya *ICT* tiko makini? Huwa ni *network*, maana katika *ICT* inabidi ianzie *TRA*, iende mpaka katika mabenki, iende mpaka *TCRA* kuona je, humo ndani yake kuna nini ili angalau huu uovu, utasema Serikali haipokei mapato, kumbe mapato yanaingia kwa watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la miradi mbalimbali ambayo imesimama kwa muda mrefu. Nataka

nitoe mfano wa *LNG (Liquefied Natural Gas)* ambao uko Lindi. Tulitegemea mradi ule ungekuwa tayari umeshaanza kazi, lakini pamesuasua kwa muda mrefu, hatuambiwi mpaka leo ule mradi umesimama wapi? Huu ni mwaka wa tano wananchi wamechukuliwa maeneo yao hawajalipwa, lakini kinachoendelea hakijulikani.

Mheshimiwa Spika, hii inawapa mwanya wawekezaji kuchukua ile miradi kuipeleka Mozambique. Sasa hivi kila mradi ambao tunaukataa Tanzania, wenzetu Mozambique wanauchukua, matokeo yake badala ya kwenda mbele itakuwa sisi tumesimama na miradi yetu tukiwa na urasimu ambao mimi sijajua, lakini naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu aniambie.

Mheshimiwa Spika, kuna kitengo ambacho ni Taasisi ya *CAG* ya Ukaguzi. Kwa kweli hapa pana mtihani mzito sana. Kuna maeneo ambayo Serikali imeyaachia yasikaguliwe. Kwa nini? Kama Jeshi linakaguliwa na Bunge linakaguliwa, maeneo hayo ndiyo mianya mikubwa ya kupoteza hela ambazo sisi hatuzijui.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano. Wafanyakazi wote wa Serikali mishahara yao inapitia *NMB*. Madaktari mishahara yao inapitia *NMB* na taasisi zote za Serikali zinapitia *NMB*, lakini hapakaguliwi. Sasa hivi nataka kufikia mwisho mpaka binadamu yule au biashara yao imekufa unakwenda kufukua makaburi. Tuache biashara ya kufukua makaburi. Kama ni sheria, walete Bungeni, Bunge lipitie sheria, wakaguliwe *NMB*, *NBC* na taasisi zote ambazo inabidi zikaguliwe. Kama hawakagui ndiyo mianya inapita ya pesa kwenda nje. Kama hawaiangalii mianya hii, leo kama taasisi kubwa, mikopo yote ya Serikali iwe ya wanafunzi, inapitia *NMB*, halafu wanasema hawaikagui, wanalionaje hili neno? Ni hatari kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni lazima *CAG* awe na meno. Sheria ya *CAG* iletwe irekebishwe, apate fedha za kutosha ili awe na uwezo wa kukagua. Ama la, *CAG* anakagua chini ya 40%, ina maana maeneo mengi

anashindwa kukagua. Kama anashindwa kukagua, ni vipi wataweza kujua athari ambazo zinapatikana katika maeneo mbalimbali? Leo hii unamwona CAG anashindwa kukagua maeneo mengine. Hakuna haja ya kufichaficha, tuseme aah, hapa TAKUKURU tusikague.

Mheshimiwa Spika, kwa nini TAKUKURU isikaguliwe? Pesa zinazokwenda pale ni za Watanzania. Matumizi ya pale ni ya Watanzania. Kama watu hawa hawakaguliwi, ndiyo mianya hiyo, maana watu wanatumia pesa bila kukaguliwa. Maana Jeshi wanakagua, ndiyo ambapo nillitegemea ni sehemu nyeti sana, lakini anasema maeneo mengine hatukagui. Hiki ni kigugumizi ambacho hakina maana, naomba Mheshimiwa Waziri atakapoingia katiak ku-*wind-up* anipe majibu kwa nini maeneo mengine yameachwa yasikaguliwe, tunaachia watu tu wanatumia wanavyotaka wao, wanakuwa na viburi vya kutosha? Hivyo naiomba Serikali iifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la barabara. Leo hii Mikoa ya Lindi na Mtwara ndiyo kwenye uchumi. Tunaona uchumi wa Mkoa wa Lindi kwa ajili ya korosho imekuwa ni *green gold* kulinganisha hata na madini mengine, lakini hatuna barabara. Tumekuwa maskini watu wa Mkoa wa Lindi, hapapitiki leo kwenda Liwale, Liwale ina *Selous*, lakini hakuna barabara, Liwale ina korosho, hakuna maendeleo ya barabara, Nachingwea hakuna barabara, Kilwa hakuna barabara. Sasa wanapelekaje uchumi bila kupeleka na barabara? Uchumi utakwenda sambamba na miundombinu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, bajeti iliyopelekwa katika maeneo yale yanayozalisha, Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma inakwendaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida. Nilishamtaja Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Tweve.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa kutupa sisi sote zawadi ya uhai, tupo hapa tunazungumza mambo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza tena na niungane na mwenzangu aliyetangulia kwa wewe jana kupokea ripoti zile mbili na kuzikabidhi Serikalini, Ripoti ya *Natural Gas* na ile Ripoti ya Uvuvi. Tumeona kazi yako na nia yako njema katika kudhibiti mianya yote ambayo inatupotezea mapato katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na niipongeze hotuba yake ambayo kwa kweli imeandikwa vizuri na tumeielewa na ndiyo maana unaona mijadala yote iko moto.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasimama nilipokuwa najiandaa ilinilazimu kwenda kule *Library* nikachukua *Hansard* ya mwaka 2017 ambayo pia wenzetu walikuwa wamechangia. Niseme wazi kwamba nimei-*miss* michango yao na sijui kwa nini mpaka leo hatupati michango ya upande wa pili? Kwa nini nimevutiwa kwenda kuchukua michango yao? Nilitaka kuona mambo waliyoyazungumzia mwaka 2017 leo yameendaje? Mengi waliyokuwa wamelalamikiwa yametekelezeka na lazima niseme wazi kwamba Mheshimiwa Waziri Mpango mambo yako yako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ni moyo wa uchumi na ndiyo maana wote wanaozungumza wanaipiga mawe, lakini tunasahau kwamba kuna mambo mazuri yamefanyika hapa katikati. Mwaka 2017 kipindi kama hiki kila mtu alikuwa analalamika bei juu, walio kwenye Mwezi Mtukufu wa Ramadhani vyakula viko juu, sukari hakuna, mahindi hakuna, mchele ghali; lakini leo kila mtu amekaa raha mustarehe. Kila kitu kinapatikana, Mwenyezi Mungu amesikia kilio chetu, uji upo, mchele upo na sukari ipo. Mambo hayo yote wanadamu tumezoea kila siku kulalamika;

hata mambo mazuri hamwoni sasa? Hata mvua zilizokuja hamzioni? Hata watu wanafuturu vizuri, wakiwepo na Waheshimiwa Wabunge wanafuturishwa kila leo, hawaoni? Bado wanalalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu akiwa na hulka ya kulalamika, hakuna namna unavyoweza kumbadlilisha, lakini namshukuru Mungu mfungo huu umekuwa mzuri. Niseme kwamba na hiyo iweze kumpa pia, ahueni huyu Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende katika ule ukurasa wa 87 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri unaozungumzia uratibu wa mikakati ya kupunguza umasikini. Nilipokwenda *Library* nilichukua pia kitabu cha Wizara hiyo cha mwaka 2017, kama hiki na nikaenda ukurasa huo huo katika uratibu wa mikakati ya kupunguza umaskini. Kilichozungumzwa mwaka 2017, mwaka jana ilikuwa ukurasa wa 76 mwaka huu ni 87, hayapishani sana. Ni mambo mazuri ndiyo, lakini yote ni kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa kawaida ukimwambia unapunguziwa umaskini kwa kuzidi kuboresha au kuandika maandiko ya *SDGs*, maandiko ya *Poverty Monitoring System*, tunazidi kuboresha mifumo, tunazidi kuboresha, haimuingii akilini. Nami pia niliyetumwa hapa na wanawake wa Kilimanjaro wanaonisubiri waone tumepiga hatua kwenye kupunguza umaskini, naomba kutamka kwamba sielewi. Ni kwa nini sasa sielewi?

Mheshimiwa Spika, nilitaraji sasa baada ya wasomi kuangalia hizo *SDGs* waje na pendekezo au waje na maagizo kwa Serikali; jamani, tumeamua kupunguza umaskini, tunaomba au tunaagiza sasa tupeleke *projects* ambazo wananchi watazisimamia na wanawake walio hapa wengi ni Viti Maalum, wanajua ambavyo wanaombwa kule kwenye maeneo yao semina ya kujifunza ujasiriamali, semina za kuboresha maeneo, za mazingira, semina za ufugaji, lakini wanafuga nini? Hakuna mifugo iliyoboreshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wangu wa Fedha akatuzungumzie kunakopatikana mitamba bora, wanawake wakopeshwe. Miaka ya nyuma Mwalimu Nyerere peke yake katika awamu zote aliweza kutoa *projects* ambazo zinafanya kazi watu wakarejesha. Ilikuwa inaitwa kopa ng'ombe lipa ndama; na mpaka leo ndiyo iliyowatoa watu. Watu waliweza kuboresha maisha yao, wanapata maziwa, wanapata samadi, wanapata nyama nzuri na ngozi.

Mheshimiwa Spika, ni Mwalimu tu katika awamu zote tano, yeye alitoa *projects* na zikalipa mpaka leo. Ndiyo akaweza kuchanganya wale ng'ombe wa kiasilia na ng'ombe wa kisasa. Maeneo mengi yaliyoboresha kipato ni yale ambayo yaliweza kufaidi mradi huo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango aangalie ni *projects* zipi zitaweza kwenda kuboresha kipato cha akinamama?

Mheshimiwa Spika, tumeona wanawake wanaingia kwenye *VICOBA*, Serikali inasema kwamba inakwenda kusimamia *VICOBA*, mnasimamiaje *VICOBA* ambavyo hamjui vimeanzishwaje? *VICOBA* hivyo ni vya kudunduliza, amechangia mmoja akasema na ile hela ya *VICOBA* sasa inakwenda kwenye kucheza kamari. Tunafanyaje? Tunatokaje hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba wanawake hawa wapewe elimu ya *VICOBA* kila mara. Hapa wenyewe sisi, wengi wa Wabunge wako ni wasomi, lakini kila leo umejitahidi kutuletea semina za mambo mbalimbali ili tuweze kuendana na wakati. Sasa wanawake wale tunawapelekeaje semina hizo? Haitoshi kabisa kuzungumzia vitu vyao walivyoanza halafu tukasema tunasimamia *SACCOS*. Unasikia Serikali inaingia kwenye *SACCOS*. *SACCOS* ni uanzishaji wa hiari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Serikali imeweza kwenda kuangalia wasiuze zile mali za *SACCOS*, lakini uanzishwaji wa *SACCOS* ni wa hiari. Wenyewe wanakaa

wanakubaliana. Maeneo ambayo SACCOS zimeshamiri ni kule ambako hazijaingiliwa. Leo Serikali ukienda ukaingilia, umeharibu.

Mheshimiwa Spika, nakuomba, dakika chache zilizopita umesimama umetoa amri. Najua, amri yako au *your wish* ni kutekelezwa na ikitekelezwa kwenye hili jumba lako Tukufu wewe ndio umesema. Naomba siku moja ikupendeze, zile hela zinazotolewa au zilizowahi kutolewa na Marais siku za nyuma zikaenda kwa wanawake, zikaenda kukopeshwa, halafu zikaishia ziliko, mimi najua ziko kwenye benki kwenye *suspense accounts*. Tuma Tume yako fedha hizo zikakaguliwe, iwe ni NMB, iwe ni NBC, iwe ni CRDB, zile hela zirudi kwenye mzunguko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zile hela ni *revolving funds*, zirudi. Hazina inajua ni kiasi gani kilitoka. Mara ya mwisho tulipata mabilioni ya JK, mpaka leo yako wapi? Waliojifurahisha wameyafungia, zime-*lock* mahali. Utashangaa hata viongozi wakubwa au wake wa viongozi walienda na wao wakakopeshwa. Hivi walikuwa wanastahili hizo hela? Nakuomba, siku itakapokupendeza zile hela zirudi kwenye mzunguko, wanawake wakopeshwe, vijana wakopeshwe hela hiyo ikombolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti tumeelezwa wazi ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, hili ni jambo jema. Naomba ubia huu usimamiwe na Serikali sasa iwe makini kuangalia ni jinsi gani ubia huu unaendeshwa. Tuna bahati moja nzuri sana ya kupata Wakaguzi wa Serikali ambao ni makini, ambapo tulikuwa huko nyuma na Uttoh, sasa hivi tuna Profesa Assad. Ukiona ripoti zake, ziko wazi, hakuna anapoficha. Pamoja na madaraka yake hayo makubwa, nafasi yake amepewa; tukitaka sasa kujua *value for money* kwenye *projects* inashindikana maana naona wataalam hawa hawapo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi ameagizwa, lakini amepewa majukumu na amefungwa mikono, hana namna ya kuajiri watu ambao wana uelewa kwenye eneo hilo. Sasa

inamwia ngumu. Tunamhoji tunasema, aah, umemaliza ukaguzi sasa tunataka tuwe tena na ukaguzi ule mahususi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond kwa mchango mzuri sana. *(Makofi)*

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga hoja mkono. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango mzuri sana ulionao. Tulikuwa tunatamani kuendelea kukusikiliza. Mheshimiwa Rose Tweve tafadhali.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu siku ya leo. Awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Ni matumaini yangu Watanzania wanatambua mchango mkubwa ambao wanautoa kwenye Wizara yao na kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nina jambo moja tu ambalo nitapenda kuliongelea siku ya leo ambayo ni *issue* ya hawa ndugu zetu wa *TIRA (Tanzania Insurance Regulatory Authority)*. Mwaka 2009 Bunge lako lilipitisha Sheria Ndogo, Sheria ya Bima Na. 10 na lengo lilikuwa ni kutatua changamoto kwa wananchi, hasa pale wanapopata ajali, kama mtu amepoteza maisha, basi ndugu zao waweze kupata fidia na kama kuna upotevu wa mali, basi waweze kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyokiri kwenye hotuba yake ukurasa wa 60 kumekuwa na upungufu mkubwa kwenye chombo hiki ambacho kilipewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu taratibu zote zinazohusu bima nchini. Kwenye ukurasa wa 60 Mheshimiwa Waziri anasema,

Wizara imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi hasa ya ucheleweshaji wa fidia pale wanapopatwa na majanga. Hiki kimekuwa ni kilio kwa nchi nzima hasa wananchi wangu wa Mkoa wa Iringa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kimekuwa na upungufu mkubwa, kwanza hakijulikani na hao wachache wanaokijua chombo hiki, *notion* iliyopo inakuwa ina-*benefit* sana makampuni ya *Insurance* badala ya wananchi wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kiliundwa kuhakikisha kinaratibu shughuli zote za bima, lakini suala hili nililuliza ilikuwa tarehe 3 Aprili, nikataka kujua takwimu ni ajali ngapi zimetokea na watu wangapi walikuwa wamelipwa stahiki zao? Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo hapa kuanzia 2016 - 2018 ni majeruhi na vifo ilikuwa ni zaidi ya 14,000. Mpaka tarehe hiyo 3 Aprili, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatolea hapa ufafanuzi ni watu 1,500 tu ndio ambao walikuwa wamelipwa stahiki hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hiki chombo kifanyiwe mapitio, kumekuwa na upungufu mkubwa sana. Kuna hata hili suala ambalo wameweka la Msuluhishi wa Bima. Chombo hiki hakitambuliki na ofisi yao ipo moja tu Dar es Salaam. Sasa kwa hali halisi Mheshimiwa Waziri mtu atoke sijui Makete, Njombe, Iringa aende kwa huyu Msuluhishi wa Bima inakuwa ni kazi kubwa. Kwanza umbali na pili ni gharama.

Mheshimiwa Spika, juu ya hilo, kuna upungufu, huyu Msuluhishi wa Bima anataka kuonana na mdai mwenyewe, hawaruhusu Mwanasheria au Mwakilishi yeyote kukutana na chombo hiki. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu hawa *TIRA* wako chini ya Wizara yake, hebu tuangalie tena kwa namna ya utendaji wao kazi. Moja, watoke maofisini waweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, elimu ya Bima bado ipo nyuma kwa wananchi wetu, wengi wanajua tu ni Bima pale ajali

inapotokea. Kuna wananchi wengi mkoani kwetu Iringa pale wanajishughulisha na shughuli nyingi za kilimo, mashamba yanaungua pale lakini hawajui bidhaa ambazo zinapatikana kwenye hizi huduma za bima ili pale wanapopata majanga waweze kupata stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kwanza tupitie sheria, kama kuna upungufu wowote ziletwe hapa zipitiwe ili tuweze kufanya mabadiliko tuwasaidie Watanzania. Pia *TIRA* wapewe pesa za kutosha. Najua sasa hivi wameanzisha *Website* yao, nawapongeza kwa hilo, *at least* inafanya kazi, watu wanaweza ku-*check* wamelipwa *premium* zao wanaweza kufanya *follow-up* kujua kama zimelipwa na hayo makampuni. Kwa hiyo, wapewe pesa za kutosha, watoke maofisini wasiishie Dar es Salaam, waweze kufika sehemu mbalimbali hata zile za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hizi dakika chache zilizobaki, naomba pia niwasemee Walimu. Kumekuwa na manunung'uniko makubwa juu ya kulipa malimbikizo yao. Tunajua wana mchango mkubwa sana kutuandaa na na kutulinda. Wengine tumefika hapa Bungeni ni mchango wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa ufafanuzi mzuri asubuhi, tunaomba kuendelea ku-*keep update* kuhakikisha tunalipa hizi stahiki zao kwa wakati, wanafanya kazi kubwa kuhakikisha wanajenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rose Tweve. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Rose Tweve ni Mbunge wa Mkoa wa Iringa. Yuko vizuri, eeh! Sawasawa kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Saul Amon uwe mchangiaji wa mwisho leo.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi adimu ndani ya Bunge hili kuchangia. Kwanza kabla ya yote, naunga mkono hoja nisije nikasahau. Pili, naomba ku-*declare interest* kwenye uchangiaji wangu kwa sababu nitachangia kuhusu biashara nami ni mfanyabiashara, kwa hiyo na-*declare interest* mapema kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka kutoa pongezi kwa Serikali yangu ya Tanzania hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa ununuzi wa ndege. Pamoja na kwamba kuna watu wanaopinga, lakini nawashangaa kweli kweli kwamba nchi inaweza kuwa bila ndege! Hata nchi ndogo zina ndege, sisi tusiwe na ndege; kwa kweli nampongeza sana na hili wanipelekee hiyo taarifa kwamba nampongeza kutoka ndani ya moyo wangu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, kuna wenzangu wamechangia kuhusu *property tax*. Nataka nimkumbushe tu Mheshimwa Waziri wa Fedha kwamba wakumbuke hili alilochangia mchangiaji mwingine simtaji jina, lakini Mheshimiwa Rais alilizungumza, akawaambia nyie wakusanya kodi mnafanya kodi zisikusanywe kwa sababu mnaweka kodi zisizobebeka. Hili amezungumza mchangiaji mwenzangu amesema kwa sisi viongozi; kiongozi akizungumza yanakuwa ni maamuzi sahihi na kama lina matatizo au ukakasi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, basi lije hapa lizungumzwe ili hizo kodi za *property tax* ziweze kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka aliongea Mheshimiwa Rais, sio mtu mwingine; akaongea bei mpaka akaongea akaweka mfano, nyumba ya ghorofa changisheni Sh.100,000/= sijui Sh.50,000/= lakini wanawaambia watu kodi ambazo haziwezi kubebeka. Ndiyo kweli aliyokuwa anazungumza mchangiaji mwingine aliyepita, wanaleta makadirio ya ajabu. Anakwambia ulipie kodi shilingi milioni 30 wakati hilo jengo wewe hupati hata shilingi milioni 30 kwa mwaka. Wanawatwisha watu mizigo ambayo haiwezi kubebeka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, aliyeongea ni Mheshimiwa Rais na watu wote walisikia. Tunachotakiwa ni kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na naamini kwamba kodi hii ikiwa ni ya kiasi ya watu kutaka kwenda kulipa wenyewe italipika, lakini kwa haya mamilioni yanayotajwa kwa kweli sidhani kama watu wengi, kama alivyozungumza mchangiaji mwingine, mzee kastaafu, unamwambia akalipie Sh.200,000/=, ndivyo walivyoenda kukagua na kutoa tathmini ya hiyo nyumba yake. Kwa kweli ni ghali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna haya matatizo na vikwazo katika biashara tunazozifanya na ndiyo maana nime-*declare interest*. Kuna hizi taasisi za umma zinaingiliana mno na zinaenda zote kwa pamoja; lakini nitazungumza mojawapo ambayo ni hii ya uingizaji wa mizigo. Unakuta, *TFDA*, kwa mfano, tunaweza kuiondoa *TRA*. Sasa hivi katika watu wanaofanya kazi nzuri kupita maelezo, ni *TRA* lakini vikwazo vinavyowekwa na hizo Idara nyingine za Serikali ndizo zinazofanya uchangiaji wa uchumi kukua upungue. Kwa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitazungumza katika eneo langu la vipodozi. Nchi nyingi kwenye vipodozi wanaoshughulikia ni watu wanaoshughulika na afya. Hapa kwetu naamini kwamba *TFDA* ndiyo wanaoshughulika na mambo ya dawa, vyakula pamoja na vipodozi. Unakuta *TFDA* wamekupa *certificate*, hawana matatizo. Wamekupa, wanakwambia kabla hujaingiza mzigo wako, lete tuukague, tuupime, tunakupa *certificate*.

Mheshimiwa Spika, unapewa *certificate* na *TFDA*, unayo. Unaenda kuleta mizigo, *TBS* wanakwambia huu mzigo haufai. Hapo wanakinzana mno na ndiyo maana wamesababisha watu wengi wapite porini. Siyo watu wote wana nguvu za kuweza kupita moja kwa moja. Naomba hilo liangaliwe na hapa siwezi kulizungumza sana kwa sababu nilikuwa nimekuja na hayo mawili. Pongezi kwa Mheshimiwa Rais kuhusiana na *property tax* na hiyo ya mambo ya kupingana kwa Idara za Serikali. Kwa kweli zinapingana sana

kiasi kwamba wale wadogo wadogo ambao wamekuja kabisa na kwamba wamelipia wana karatasi za *DFTA*, lakini huyu anakataa. Kwa hiyo, unakuta wanakinzana.

Mheshimiwa Spika, *TRA* wako *very efficient*, unakwenda unafika siku tatu. Maana tulikuwa tunachukua wiki tatu au nne, lakini sasa hivi *TRA* siku mbili au tatu wamemaliza kazi yao. Unaanza kupiga kwata huku *TFDA*, wamemaliza; unaanza na *TBS*. *TBS* umemaliza nao wanakwambia kuna vipimo. Jamani, Kampuni iliyotengeneza hiyo mizigo ni ya Kimataifa, nittoa tu mfano labda *Procter and Gamble*, watengenezaji wakubwa ambao wako katika kila nchi na vipimo vinajulikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu anakwambia lazima tupime tu hii chupa kama kweli ni *mills* 50, naye umlipe. Tupime hii chupa ni *mills* 100 naye umlipe. Ni kweli kabisa na siyo kwamba nazungumza kwa kuambiwa, ni vitu ambavyo navisikiliza. Kwa hiyo, wangekaa pamoja ili wahakikishe kwamba tunafanya shughuli za uzalishaji na kukusanya kodi iwe rahisi. Itakuwaje rahisi? Ni kwa kuchukua hizi mamlaka kwamba wewe ndio utashughulika na hili, wewe ndio utashughulika na hili, kuliko kila mmoja huyu kikwanzo, huyu hapana.

Mheshimiwa Spika, nitampa Mheshimiwa Waziri mifano mingi lakini hapa muda sina, kwa hiyo, muda nitautafuta mwenyewe nimpelekee mifano nimwambie kwamba na hawa wanamkwamisha kukusanya mapato na ndiyo sababu ya watu kupita porini, siyo kwamba watu hawapiti porini na vitu havingii.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni kubwa, mipaka yake ni mikubwa. Wewe mwenyewe ukiangalia kutoka Mombasa uje ufike Mtwara, utoke Mtwara umalize yote Malawi; utoke Malawi uende Zambia; yaani mpaka ni mkubwa sana. Nakumbuka tukirudi huko nyuma, kulikuwa na uongozi uliwahi kulegeza, walikuwa wanakusanya mapato makubwa sana. Vikwazo havileti mapato, wala kodi kubwa haileti mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, naomba kumalizia, nalo hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakushukuru kwa sababu kwanza namfahamu ni rafiki yangu kwa muda mrefu, mkaliangalie. Vipodozi siyo kweli kwamba ni anasa, vipodozi siyo sigara wala siyo pombe. Kama siyo sigara wala pombe na kila aliyepo hapa ndani hakuna ambaye hakupakaa kipodozi. Wanapoweka *tax* kubwa namna ile mpaka na *excise duty* utafikiri unauza sigara au pombe kali, hawamtendei haki huyu mlaji wa mwisho. Mimi nitaleta, lakini atakayeumia ni huyu aliyemo humu. Sasa wanaponiwekea hiyo kodi kubwa...

SPIKA: Wabunge wanawake mbona hii hoja nilifikiri mtaiunga mkono! (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Spika, siamini hata kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango anataka watu wanuke vikwapa humu ndani, haiwezekani. Kwa hiyo, vipodozi, nataka nimwambie kabisa siyo kitu cha anasa. Nenda nchi yoyote; nenda Amerika, nenda Ulaya vipodozi vinaingizwa kwa sababu wanajua faida yake, hakuna asiyepakaa. Kwa hiyo, waangalie hilo na waliangalie vizuri sana. Hayo mambo matatu; Idara zinazokinzana wakae pamoja...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Saul.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Saul. Nilikuwa najaribu ku-*imagine* siku moja vingekosekana vipodozi kabisa, halafu na Waheshimiwa Wabunge wote ikabidi waje hapa bila kipodozi hata kimoja, huenda wengine tusingeweza kuwatambua. Spika anasema nani huyu? Nani?

Mheshimiwa Mbaraka Dau kwa dakika zilizobaki, unaweza ukazitumia? Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MBUNGE FULANI: Ametoka.

SPIKA: Ametoka. Basi nina dakika kama tano. Basi hakuna aliyote tayari, mtamalizia kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawashukuru sana kwa michango yenu. Kesho tutaendelea na uchangiaji wa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aliyoiweka mezani na jioni kama saa hizi tutakuwa tunaifanyia uamuzi kuhusiana na hoja hiyo. Nashukuru tunakaribia kumalizia Wizara, hii ndiyo huwa inafunga geti.

Sasa toka tulivyoanza shughuli hizi za Bunge hili la Bajeti pamekuwa na zoezi la kushika shilingi ya mshahara wa Waziri. Sikutaka kusema mapema, lakini leo niseme kidogo, siyo wote tunafahamu, maana ya kushika shilingi ya Waziri.

Katika Jumuiya ya Madola ambako ndiko utaratibu huu ulikoanzia, unaitwa kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa jambo la Kisera na kadhalika. Hivi jaribu tu ku-*imagine* kwamba kweli shilingi Waheshimiwa Wabunge mmekubali kwamba ushikwe. Kwa hiyo, Waziri akipata mshahara wake *minus* shilingi moja, ina *impact* gani kwa Mheshimiwa Waziri? Haina maana yoyote, si ndiyo! Kwa nini kwenye Mabunge haya kuna hicho kitu kinaitwa kushika shilingi? Ndicho ninachotaka kukielezea kwa dakika chache hapa.

Ni kwamba katika uzoefu huo wa haya Mabunge yaliyo mengi, kama Mbunge akishika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, halafu Wabunge mlio wengi mkaunga mkono kabisa kwamba Waziri huyo, shilingi hiyo ikatwe, itoke kwenye mshahara wake; hoja hiyo itapita *minus* shilingi moja, lakini maana yake na tafsiri yake ni kwamba Waziri huyo anatakiwa muda mfupi baadaye ajiuzulu. Sijui kama wengi mnajua, ndiyo hivyo. Hiyo maana yake, Wabunge hawana imani na Waziri huyo. Ndiyo tafsiri yake ilivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wengi tunashikaga tu, tunafanya kama utani hivi na nini, lakini kwa sababu mimi huwa najua shilingi

itarudishwa, kwa hiyo, huwa sina wasiwasi. Ni vizuri mjue kuanzia leo kuwa ni *indicator*; na ndiyo maana inatakiwa usimame kwa jambo la msingi kwa kweli siyo tu nashika shilingi, nashika shilingi. Siyo kitu cha kucheza kucheza nacho hivi. Kwa sababu kama kweli wenzako wakikuunga mkono, maana yake kwa kweli umemweka pabaya sana Mheshimiwa Waziri anayehusika na Wizara hiyo.

Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hivyo sina maana sasa ndiyo muanze mchezo huo, kwamba mkishakuwa na kisasi, basi inatumika hii. Hapana, hatuitumii kulipa kisasi wala nini, ni kitu *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mkuchika, Simba wameshinda huko leo. Rafiki zetu wa Yanga jana wamerudi, basi tunawakaribisha yumbani, hakuna shida. (*Kicheko/Makofi*)

Waheashimiwa Wabunge, kuna pochi hapa Mbunge aliisahau. Jinsi ilivyo nadhani inaweza ikawa ni ya Mbunge mwanamke, lakini ina pesa nyingi kweli humu ndani. Kabisa kabisa. Kwa hiyo, mwenye pochi yake na pesa hizi atakuja kuchukua mezani kwa Makatibu hapa baadaye. Hirizi hamna, ni pesa tu. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa ushirikiano mliotupatia kwa siku ya leo. Niseme tu kwamba sasa tumefikia mwisho wa shughuli zetu kwa siku ya leo. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(*Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi*)